**27 JUNI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 27 Juni, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA**: Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance Bill, 2024)*.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, inaonekana wajumbe wako kwenye kikao, lakini sasa atafutwe mmoja aje asome hapa kabla hatujaendelea. *(Makofi)*

**MHE. FLATEI G. MASSAY K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance Bill, 2024)*.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Flatei Massay.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 706

### Hitaji la Vifaa Tiba Vituo vya Afya vya Kifanya na Makowo – Njombe

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba katika Vituo vya Afya vya Kifanya na Makowo vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024 Halmashauri ya Mji wa Njombe ilipokea shilingi milioni 450 ambayo ilitumika kununua vifaa tiba kwenye vituo vya afya vya Kifanya na Makowo. Vituo hivyo vimeshapokea vifaa tiba muhimu vinavyotoa huduma ikiwemo upasuaji wa dharura kwa akinamama wajawazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inashughulikia upatikanaji wa *generator* kutoka Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya vituo hivyo ambapo kiasi cha shilingi milioni 40 kimeshalipwa. Aidha, Serikali itaendelea kuratibu na kutenga bajeti ya ununuzi wa vifaa tiba ambavyo vitapelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini vikiwemo Vituo vya Afya vya Kifanya na Makowo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote tunaishukuru sana Serikali kwa kutupa vifaa tiba hivi, na vituo hivi viwili vya Makowo na Kifanya vimejengwa kwa nguvu za wananchi, michango ya Mbunge na Halmashauri yetu ya Mji wa Njombe. Nina maswali mawili, la kwanza, bado hatuna *dental unit* kwenye vituo vyote viwili; ni lini sasa Serikali itafanya utaratibu ili tuweze kupata vifaa vinavyohusiana na tiba ya kinywa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Halmashauri ya Mji wa Njombe imeendelea kujenga vituo vingine na sasa tumejenga kituo cha Iwungilo na Mji Mwema kwa nguvu za wananchi na halmashauri yetu, ni lini Serikali itatupatia vifaa tiba kwenye hivi vituo vipya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nirejee kuwapongeza wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa kuendelea kuchangia nguvu zao, lakini pia

Halmashauri ya Mji wa Njombe, kwa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya, jambo ambalo ni muhimu sana, Wakurugenzi kote nchini wajifunze kutoka Halmashauri ya Mji wa Njombe kwa sababu wamekuwa wakitumia sana fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa vituo badala ya kutegemea fedha za Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya afya ya kinywa na meno kwa maana ya *dental chair* na *dental unit* kwa ujumla nimhakikishie Mheshimiwa Mwanyika kwamba tumeshaweka mpango wa kununua vifaa tiba vile ambavyo vinahitajika kwa ajili ya matibabu ya huduma za dharula hususan huduma za upasuaji wa akinamama wajawazito na huduma za watoto ambapo Kifanya na Makowo tayari mmeshapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awamu inayofuata katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 66.7 kwa ajili ya vifaa tiba na miongoni mwa vifaa tiba ambavyo tutavileta katika vituo hivyo ni vifaa kwa ajili ya huduma ya afya ya kinywa na meno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu suala la vituo vya afya viwili ambavyo vimejengwa, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kupeleka vifaa tiba kwa ajili ya vituo hivyo ili vianze kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, naipongeza Serikali kwa kutujengea vituo vya afya vya Kanyigo na Kakunyu pamoja na hospitali mpya ya wilaya. Sasa, je, ni lini Serikali itatuletea vifaa tiba vya kutosha ili tuweze kutoa huduma stahiki kwa wananchi wa wilaya ya Misenyi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, ahsante

sana, ni kweli kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa miundombinu ya huduma za afya za msingi kwa kujenga hospitali za halmashauri zaidi ya 126 ndani ya miaka minne, ujenzi wa vituo vya afya zaidi ya 878 na zahanati zaidi ya 2,000 ikiwemo halmashauri ya wilaya ambayo Mheshimiwa Mbunge anatoka, Misenyi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba Serikali imeshapeleka fedha kwenye halmashauri zote 184. Kati ya shilingi milioni 450 mpaka shilingi bilioni 1, ukubwa wa fedha unategemeana na idadi ya vituo vilivyojengwa lakini pia na uhitaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, Misenyi wameshapata fedha lakini kwenye bajeti ya mwaka huu ujao 2024/2025 tutahakikisha vituo hivyo vya afya ulivyovitaja tunapeleka vifaa tiba ili vianze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 707

**Kudhibiti Matumizi ya Mifuko Myepesi ya Plastiki**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza Khamis.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kwanza, ulikuwa ni kutoa elimu kwa Umma kuhusu athari za matumizi ya mifuko ya plastiki; Pili, Serikali ilipiga marufuku uzalishaji, matumizi, uingizaji, usambazaji na usafirishaji nje ya nchi mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 01 Juni, 2019 na tatu, Serikali ilitunga kanuni za kupiga marufuku mifuko ya plastiki za mwaka 2019 kupitia Tangazo la Serikali Na.394 la 2019 ili kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki isiyofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa mamlaka na taasisi zote za Serikali kuimarisha na kuwezesha vitengo vyake vinavyosimamia utekelezaji wa marufuku ya mifuko ya plastiki ili viweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 na kanuni zake. Aidha, naomba Asasi za Kiraia pamoja na wananchi kwa ujumla kushirikiana na Serikali katika kupambana na matumizi ya mifuko ya plastiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimepokea majibu ya Serikali; imekuwa mashaka na mtihani mzito, mazingira yanachafuka kwa vifungashio na plastiki mbalimbali ambapo ardhi pia inaharibika na wanyama wanakufa kwa kumeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongezea meno sheria ambayo ipo ili kuwabana waharibifu hawa na kuwapa adhabu kali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni hatua gani Serikali itawachukulia wenye viwanda ambao bado wanaendelea kutengeneza mifuko myepesi na mifuko iliyopigwa marufuku ambavyo inachangia kuharibu mazingira yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu letu la msingi kwamba sheria ipo, ambayo inasimamia matumizi mabaya ya mifuko ya plastiki, na Sheria hii tayari tumeiundia timu maalum na inasimamiwa na inatekelezwa vizuri, tayari sheria hii imetuelekeza tuwe tunafanya doria na hivyo tunafanya. Pia, sheria hii imeelekeza tuwe tunachukua hatua na tunachukua. Sheria hii imetuelekeza tuwe tunasimamia kikamilifu utekelezaji wa sheria hii na sheria ipo na inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa nataka kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wenzetu wa *NEMC* ambao wanafanya kazi kubwa katika utekelezaji na usimamizi wa sheria hii. Sasa kama Mheshimiwa anahisi kuna haja ya kuiongezea meno basi wazo tumelichukua ili tuone namna ambavyo tunaweza tukaongeza baadhi ya vitu vya kuongeza usimamizi wa mifuko ya plastiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanda tunafanya kazi kubwa, tayari viko viwanda tumeshavifanyia doria kwa ajili ya kuona namna ambavyo wanatengeneza hiyo mifuko. Lakini tumeshaanza hatua nyingi sana za misako na hatua nyingine zikiwemo za kutoa faini, kufunga kabisa, kutoa onyo, pamoja na kuwapa elimu wamiliki wa viwanda na tayari viko viwanda ambavyo tumeshavichukulia hatua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nimuambie tu kwamba tutaendelea kufanya kazi hii ili kupunguza hii athari kubwa ya ongezeko la mifuko ya plastiki katika jamii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; je, Serikali inatumia njia gani kuelimisha wananchi juu ya athari ya mifuko hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA)**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Abdul kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, baada ya sheria hii kuwepo, kwa sababu sheria imeelekeza tuwe tunatoa elimu kwa wananchi kupitia njia mbalimbali. Kwa hiyo, zipo njia mbalimbali za vyombo vya habari tunazotumia ikiwemo televisheni, redio, magazeti na namna nyingine. Pia, tumekuwa tunawakusanya wadau hasa wamiliki wa viwanda tunakutana nao kwa pamoja na kuwapa elimu namna ambavyo wanaweza wakapunguza, au ikiwezekana wakaondoa kabisa changamoto ya kuzalisha mifuko ya plastiki kwa sababu imekuwa inaleta athari kubwa kwa jamii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Omar, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha vifungashio mbadala ya mifuko hii ya plastiki inapatikana kwa wingi hapa nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA**: Mheshimiwa Spika, nataka Mheshimiwa Maryam afahamu kwamba kuna vifungashio, lakini pia kuna mifuko ambayo imependekezwa na hiyo ndiyo ambayo haichafui mazingira. Sasa, vifungashio vitaongezeka kwanza kwa mujibu wa sheria kwa sababu viko vifungashio ambavyo vimeruhusiwa kisheria na viko vifungashio ambavyo vipo vinasambaa huko ambavyo havijaruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili kifungashio kiwe kisheria, kwanza kiwe kina nembo ya kampuni husika, maana yake tukione hiki ni *Chilo Company* ili hata ikitokea kifungashio kimeenea tunajua tumfuate nani ambaye amesambaza vifungashio hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kikubwa ni kwamba tutaendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii, hasa wenye viwanda,

watengeneze vifungashio ambavyo vimeruhusiwa ili viweze kuwa vingi na tuondoe kabisa vifungashio ambavyo haviko kisheria katika jamii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 708

**Mradi wa Umeme Kata ya Makurunge – Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza: -

Je, lini mradi wa umeme katika eneo la Kitume Kata ya Makurunge - Bagamoyo utaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini yaani *REA* imeendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika maeneo ya Bagamoyo ambapo katika Kata ya Makurunge eneo la Kitume, *REA* inatekeleza mradi uitwao *Electrification of Small-Scale Mining, Industries and Agricultural Areas in Mainland Tanzania* kupitia mkandarasi aitwae *M/s Dieynem Company Limited*.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulioanza mwezi Machi 2023, umefikia asilimia 57 ambapo kwa sasa mkandarasi amekwisha simika nguzo kwa umbali wa kilometa 9. Mkandarasi anaendelea na kazi iliyobaki baada ya kusimama kutokana na maji ya mvua kujaa katika eneo kubwa ambalo mkandarasi anafanyia kazi. Mradi unategemea kukamilika mwishoni mwezi Desemba, 2024. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, katika Kitongoji cha Changwahela kilichopo katika Kata ya Mapinga, mradi kama huo wa kupeleka umeme katika migodi ya wazalishaji chumvi umefanyika lakini wananchi wa kitongoji hicho hawajapata umeme. Je, ni lini sasa Serikali itawapatia umeme wale wananchi walio katika kitongoji hicho ili na wao waweze kufaidika na huduma hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge, katika hiki kitongoji ambacho kipo katika Kata ya Mapinga, Mheshimiwa Mbunge, tumepokea changamoto hiyo na tutaenda kufanya *survey* kuona ni namna gani tutaweza kufikisha umeme katika kitongoji hiki na wananchi hao waweze kupata umeme wa uhakika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Jimbo la Mbagala litaisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Abdallah Chaurembo. Nimhakikishie kwa kweli siyo kama ilivyokuwa mwaka jana, kwa kiasi tumepunguza kukatiwa kwa umeme katika Jimbo la Mbagala. Lakini, Mheshimiwa Mbunge, tunatekeleza mradi wa kuongeza transfoma pale kwenye kituo cha kupooza umeme cha Mbagala.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tukimaliza mradi huu wa kupanua kituo kile cha kupooza

umeme pale Mbagala, basi tutakuwa tumemaliza kwa kiasi kikubwa changamoto ya kukatika kwa umeme. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge atupe subira kidogo ili tuweze kukamilisha mradi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum…

Mheshimiwa Mbunge rudi kwenye kiti chako tumalize maswali kwanza, ahsante sana. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, sasa aulize swali lake.

Na. 709

**Mauaji Kutokana na Wivu wa Kimapenzi**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na vitendo vya ukatili ikiwemo mauaji yanayotokea kwenye jamii kwa sababu za wivu wa kimapenzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mikakati mbalimbali inayolenga kutokomeza ukatili dhidi ya watoto hapa nchini, mikakati hiyo pamoja na:-

(i) Kuboresha vituo vya huduma kwa wateja ili kuwawezesha wananchi kupata elimu na kutoa taarifa za vitendo vya ukatili kwa wakati;

(ii) Kutoa huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia kwa jamii na kutoa hifadhi ya dharula kwa manusura wa vitendo vya ukatili;

(iii) Kuratibu Madawati ya Jinsia katika maeneo ya umma na kuwawezesha wananchi kiuchumi;

(iv) Kuimarisha uendeshaji, usimamizi na uratibu wa mabaraza ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo imebainishwa katika Mpango Kazi wa Taifa wa Pili wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto pamoja na Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 kwa lengo la kukabiliana na vitendo vya ukatili ikiwemo mauaji yanayotokea kwenye jamii kwa sababu za wivu wa kimapenzi.

Mheshimiwa Spika, ni pamoja na kuboresha vituo vya huduma kwa wateja, ili kuwawezesha wananchi kupata elimu na kutoa taarifa za vitendo vya ukatili kwa wakati, kutoa huduma za afya ya akili na msaada wa kisakolojia kwa jamii. Kutoa hifadhi ya dharura kwa manusura wa vitendo vya ukatili, kuratibu madawati ya jinsia katika maeneo ya umma na kuwawezesha wananchi kiuchumi, kuimarisha uendeshaji, usimamizi na uratibu wa mabaraza ya usuluhishi na migogoro ya ndoa.

Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo imebainishwa katika Mpangokazi wa Taifa wa pili kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, pamoja na Sera ya Jinsia ya Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 kwa lengo la kukubaliana na vitendo vya ukatili, ikiwemo mauaji yanayotokea kwenye jamii kwa sababu ya wivu wa kimapenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, wakati ukisema namba ya swali lako, umesema 704 badala ya 709. Kwa hiyo, inabidi kumbukumbu zetu za Bunge zikae sawa. Hayo ndiyo majibu umepewa, sasa una nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo; nimeona mikakati ya Serikali na ni mizuri, lakini sijaona mkakati wa kuishirikisha jamii yenyewe katika ulinzi dhidi ya vitendo vya udhalilishaji. Sasa, je, Serikali haioni haja ya kuishirikisha jamii moja kwa moja katika ulinzi dhidi ya vitendo hivi kama ambavyo wanafanya wenzetu wa Jeshi la Polisi katika dhana ya ulinzi shirikishi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, vitendo hivi kwenye jamii vinatokea mara nyingi, Watanzania wenzetu wanapoteza Maisha. Je, Serikali haioni haja ya kushirikiana na viongozi wa dini katika kuwapa elimu wananchi kwa sababu, vitendo vinasababishwa na mmong'onyoko wa maadili vilevile na hofu ya wananchi kupoteza hofu ya Mungu na wanaojenga hofu ya Mungu na maadili ni viongozi wetu wa dini, sasa Serikali haioni haja ya kushirikisha viongozi wa dini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Swali lake la kwanza, Serikali imekuwa ikishirikiana na jamii katika kutekeleza afua za ulinzi na usalama katika jamii. Ndiyo maana Kamati zetu zinaanzia katika vijiji, Mwenyekiti wa Kijiji hadi Taifa, ili kuhakikisha kuwapa elimu ya ulinzi na usalama kwa jamii, ili wananchi wawe na uelewa kuhakikisha kwamba, usalama katika nchi unakuwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Wizara inashirikiana na viongozi wa dini katika kutekeleza Mpango wa Pili, MTAKUWWA, ambao viongozi wa dini wamo katika Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kamati hiyo inaanzia Vijijini hadi Taifa kuhakikisha Mpango wa Pili wa Taifa wa MTAKUWWA unakamilisha Sheria na hatua zake na viongozi wa dini kuhakikisha kwamba, wanatoa miongozo na makongamano katika jamii, kutoa elimu ya kutokomeza vitendo vya

ukatili dhidi ya wanawake na migogoro ya msongo wa mawazo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia vimekuwa vikiongezeka kila mwaka. Sasa, nataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je, Serikali iko tayari kupitia Vifungu vya Sheria kwa sababu, vimekuwa vikikinzana na kuchochea changamoto hii? Kwa mfano, kijana wa miaka 18 Sheria yetu inamtambua anaweza kuoa na kuolewa na anaweza kupiga kura kwa sababu, anaweza kutambua mazuri na mabaya.

Mheshimiwa Spika, lakini ikija kwenye adhabu, kijana wa miaka 18 na ambaye, yuko chini ya miaka 18 ambaye, amelawiti na kubaka adhabu yake ni siku 30 na kuchapwa viboko. Kwa hiyo nataka kujua, je, mko tayari kufanya mapitio ya hii Sheria? Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rose. Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria ipo katika hatua za kuendelea kurekebisha Sheria za adhabu. Tutakapokamilisha tutaleta katika Bunge lako Tukufu, ili kuhakikisha Sheria hizo zinapitishwa na adhabu zinazotolewa zinastahiki kwa mtuhumiwa ambaye amefanya vitendo hivyo vya ukatili. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimemuona Mheshimiwa Maryam Mwinyi, lakini subiri kidogo nipate jina lako la kati, maana nikiita tu Maryam Mwinyi, isije ikaonekana ni Mheshimiwa *First Lady* wa Zanzibar. *(Makofi)*

Ngoja nipate jina lako la kati hapa haraka, ama wewe nikumbushe. Aaah! Haya, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni juzi tu mtoto mwenye ulemavu wa ualbino Sengerema amenusurika na kifo. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu jambo hili ambalo linaanza kutoa mizizi mikubwa katika nchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Najiuliza kama ni la kwako au ni la Mambo ya Ndani ya Nchi. Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumjibu Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi kwa kumwambia kwamba, Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa alitoa taarifa ya Serikali. Serikali imekwishatoa maelekezo kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa yote na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha kwamba, wanaimarisha ulinzi na usalama kwa watu wenye ualbino.

Mheshimiwa Spika, lakini tuseme tunaendelea kuwapa elimu Watanzania kuwathamini na kuwajali watu wenye ualbino, ili wasiwadhuru. Sisi tutaendelea kufuatilia kwa ukaribu jambo hili na tunawataka pia, walezi waendelee kuwa karibu na watoto hawa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 710

**Kuwasaidia Wasichana Wanaokatiza Masomo kwa Ujauzito**

**MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wasichana wanaokatisha Masomo kwa sababu ya kupata ujauzito?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha wanafunzi wasichana wanaokatisha masomo kwa sababu ya kupata ujauzito wanarejea shuleni. Hatua hizo ni pamoja na kutoa Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 2021 kuhusu kuwarejesha wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu, mbalimbali ikiwemo kupata ujauzito.

Mheshimiwa Spika, waraka huu umetoa fursa kwa mwanafunzi wa kike aliyepata ujauzito kurudi shule kukamilisha mzunguko wake wa kielimu ama katika shule yake ya awali au shule yoyote ambayo mzazi/mlezi na mwanafunzi watakubaliana na mamlaka husika kwa lengo la kuhakikisha mwanafunzi anakamilisha mzunguko wake wa kupata elimu. Vilevile, Serikali imeweka mfumo usio rasmi ambao unaruhusu mtu yeyote kujiendeleza kielimu, ili kukamilisha malengo yake, hususan katika Elimu ya Watu Wazima au vyuo vya maendeleo ya wananchi ambapo hata mwanafunzi aliyekatiza masomo anaruhusiwa kujiunga, ili kukamilisha mzunguko wake wa kupata elimu. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa moyo wake wa huruma kwa kufanya maamuzi magumu kwa kuwarejesha wasichana waliopata mimba na kukatiza masomo yao. Je, Serikali imetekeleza mikakati gani, ili kuhakikisha wahanga wa ubakaji wanapata sauti na mifumo ya Sheria na haki inaboreshwa, ili kuzuia wasichana wasikatishe masomo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Norah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali langu la msingi, zipo jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kuwalinda watoto wetu wa kike dhidi ya ubakaji na ukatili kwa ujumla. Jitihada hizo ni pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa wanafunzi wawapo shuleni, ujenzi wa mabweni pamoja na hosteli, kuanzisha madawati ya ushauri nasaha kwenye maeneo yetu ya shule na mpaka vyuoni kwa ujumla. Aidha, Serikali imeendelea na utoaji wa elimu kwa jamii, hususan dhidi ya vitendo hivi vya ukatili kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya ubakaji ni kosa la jinai na adhabu yake inatolewa chini ya Sheria ya Adhabu, Kifungu Na. 16 ya Sheria yetu ya Bunge. Sheria hiyo inatoa adhabu kali ikiwemo kifungo cha miaka 30 au zaidi ya hapo. Kwa hiyo, hii ni mikakati ya Serikali kuhakikisha kwamba, vitendo hivi vinakomeshwa kwenye jamii yetu. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, Ahsante. Kumekuwa kuna unyanyapaa mkubwa sana kwa hawa wasichana

ambao walipata mimba pindi wanapoamua kurejea kwenye shule zao walizokuwa wanasoma awali. Unyanyapaa huu unasababishwa kwanza na walimu wenyewe na pia, wanafunzi ambao wanasoma darasa moja.

Mheshimiwa Spika, je, sasa Serikali haioni sababu ya kutenga madarasa maalum kwa hawa ambao wanarudi mashuleni kwa sababu, ni watu maalum na wana mahitaji maalum? Kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuanzisha hayo ma…?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Najibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Rehema Migilla, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Migilla anasema kuwarudisha kwenye shule hizo kunaleta unyanyapaa; kwanza tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Migilla. Tutakwenda kufanya tathmini ya kina, lakini tunadhani kuwatenga na kuanzisha madarasa yao ndiyo unyanyapaa zaidi kuliko tutakapoanzisha ile elimu changamano.

Mheshimiwa Spika, lakini tumesema kwenye majibu ya swali la msingi, mwanafunzi huyu anapotaka kurudi shuleni ni ushauri wa mzazi au mlezi pamoja na mwanafunzi yeye mwenyewe kwamba, ni eneo gani anahisi kwa upande wake yeye litakuwa ni rahisi na jepesi kurudi bila kupata changamoto yoyote. Kwa hiyo, ngoja tukafanye tathmini ya kina kwenye maeneo hayo kwa sababu, waraka huu ni wa mwaka 2021 ndiyo tunaendelea kuutekeleza tuweze kuona *performance* yake halafu tukiona kwamba matokeo yake siyo chanya, tutafanya marekebisho na kufuata ushauri wa Mheshimiwa Migilla. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hapo kwenye tathmini ni pa muhimu sana na wadau itabidi kwa kweli, mtuulize. Maana sasa wanarejeshwa shuleni, shule ya kawaida, ili wandelee na mfumo ambao walikuwa wametoka kupumzika, wamerejea. Sasa wakianza

kutengenezewa madarasa, yaani shule nzima itakuwa walipata mimba halafu wakarudi shuleni au mwanafunzi akafundishwe pekeyake kwa sababu, yeye ni *special?* Mbona utakuwa mtihani huu. Eeh! huu utakuwa mtihani.

Mheshimiwa Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kuna kama mazoea fulani hivi kwamba, mashauri ya kesi za jinai za kuwapa ujauzito watoto zinachukua muda mrefu sana kuamuliwa Mahakamani kiasi kwamba, wakati mwingine ni kama vile zinapotea njiani. Serikali haioni umuhimu wa kuja na utaratibu wa ku-*fast track* mashauri yote yanayohusiana na kuwapa watoto ujauzito, ili kuweza kuyamaliza kwa kipindi kifupi iwezekanavyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuwa natazama hapa Wizara ya Katiba na Sheria, lakini naona Mheshimiwa Waziri hayupo wala Mheshimiwa Naibu wake. Hilo ni la Katiba na Sheria kwa sababu, kule ndiyo Mahakama inahusika. Sasa tukimpa huyu wa elimu kidogo, kwa hiyo, kwa kuwa hawapo ili watoe hayo majibu, Mheshimiwa Tarimba utalileta kama swali la msingi, ili liweze kujibiwa kikamilifu swali lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, ulikuwa umesimama.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, kuna baadhi ya walimu wakuu wa shule huwawekea vikwazo watoto ambao walipata ujauzito kurudi shuleni kwa wakati. Nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Najibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mnzava kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waraka Na. 1 wa Mwaka 2021 unaelezea utaratibu mzima wa namna gani ya watoto hawa kurudi shuleni. Kwa hiyo, mwalimu mkuu hawezi kuwa kikwazo cha watoto hawa au huyu anayetaka kurudi shuleni, kurejea kama atafuata vizuri huo waraka.

Mheshimiwa Spika, nadhani wajibu wetu sisi ni kuhakikisha kwamba, waraka huu unaufikia umma, ili kujua ule utaratibu kwa sababu, kimsingi hatakiwi kuanzia pale shuleni moja kwa moja, anaanzia kwa Afisa Elimu na kama mwalimu mkuu ataleta changamoto yoyote, basi Afisa Elimu au Mkurugenzi au Mkuu wa Wilaya wa eneo husika anahusika moja kwa moja kuhakikisha kwamba, mtoto huyo anarudi shuleni bila kikwazo chochote cha mwalimu mkuu. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sasa hivi takwimu zinaonesha kuna ongezeko kubwa sana la wavulana kuacha elimu ya msingi na elimu ya sekondari. Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa hivi kutenegeneza mkakati ambao pia, utawarejesha katika mfumo wa elimu wavulana hao ambao wameacha shule kwa sababu, ni haki yao ya msingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kuna changamoto kwa upande wa watoto wetu wa kiume na wao vilevile wamekuwa wakikatiza masomo kwa namna moja au nyingine, lakini Waraka wetu huu Na. 1 wa Mwaka 2021 umeeleza wazi kwamba, utahusiana na watoto wetu wa kike waliopata ujauzito pamoja na watoto wengine waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini namuondoa wasiwasi Mheshimiwa Chikota, hivi sasa pale Wizarani tumetengeneza timu ya kufanya utafiti wa kupata sababu hasa za msingi ni kwa nini kuna hii *dropout* au kukatiza masomo kwa wanafunzi wetu au vijana wetu wa kike na wa kiume. Baada ya utafiti huo tutapata kujua hasa sababu maalum zinazosababisha jambo hilo, lakini kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba, watoto wetu hawakatizi masomo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, kama mnavyofahamu kwamba, Sera yetu ya Elimu imepanua wigo wa elimu ya lazima kutoka miaka 7 kwenda miaka 10 kwa hiyo, ni lazima mtoto huyu atakapoingia darasa la kwanza akamilishe mzunguko wake wa miaka 10. Kwa hiyo, tunahakikisha tunatengeneza mikakati ya kuwa-*retain* wanafunzi hawa shuleni. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, sasa aulize swali lake.

Na. 711

**Kuanza Matumizi ya Sarafu za Kidijitali Nchini**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kwa matumizi ya Sarafu za Kidijitali *(Central Bank Digital Currency)* hapa nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Benki Kuu ya Tanzania kwa sasa inaendelea na hatua ya utafiti wa uanzishwaji wa matumizi ya Sarafu za Kidijitali za Benki Kuu *(Central Bank Digital Currency)*.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu imebaini kwamba, kama ilivyo kwa mataifa mengi, uanzishwaji wa Sarafu za Kidijitali za Benki Kuu, unahitaji kuanzishwa kwa uangalifu na umakini bila kuleta athari hasi katika mifumo ya malipo iliyopo nchini. Pia, kuweza kutatua tatizo halisi la malipo ambapo kwa sasa bado mifumo iliyopo nchini inakidhi hali halisi ya uwezeshaji mwananchi kutuma fedha na kufanya malipo.

Mheshimiwa Spika, aidha, soko letu bado linahitaji kuendelea kuboreshwa katika kuimarisha mifumo iliyopo kwa kutumia vyanzo vinavyopatikana kwa urahisi na wananchi wengi (simu za kawaida) tofauti na matumizi ya Sarafu za Kidijitali zinazoitaji matumizi ya simu janja *(smartphones)*. Nchi nyingi ikiwa ni pamoja na majirani zetu na ukanda wetu bado wapo katika hatua hizi za awali za utafiti na kuboresha mifumo ya malipo iliyopo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali madogo mawili. Sasa hivi nchini kuna biashara ya *foreign currency markets* inazofanyika kwenye mitandao, Pamoja na biashara ya *crypto currencies*. Nini mkakati wa Serikali wa kusimamia na kuratibu biashara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kuna Watanzania wengi wanafanya kazi nje ya nchi na wengine waliopo nchini wanafanya kazi za kisanii, kibiashara na kishauri kupitia mitandao, wanalipwa kwa fedha za kigeni, lakini fedha zile kuingia nchini imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa sababu ya gharama kubwa za makato wanazopitia.

Mheshimiwa Spika, waweze kupitia nini makakati wa kupunguza gharama za makato ili Watanzania wale wanufaike na jasho lao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, mkakati wa Serikali, moja kati ya Mkakati wa Serikali ni kuboresha mifumo ya utumaji na upokeaji fedha ili kupunguza gharama ikiwa ni pamoja na kupunguza tozo na makato mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili Serikali inaendelea kufuatilia suala hili na tumechukua ushauri wake tukiona ipo haja ya kufanya hivyo basi tutafanya, wala hakuna shida yoyote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Ili nchi yoyote iweze kujiendesha vizuri kutoa miradi mijini na vijijini ni pamoja na kuongeza vyanzo vya mapato. Kwenye eneo hili la *digital currencies* kumeonekana kwamba kuna fursa nyingi sana na vijana wengi wa Kitanzania wanafanya biashara hii.

Mheshimiwa Spika, swali langu kwa Serikali, Serikali inaonaje kwa kushirikiana na Ofisi ya *CAG* mumpe kazi *CAG* aweze kufanya *forensic audit* kwa ajili yaku-*audit transaction* zote ambazo zinafanyika kwenye *currencies* mfano *Bitcoin, Ethereum, LEPO, USDT* na *currency* zingine ili tuweze kujua ni kiasi gani tunapoteza ili tuweze kukitumia kama chanzo cha mapato kwa ajili ya kusaidia Taifa letu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri pamoja na swali zuri lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali inaendelea na utafiti kuhusu *the whole scenario* ya matumizi ya *other currencies* zikiwemo hizi za kieletroniki pamoja na matumizi ambayo yanaendelea na *currencies* hizi za kawaida ambazo ni *hard cash,* ambazo tumekuwa tukizitumia katika baadhi ya maeneo kuangalia kama kuna *benefit* tunazoweza kuzipata endapo tuka-*shift* kwenda kwenye matumizi ya *alternative currencies* hizi *digital currencies.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utafiti unaendelea na sasa wanaangalia *experience* kutoka katika mataifa yakiwemo ya Afrika ambayo yameishaenda kwenye *digital currency* kama Nigeria pamoja na nchi za Asia ambao wameshaanza kutumia utaratibu huo. Baada ya kuwa imekamilika tutaanza hatua kwa hatua kama tutaona ni jambo lenye faida na ambalo litatupigisha hatua zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ama Waziri, kuna hili jambo linalojadiliwa sana huko nje ya hii mikopo inayotolewa kwa njia ya mtandao na watu kudhalilishwa. Sijui kama kuna mwongozo wowote ama na Serikali mmelipokea mnalifanyia kazi? Ama hilo limekuaje? Maana inavyoonekana hata mimi nimepata ujumbe wa mtu akiambiwa sijui anadaiwa sasa nawaza mimi nahusika vipi kwenye yeye kudaiwa? Sasa hilo naona limelalamikiwa sana na wananchi, sijui kama kuna maelezo yoyote upande wenu Serikali? Kwa sababu hapa tunazungumzia hayo hayo mambo ya fedha za mitandao. Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa muda sasa kumekuwa na hii changamoto ya watu ambao wanakopeshana mitandaoni lakini baadaye wanatumia taarifa za watu wanaomzunguka yule

waliomkopesha, kwa maana ya namba za simu na kuanza ku-*harass* pale ambapo wameshindwa kurudishiwa ule mkopo wao.

Mheshimiwa Spika, hili jambo limetokea kwa wiki kadhaa kama siyo miezi miwili, mitatu na baada ya kuliona tumewaagiza wenzetu wa *TCRA*, wakishirikiana na *Cyber Crime Unit* ya Jeshi la Polisi wanalifanyia kazi. Ni matumaini yangu kwamba hii kazi itakamilika mapema ili tuone msingi wa hili jambo ukubwa wake na wapi wanapozipata hizi namba? Kwa sababu msingi mkubwa hapa ni ule udhalilishaji unaofanyika baada ya kushindwa kulipana baada ya kukopeshana.

Mheshimiwa Spika, maana ni jambo ambalo linatokea mtu anachukua namba za watu wengi sana wenye uhusiano na yule waliomkopesha. Tunatafuta hili jambo linatokea wapi ili tuchukue hatua na kulikomesha lakini hili jambo siyo jambo la kiungwana na kinyume cha sheria na hasa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutumia taarifa za watu wengine kufanya chochote na hizo taarifa. Hili jambo ni kinyume cha sheria ni nje ya utaratibu si la kiungwana na linapaswa kukomeshwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso. *(Makofi)*

Na. 712

**Ujenzi wa Maghala ya Mazao – Ushetu**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO K.n.y. MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao katika Halmashauri ya Ushetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imejipanga kujenga ghala katika Halmashauri za Wilaya nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, Mkoa wa Shinyanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ilishatoa maeneo na Mheshimiwa Mbunge wa eneo husika alikidhi vigezo ambavyo Wizara ilileta kwa ajili ya kutoa maeneo ni kwa nini mpaka sasa maghala hayo hayajengwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili halmashauri nyingi nchini zimekuwa zikinufaika na *cess* ya mazao yanayotolewa kwenye halmashauri zote zinazonufaika na mazao hayo. Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wakulima ili kuwajengea maghala wakishirikiana na halmashauri ambazo wananufaika na *cess*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kama nilivyojibu katika swali langu la msingi ni kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja ndipo tunaanza ujenzi wa maghala katika maeneo yote ambayo tumeainisha. Kwa hiyo, jambo hili anavyosema lini? Ni kuanzia mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga maghala ndiyo jukumu kubwa ambalo tunalifanya sisi kama Wizara kwa kushirikiana na

halmashauri pamoja na wakulima kupitia *AMCOS* zao ili tuhakikishe kwamba wananufaika na hii faida ambayo wanaipata kwa wao kushiriki katika kilimo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama nimewaona lakini maswali kwa kifupi, moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nini mkakati wa Serikali kupitia Ushirika kukarabati maghala yaliyokuwa yakitumika kuhifadhi pamba na pembejeo yaliyochakaa sana Jimboni Busanda? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, moja ya mkakati tulionao ni pamoja na maghala ambayo yako katika eneo la Jimbo la Busanda katika mwaka wa fedha unaokuja tutayakarabati, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, teknolojia ya kuhifadhi hii nafaka katika mifumo ya tabaka tatu ndiyo teknolojia ambayo inaweza ikamudu katika ngazi ya kaya lakini ni ghali. Serikali ina mpango gani kupunguza bei ya mifuko hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge na moja ya mkakati tulionao sisi kama Wizara ni kuhakikisha kwamba tunafuta fedha ili tuweke ruzuku katika hiyo mifuko ili tuwapunguzie adha wakulima, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, pale kwenye Kata ya Mwamanyili na Kata ya Ngasamo kuna maghala ya ushirika ambayo yamechakaa je, Serikali iko tayari kuja kufanya ukarabati kwenye maghala haya ili yatumike kuhifadhia chakula? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika mwaka wa fedha unaokuja, sehemu ya maghala tutakayojenga ni pamoja na maeneo ya Busega. Kwa sababu lengo la Serikali ni kuongeza uhifadhi wa chakula kutoka tani laki tano kufikia tani laki saba mwakani kwenda tani milioni 1.2 katika mwaka wa fedha unaofuatia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ina wakulima wengi; Mheshimiwa Waziri tayari tuna eneo la kujenga maghala kwa ajili ya kuwasaidia Wakulima wa Mbogwe; je, lini Serikali mtatoa pesa ili kusudi mkawajengee Wakulima wa Mbogwe maghala? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge, kwanza nimepokea ombi lake lakini la pili nitangalia katika mpango kama upo katika mwaka wa fedha huu unaofuatia na kama halipo tutahakikisha kwamba linawekwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 ili tuhakikishe Wananchi wa Mbogwe nao wanajengewa ghala, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ni lini mtalipa *cess* ambayo Halmashauri ya Mji wa Makambako tunawadai shilingi milioni 250 ili ikidhi matarajio ambayo bajeti yake…

**SPIKA:** Mheshimiwa, weka kisemeo vizuri ili uingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Uliza tena swali lako.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ni lini Serikali italipa shilingi milioni 250 kwenye Halmashauri ya Makambako ambayo ni *cess* ya makusanyo ya ambayo walikuwa wananua mazao ya mahindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kama majibu unayo unaweza kumpa Mbunge lakini kama huna unaweza kumpatia baadaye kwa sababu swali lake liko nje kidogo ya swali la msingi. Unayo majibu au utampatia baadaye?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninayo majibu.

**SPIKA:** Mpatie majibu Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kwamba kuna halmashauri zinazotudai *cess* ikiwemo Makambako hata Wanging'ombe pamoja na halmashauri nyingine na madeni yao yote tumeshapeleka Wizara ya Fedha tunasubiri tu fedha ambayo itatoka Wizara ya Fedha na sisi tutahakikisha tunawalipa kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Mkoa wa Simiyu utajengewa maghala ya kutosha ya kuhifadhia mazao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika mpango tulionao katika mwaka wa fedha unaokuja kuna halmashauri kadhaa ambazo tunajenga katika Mkoa wa Simiyu. Kwa hiyo niseme tu katika mwaka unaokuja watapata maghala mapya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali kupitia Bodi ya Korosho ilianza kujenga maghala ya kuhifadhia mazao katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru tangu 2014 na ujenzi ule ulikwama kwa muda mrefu na mpaka sasa bado haujaweza kuendelea, ni lini ujenzi huu utaendelea ili kupata maghala ya kuhifadhia mazao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, katika mpango wa mwaka wa fedha unaokuja 2024/2025 maghala yalioko katika Jimbo na Halmashauri ya Tunduru yapo katika mpango wetu. Kwa hiyo mwakani tutakwenda kuyamalizia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa Jimbo la Mchinga ni miongoni mwa Majimbo yanayozalisha ufuta kwa wingi na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema atajenga maghala; je, Jimbo la Mchinga litakuwa ni miongoni mwa maghala hayo yatakayojengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimwondoe shaka mama yangu, Mama Salma Kikwete, Wananchi wa Mchinga ninaamini tutawafikia. Nitakwenda kuangalia katika mpango kama haipo sasa hivi tutahakikisha tunaweka katika mwaka wa fedha unaokuja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 713

**Ujenzi wa Barabara ya Chela – Kahama**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza Ujenzi wa Barabara ya Chela - Busengi hadi Kahama kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, zabuni kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Nyang'oholongo ambayo ipo mpakani mwa Geita na Shinyanga kwenda Chela – Busangi hadi Nyambula yenye urefu wa kilometa 40.45 ipo katika hatua ya tathmini ambayo inatarajiwa kukamilika na kusainiwa kwa mkataba mwishoni mwa mwezi Julai, 2024. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2025. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kila mwaka majibu yamekuwa ni yale yale kuhusu barabara hii, kwamba upembuzi yakinifu unakaribia kukamilika. Sasa tunataka tujue hivi upembuzi yakinifu huu ni lini sasa utakamilika? Kwa sababu majibu unayotoa leo Mheshimiwa Naibu Waziri ni majibu ambayo mwaka jana pia uliyatoa hayo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni lini sasa Mheshimiwa Waziri atatekeleza ile ahadi ya kuunganisha barabara inayotoka Bulige kuja mpaka Busangi kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea sasa hivi tumetaja tarehe ya kukamilisha kumpata mhandisi mshauri na tarehe ya kukamilisha usanifu. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hilo linaendelea na litafanyika kama tulivyosema kwenye jibu letu la msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kuna hilo eneo lenye kilometa kama 10 kuunganisha hiyo miji midogo ambayo ni sehemu ya barabara ambayo inaanzia huko Misasi kuja Kahama. Tayari tunafanya kazi kwa awamu kulingana na maeneo kwa awamu lakini barabara imefanyiwa usanifu. Wakati Serikali inatafuta fedha kufanya kujenga barabara yote tutahakikisha kwamba ile miji na maeneo machache machache tunaendelea kuyajenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, wakati wa zoezi la ujazaji maji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere Mheshimiwa Rais alitoa agizo la ujenzi wa Barabara kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere kupita Magindu hadi Chalinze. Wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini ambao watapitiwa na mradi huo wanataka kujua hatua zilizofikiwa za utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Kibaha pamoja na wananchi wote ambao wanapita katika barabara hiyo. Ilikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais na barabara hiyo haipo ni barabara ambayo inajengwa upya. Katika mwaka huu wa fedha tumeshatenga fedha na tuko kwenye manunuzi kuanza kumpata mtu wa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu, kwa hiyo zoezi hilo tayari limeishaanza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza naishukuru Serikali kwa ujenzi wa Barabara ya Kidatu mpaka Ifakara kwa kiwango cha lami. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kivukoni – Mahenge – Ketaketa – Ilonga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara aliyoitaja tayari tumeshafanya usanifu na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsantem je, ni lini barabara ya kutuko Nangurukuru kwenda Liwale itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, hii barabara mwaka huu tumetenga tutaanza kuijenga kwanza kilometa 10 na hasa tutaanza maeneo yale ambayo ni korofi katika hiyo barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni lini Serikali itaanza Ujenzi wa Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani hadi Mbulu kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pia barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, Mbuyu wa Mjerumani kwenda Mbulu imeshakamilisha usanifu na tulichokuwa tunakifanya ni kujenga kwa awamu hasa kwenye ile milima (zile *escapement)* wakati Serikali inatafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang, sasa aulize swali lake.

Na. 714

**Ujenzi wa Barabara ya Haydom hadi Mogitu – Hanang**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia hatua gani ya ujenzi wa barabara ya Haydom hadi Mogitu kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Haydom – Mogitu yenye urefu wa kilometa 70 imekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kazi ya upembeuzi yakinifu kwa barabara ya Nangwa – Gisambalang – Kondoa imefikia hatua gani?

Swali la pili, tuliomba barabara ya kutoka Bashnet – Setched – Bassodesh – Hirbadaw - Zinga ambayo kwa upande wa Singida kwa maana ya Zinga – Singida na upande wa Dareda – Bashnet ipo *TANROADS*.

Je, ni lini hiyo barabara yote mtaipandisha hadhi ili ihudumiwe na *TANROADS?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nangwa – Gisambalang – Munguli B - Kondoa inapita kwenye madaraja makubwa mawili. Daraja kubwa la Munguli *B* lenye mita 500, tayari usanifu umeshakamilika na barabara yote mwaka huu tumeingiza kwenye usanifu ikiwa ni pamoja na Daraja la Kondoa ili tuweze kuunganisha hiyo Mikoa ya Manyara na Dodoma kwa maana ya Wilaya ya Hanang’ na Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandisha hadhi hizi barabara, zipo taratibu ambazo kama zimekamilishwa na wataalam wamejiridhisha kwamba barabara hizi zote zinahadhi ya kuingia *TANROADS* basi hilo litafanyika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Kamguna swali la nyongeza. Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri.

Barabara ya kutoka Mererani kupita Lendanai kwenda Orkesumet usanifu wake wa kina umemalizika. Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Kama alivyosema hatua ya kuanza lami ni kukamilisha usanifu na baada kukamilisha usanifu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza kuijenga hiyo barabara maana sasa gharama zimeshajulikana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa barabara ya Haydom tumekwenda na Naibu Waziri tumesaini. Je, unawaambia nini wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini kuhusiana na barabara hiyo kujengwa kutoka Haydom kwenda Labai?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumeshasaini na mkandarasi ameshapatikana, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuijenga na mkandarasi hatatoka *site* kwa sababu tayari ameshasaini mkataba, ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 715

**Kuongeza kasi ya Ujenzi wa Vituo vya Polisi Nchini**

**MHE. MWATUMU DAU HAJI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuongeza kasi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga Vituo vya Polisi nchi nzima ili kutoa huduma ya ulinzi kwa wananchi. Utekelezaji wa mpango wa ujenzi unategemea fedha zinazotengwa kutoka kwenye bajeti ya Serikali kila mwaka, toka kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo pamoja na michango ya kujitolea ya wananchi na wadau mbalimbali. Hadi sasa Serikali imeshajenga vituo vya Polisi Daraja *A, B* na *C* 487 na vituo vidogo vya Kata/Shehia 667 nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza kasi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahanste sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyoyatoa hapo lakini nina maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya maeneo nchini havijafikiwa kujengwa vituo vya polisi, lini Serikali itajenga vituo hivyo? *(Makofi)*

Swali langu la pili, sambamba na ujenzi wa vituo vya polisi, vipi kuhusu ujenzi wa nyumba za askari nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa vituo vya polisi ambavyo havijafikiwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwenye mwaka wa fedha 2024/2025 tunajenga vituo vya polisi 12 na tunamalizia maboma 77 ambayo tayari yamejengwa katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, kwenye bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani tunajenga vituo 26 kutoka kwenye bajeti pamoja na Mfuko wa Tuzo na Tozo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Serikali imeendelea kujenga nyumba za askari katika maeneo mbalimbali na itaendelea kutenga fedha na kujenga nyumba awamu kwa awamu na kukamilisha katika maeneo ambayo hayana nyumba za askari. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Tarafa ya Njinjo wamekuwa wakisafiri umbali wa zaidi ya kilomita 100 kufuata huduma za Kipolisi Kilwa Masoko.

Je, ni lini Serikali itawajengea Kituo cha Polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Ndulane kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, tayari tunajenga vituo vya polisi awamu kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama kwenye mwaka wa fedha

huu kituo chake hakipo basi kwa mwaka wa fedha unaokuja tutatenga fedha na kujenga kituo cha polisi katika eneo ambalo amelitaja Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Susuni ni moja kati ya Kata ambazo zipo pembezoni kabisa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, nataka kujua ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi ukizingatia Kata jirani ya Mwema ina vituo viwili vya polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama niliyosema tunajenga vituo vya polisi vya Kata kwa awamu. Kwa mwaka wa fedha huu 2024/2025 tunajenga vituo 12, lakini hii ni kwa awamu ya kwanza, kwa mwaka unaofuata tutajenga vituo 196 na vinakuja vituo 212.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kituo chako kama hakipo kwenye mpango wa mwaka huu tutapanga mwaka wa fedha unaokuja ili kujenga kituo cha Polisi cha Kata ya Susuni kama ambavyo umeomba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, Halamshauri ya Itigi, Kituo cha Polisi Itigi, Polisi wa Itigi wanakaa kwenye majengo ya Reli na Reli wanajiimarisha pia yamechakaa sana.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga kituo cha polisi katika Halmashauri ya Itigi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majengo, nyumba? Kipi kati ya hicho?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi.

**SPIKA:** Majengo wanayoishi yamechakaa sana.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, yamechakaa sana na ni ya reli.

**SPIKA:** Wakati huo huo Kituo cha Polisi hakipo?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, kile Kituo cha Polisi siyo cha Wizara ya Mambo ya Ndani ni Kituo cha Polisi Reli na wanajiimarisha sasa.

**SPIKA:** Nataka kuelewa swali lako ni la kituo cha polisi au nyumba wanazoishi ambazo zimechakaa?

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi.

**SPIKA:** Kituo cha Polisi. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Massare kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tunajenga vituo vya polisi kwa kutumia bajeti ya Serikali, Mfuko wa Tuzo na Tozo lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama kituo chake mwaka wa fedha huu hakipo basi tutakitengea fedha kwenye mwaka wa fedha 2025/2026 ili tujenge kituo cha polisi katika eneo lake la Itigi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa wananchi wa Kiteto, Kata ya Magungu, Kijungu na Lengatei

wameshaonesha nia ya kujenga vituo vya polisi. Lini Naibu Waziri utakuwa tayari kutembelea vituo hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nipo tayari kwenda Kiteto kutembelea vituo hivyo ambavyo vimeshaanza kujengwa na wananchi, kama nilivyosema maboma yote ambayo wananchi wameshaanzisha, Serikali ipo tayari kumalizia kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Tumetenga shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nitakuja kukutembelea katika eneo lako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Jibu la Mheshimiwa Waziri la sasa ndiyo lilikuwa swali langu pia. Nashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naibu Waziri aliyekuwepo Mheshimiwa Sagini alienda Nyanungu kule ni mpakani karibu na Hifadhi ya Serengeti hakuna kituo cha polisi wala nyumba ya polisi. Ni nini kauli ya Serikali katika eneo hili ili watu wapate huduma ya ulinzi na usalama? ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waitara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, eneo alilotaja kama alivyosema lipo mpakani na lina changamoto ya usalama. Nitakaa na Mheshimiwa

Mbunge tuone namna ya kwenda kulitembelea eneo hilo na kulitengea bajeti kwa mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026 ili tupate kituo cha polisi kwa eneo la Mheshimiwa Mbunge alilolitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Hoja ya dharura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa ninalo tangazo hapa la wageni ambao wamepata nafasi ya kuingia hapa ndani asubuhi hii.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, kwanza ni wageni sita wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni walimu wa *Academic International Schools* kutoka Mikocheni Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Namsifu Joshua - Mratibu wa Safari, Ndugu Maganga Methusela - Makamu Mkuu wa Shule, Ndugu Joyce Pontian - Mwalimu wa Sayansi, Ndugu Gasper Kapwani - Mwalimu wa Jiografia, Ndugu Elias Souvenir - Mwalimu wa Kifaransa na Ndugu Chiza Marekani - Mwalimu wa Sayansi. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 22 wa Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Mafinga Mkoa wa Iringa, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania Wilaya ya Mufindi Ndugu Macelina Mkini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni watano wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, ambaye ni Waziri wa Madini na hawa ni *Miss Tanzania 2022* ambaye pia ni *Miss World Tanzania 2024* na Wajumbe wa Kamati ya *Miss* Kanda ya Kati, karibuni sana. Miss *Tanzania* ndiyo yupi hapo? *Ooh!* karibu sana. Haya ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima, ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambao ni Wajumbe wa Baraza Asasi Zisizo za Serikali na *(NACONGO)* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hawa ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Babati Vijijini, Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, Jumuiya la *Lokeen-Natron* kutoka Longido, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaozungumza kuna wageni hapa wametangazwa sikilizeni. Nikiwa nimesimama tuelewane, maana wakati mwingine tunawalaumu watoto wetu huko kwamba darasani kidogo inakuwa mtihani, kumbe na sisi ni hivyo hivyo, kwa sababu jambo jepesi kweli mtu amesimama hapa unashindwa kunyamaza ni dakika ngapi nitakuwa nimesimama? Waheshimiwa Wabunge tunatoa picha hiyo kwa wageni wanaokuja kujifunza hapa Bungeni.

Nilikuwa nimewataja wageni 30 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Momba, Mkoa wa Songwe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ambao ni wanafunzi 72 na walimu wa Shule ya Msingi Ignatius kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Afisa Mtendaji Mkuu wa *Ainmark Technologies* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki ambaye ni rafiki yake kutoka Tarime. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, wapigakura wake kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, wapigakura wake kutoka Moshi Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula ambao ni mpigakura wake kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, marafiki zake kutoka Jijini Mwanza. *(Makofi)*

Waheni watatu wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ambaye ni Kiongozi wa Jumuiya ya Wazazi Singida Kaskazini na wapigakura wake. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole ambao ni marafiki zake kutoka Mbozi Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, ambao ni dada zake kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Eric James Shigongo ambao ni wapigakura wake kutoka Buchosa. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ambao ni wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam na Dodoma. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni wanachama wa *Bring Hope Foundation* kutoka Mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Adballah Jafari Chaurembo, wapigakura wake kutoka Mbagala, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ambao ni wanakwaya wa hamasa na waumini wa Kanisa la *DRV Anglican* Makanda kutoka Manyoni, Singida. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex ambao ni Watu Wenye Ulemavu, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 18 wa Mheshimiwa Rose Tweve ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Mufindi Kaskazini, Mkoa wa Iringa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Makada 5 wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jijini Mwanza wakiongozwa na Ndugu Consolatha Malunde, ambaye ni Mjumbe wa Halmshauri Kuu Mkoa wa Mwanza, ahsante sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 16 na Walimu 4 wa Shule ya Msingi Sakilight kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 18 wa Chuo cha Afya ya Sayansi Shirikishi *(DECCA)* kutoka Jijini Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 17 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari Ngateu kutoka Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndiyo wageni waliopo hapa Bungeni wengine watatangazwa kadri orodha yao inavyoletwa hapa mbele.

Baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Hoja ya dharura.

**SPIKA:** Hoja ya dharura na mwongozo. Haya mwongozo Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa Kanuni ya 76 sitaisoma kutokana na muda**.**

Mheshimiwa Spika, ninatambua kabisa kuna kanuni inayohusu akidi ya Bunge, lakini ninasimama kwa mwongozo wa Kanuni ya 76 kwa ajili ya kutaka mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, jana tulikuwa na shughuli ya Kibunge hapa, Bunge zima lilijaa na viti vyote vilienea, lakini asubuhi hii ninaomba kujua ni kwa nini, ninafahamu Mawaziri wako kazini yawezekana wana vikao mbalimbali, kuna baadhi ya Kamati labda zimetoka, lakini inaonekana idadi hii ni ndogo sana na imekuwa ni kawaida kwa *party caucus* zote, iwe upinzani au iwe kwenye Chama Tawala Wabunge kutokuhudhuria; kwanza kwa kutokuja mapema Bungeni lakini pili kwa kutokukaa Bungeni kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kuweza kujua ni kwa nini jana tulifanikiwa kujaza na leo kwa nini tumekuwa wachache. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge amesimama hapa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda akiomba mwongozo kuhusu akidi. Kanuni ya 90 kwa ujumla wake inazungumza akidi katika mambo mbalimbali, na Kanuni ya 91 inazungumza kuhusu uhalali wa maamuzi ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge akidi ya vikao vya Bunge kwa Kanuni zetu namna zilivyo zinataka wakati wa kufanya maamuzi. Kwa idadi hii iliyopo hapa ndani inaniwia ngumu kuagiza kwa sababu Mbunge akisema Akidi huwa inabidi tuhesabu ili tujue tuko wangapi. Sasa, kwa sababu sijatoa pia fursa ya kupiga kengele ili Wabunge warejee humu ndani niweze kuhesabu kwa sababu hakuna maamuzi ambayo tunataka kufanya kwa muda huu; na kwa hivyo, kwa kuwa hakuna mamuzi yanayochukuliwa mwongozo ni kwamba, Wabunge waliopo hapa Bungeni wanatosheleza kuendelea na shughuli zilizopo. *(Makofi)*

Ninafikiri ujumbe ambao ulikuwa unataka kuufikisha umefika mahali unapotakiwa. Kwa upande wa Wabunge, kwamba hii ni kazi yao ya msingi kuhudhuria hilo kwa kweli Wabunge wakishakuja hapa wakishaapa kila mtu anajua kazi yake ni nini. Sasa, huyo ambaye yeye kazi yake yeye ni kupiga kura basi hayo sasa si ya kwangu mimi, ni ya huko anakatoka kuja mpaka hapa. Kwa hiyo kwa akidi iliyopo tunaweza kuendelea na shughuli iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

## JAMBO LA DHARURA

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 54. Tarehe 9 Mei, 2024 nilisimama kuomba ridhaa yako ili nitoe Hoja ya Dharura, Bunge liahirishe shughuli zake kujadili kadhia wanayoipata wakulima wa chai wa Tarafa ya Bungu Wilaya ya Korogwe kwa kufungiwa kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulimpa nafasi Mheshimiwa Waziri, naye aliomba tuwape muda na kabla ya Bunge hili kwisha ataleta taarifa. Ninatambua kwamba Bunge linaisha kesho; lakini pia ulielekeza, pamoja na kusubiri majadiliano hayo kuendelea, ukaelekeza ni vyema Serikali ione namna ya kufanya ili wananchi waendelee kuchakata mazao yao. Kwa bahati mbaya jambo hilo halijafanyika, wakulima hao mpaka sasa hivi wanapata shida, hawana mahali pa kupeleka kuchakata mazao yao na chai ile inaharibika mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama niombe tena ridhaa yako; sijui, Bunge hili ni la kwako inawezekana ukawa umeshapata taarifa Serikalini. Kama hujapata taarifa Serikali niombe uniruhusu nitoe hoja hii ya dharura ili Bunge liahirishe shighuli zake ili Waheshimiwa Wabunge wenzangu wapate nafasi ya kujadili na kuniunga mkono, tuwe na maazimio ya kuishauri Serikali juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba ruhusa yako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge yuko sahihi; na kwa sababu tulishalizungumza hapa Bungeni na tukaipa kazi Serikali, kabla sijalitoa ama kabla sijafanya tathmini ya kwamba hili ni jambo la dharura kwa hivyo tulijadili ama hapana, tuisikilize Serikali imefikia wapi na jambo hili.

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Alichokisema Mheshimiwa Mnzava ni sahihi, na tulitoa *commitment* kama Serikali kwamba tunayafanyia kazi. Majadiliano yameanza kati ya Serikali na wawekezaji; siyo tu mwekezaji *Mohammed Enterprises* peke yake bali ni pamoja na *Dearly Group* na wawekezaji wanaotaka kununua Kiwanda cha Wakulima Wadogo kilichoko Rungwe.

Mheshimiwa Spika, hatua tuliyofikia sasa hivi Bodi ya Chai inafanya *evaluation* ya yale mashamba ya *Mohammed Enterprises*

na viwanda vyake; na kwa sababu tumeshampelekea *notice* ya *intention* ya Serikali, kwa sababu alivyochukua viwanda hivi kulikuwa na makubaliano kati ya Serikali na yeye wakati anauziwa mashamba na viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wetu sisi kama Serikali ni kwamba tunaona kama ame-*violate* msingi wa makubaliano ya awali. Kwa hiyo Serikali bado inaendelea kulifanyia kazi jambo hili. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumempelekea *notice* ya *intention* ya ku-*reposes assets* alizouziwa na *PSRC*. Hatua tuliyofikia sasa hivi kwa pande zote mbili ni kwamba wako kwenye hatua za majadiliano kati ya yeye mwekezaji na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ametoa maelezo yake kwamba kuna baadhi ya mashamba na *property* zina kesi Mahakamani. Tunaendelea kufanya majadiliano namna ya kulitatua jambo hili. Tunalichukulia uzito mkubwa kama Serikali, na sasa hivi tunaangalia namna ambavyo tunaweza kupata njia ya muda mfupi ya kutatua hili tatizo lililoko katika Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Mbeya, tuweze kuyatatua haya matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbeya, timu ya Wizara ya Kilimo iko kule; tumestopisha *(to stop) process* ya kuuziana zile *assets* kwa sababu kuna malalamiko ya wakulima yanaendelea juu ya mali za yale mashamba na *ownership* ya yale mashamba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo siyo jambo rahisi sana la kulimaliza kwa muda mfupi, lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wanaotoka eneo la chai kwamba tumefika hatua nzuri. *Option* ni *either* wa-*implement* makubaliano ya kuuziana yale maeneo ama Serikali i-*reposes* na tuweze kuendeleza sekta ya chai na hatutakubali sekta hii ife.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hii changamoto ililetwa mapema wakati Bunge linaendelea, na ilikuwa tupate taarifa rasmi kutoka upande wako, maana hapa asingeuliza Mheshimiwa

Mbunge tusingepata haya maelezo; Wabunge ambao wanatoka hayo maeneo ya chai ambayo yana changamoto, hebu wasimame. Wabunge moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba na wewe umesimama! Kuna chai? Anha, sawa; Mheshimiwa Kihenzile na yeye ni Mbunge lakini pia ni Waziri. Kwa hiyo huenda amekwishapata taarifa nyingine huko.

Mheshimiwa Waziri Wabunge hawa kwa sababu hii changamoto inaendelea kwao tutakapositisha Bunge saa saba ukutane nao, ili kile mtakachokubaliana huko sasa utakuja hapa utueleze Bungeni ili tuondoke wote tukiwa na amani tukijua wananchi wanaolima chai hatua zimechukuliwa na Serikali na tutafikia wapi. Kwa sababu kama nilivyosema wakati ule, chai ukishaacha kuchuma kwa wakati inaopaswa ichumwe, ikishakomaa haifai tena. Kwa hiyo, mazingira ya wakulima wa maeneo hayo ni magumu kidogo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtaonana na Mheshimiwa Waziri halafu mtanipa taarifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo lingine lilijitokeza jana wakati wa kupiga kura. Humu Bungeni wako Waheshimiwa Wabunge watatu ninafikiri; Wabunge watatu ambao jina lao la kwanza wanaitwa Asia. Sasa, kuna Mheshimiwa Asya kutoka vyama vya upinzani na kuna Mheshimiwa Asia kutoka Chama cha Mapinduzi.

Sasa inavyoonekana chombo cha habari kimojawapo, *TBC*, waliposikia Asia, na huwa tunaita majina yote matatu lakini sijui ilikuwaje wamesikia Asia na ninaona pengine katika Asia walioko humu ndani, Asia maarufu labda ni huyu Asia anayetoka Manyara ambaye ni Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Asia Halamga. *(Makofi)*

Sasa, wakati wa kutoa orodha ya Waheshimiwa Wabunge ambao walipiga rura ya Kutokuamua hawa *TBC* wakaandika kwamba Mheshimiwa Asia Halamga amepiga kura ya kutokuamua; jambo ambalo limemletea usumbufu Mheshimiwa Mbunge.

Kuna Asia watatu hapa, kuna Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga ambaye ni Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi, kuna Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, Mbunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo na kuna Mheshimiwa Asya Sharif Omar, huyu ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi pia. *(Makofi)*

Sasa hawa Asia hawa wawili walipiga kura ya ndiyo kwa bajeti. Kwa maana ya kwamba Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga Pamoja na Mheshimiwa Asya Sharif Omar. Aliyepiga kura ya kutokuamua ni Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed. *(Makofi)*

Sasa, ndugu zetu wa *TBC* walipoandika wakasema Mheshimiwa Asia Halamga badala ya huyu Mheshimiwa Asya Mohammed Mwadini. Hili limemletea usumbufu Mheshimiwa Mbunge kama Mbunge wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Sasa, nimetoa huu ufafanuzi lakini kwa sababu ni chombo cha habari kilichokuwa kimeandika, ili Mheshimiwa Mbunge akae kwa amani, *TBC* tafadhali mumwombe radhi Mbunge kwa sababu linamsumbua jambo hili kama Mbunge wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mheshimiwa Mbunge kwa namna ile ile ambayo taarifa hii ilichapwa, kwamba Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga amepiga kura ya kutokuwa na maamuzi, njia hiyo hiyo iliyotumika itumike kuomba radhi ili Mbunge akae salama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo tunaendelea na ratiba yetu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**SPIKA:** Msiwe na wasiwasi, hawana haja ya kupewa siku ngapi kwa sababu Mheshimiwa Waziri wao yuko hapa ndani na ninaamini amesikia. Kwa hivyo, tutaliona tangazo. Ninaamini nikiwa hapa

mbele tayari watakuwa wameshafanya hilo ambalo wameambiwa wafanye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendele. Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024**
***(The Finance Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu unasomwa kwa mara ya pili, na kwa hivyo nitumie fursa hii sasa kumwita Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ili aje awasilishe hoja yake hii kuhusu Muswada huu. Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance Act, 2024)* pamoja na marekebisho yake usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri ili Muswada huu uweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo mazuri ya Kamati ya Bajeti. Aidha, kwa mara nyingine ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika

hotuba ya Bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapo jana tarehe 26 Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, pia, ninamshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na waandishi wa sheria na wataalamu wa Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Aidha, ninawashukuru wadau wengine mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25 ambayo iliwasilishwa Bungeni tarehe 13 Juni, 2024 na ilipitishwa jana tarehe 26 Juni, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama ulivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, unakusudia kufanya marekebisho ya Sheria 25 zinazohusu mfumo wa kodi, ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo, ada pamoja na sheria mbalimbali, kuratibu ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho: -

(i) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura Na. 342;

(ii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura Na. 197;

(iii) Sheria ya Bajeti, Sura Na. 439;

(iv) Sheria ya Korosho, Sura Na. 203;

(v) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Na. 447;

(vi) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura Na. 196;

(vii) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura Na. 41;

(viii) Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura Na. 276;

(ix) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Na. 332;

(x) Sheria ya Ardhi, Sura Na 113;

(xi) Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Utozaji Kodi ya Majengo, Sura Na. 289;

(xii) Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sura Na. 407;

(xiii) Sheria ya Madini, Sura Na 123;

(xiv) Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura Na. 124;

(xv) Sheria ya Leseni na Usajili wa Viwanda Nchini, Sura Na. 46;

(xvi) Sheria ya Afya ya Mimea, Sura Na. 133;

(xvii) Sheria ya Bandari, Sura Na. 166;

(xviii) Sheria ya Reli, Sura Na. 170;

(xix) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Na. 220;
(xix) Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura Na. 161;

(xx) Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura Na. 251;

(xxi) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura Na. 438;

(xxii) Sheria ya Rufani za Kodi, Sura Na. 408;

(xxiii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura Na. 148; na

(xxiv) Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura Na. 82.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu 26 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza yenye Ibara za Kwanza na ya Pili inahusu masuala ya utangulizi, hususan jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo itaanza kutumika tarehe Julai Mosi, 2024.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, ya Tatu na ya 13 zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura Na. 197 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sura Na. 407.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura Na. 439 kwa kurekebisha Kifungu cha 35 kinachojumuisha vyanzo vipya vya mapato katika Mfuko wa Dharura ambayo ni asilimia 50 ya Tozo ya Maendeleo ya Reli.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Korosho, Sura Na. 203 na kurekebisha kifungu cha 17(A) ili kuelekeza mapato yatokanayo na Tozo ya Kusafirisha Korosho Ghafi Nje ya Nchi kupelekwa Bodi ya Korosho kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura Na. 147 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 14 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 124 ili kutoza Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye Ada ya Matangazo ya Biashara ya Michezo ya Kubahatisha ili kupunguza madhara hasi ya michezo ya kubahatisha kwa jamii na kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 130 cha mzalishaji wa mwisho wa pombe kali aweze kurejesha ushuru wa bidhaa inayotozwa kwenye ununuzi wa malighafi ya uzalishaji pombe kali ya kiwango cha pombe ya zaidi ya asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15(A) kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 137 ili kuainisha muda wa 25 kwa walipa kodi kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ritani ya Ushuru wa Bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 16 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 146(A) ili kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye kilevi kinachotambulika chini ya kundi la bidhaa za *HS Code* 2207 kwa mtu atakayeizalisha na kuitumia katika uzalishaji wa nishati ya viwandani au kwenye matumizi ya kitabibu au maabara.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 148 ili kuondoa maneno yanayoleta mkanganyiko kwenye kifungu hicho kwa kuongeza ufasaha wa utaratibu wa utozaji. Kifungu cha 18 kinapendekeza kufanya marekebisho kwenye jedwali kwa kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 300 kwa kilo cha *tomato sauce* na *tomato ketchup HS Code* 210032000 na bidhaa nyingine za *HS Code* hizo zinazotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kupunguza ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 6380 hadi 56 kwa lita kwenye maji ya chupa yanayozalishwa nchini. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa bia isiyochujwa yaani Upakwe Bia ya mfano wa kibuku na kundi lingine la aina hiyo ya bidhaa inayotokana na matunda mchanganyiko inayoingizwa kutoka nje ya nchi kwa kiwango cha mfuto ya shilingi 963.90 na shilingi 2959.74 mtawalia kwa lita.

Mheshimiwa Spika, deni; kutoza ushuru wa bidhaa kwenye pombe kali yenye kilevi zaidi ya asilimia 80 inayozalishwa ndani ya

nchi na itakayoingizwa kutoka nje ya nchi kwa kiwango cha shilingi 5,000 na shilingi 7,000 kwa lita mtawalia.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa bidhaa *(e),* ni kutoza ushuru wa bidhaa kwa shilingi 500 kwa kilo moja ya rangi za mafuta zitokazo nje ya nchi zitakazotambulika kwa kundi la bidhaa yenye *HS Code* 32008.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya jedwali la Sheria ya Usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi sura namba 196 kwa kurekebisha jedwali ili kutoza ushuru wa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta gafi ya kula ya Alizeti, Mashudu yanayotokana na mbegu za Alizeti zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane, kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho ya sheria michezo ya kubahatisha sura namba 41 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22, inapendekezwa kurekebishwa, kifungu cha 26 ili kuweka takwa la watu wanaotaka kufanya biashara ya kuuza ama kusambaza *token* zinazotumika kwenye mashine za michezo ya kubahatisha kuomba leseni, kuongeza aina ya leseni kwa mtu yeyote atakayefanya kazi kwa wakala wa michezo ya kubahatisha. Kupata leseni kwa lengo la kuboresha na kutambua rasmi shughuli za uwakala.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa, kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Udhibiti ya uingizwaji wa bidhaa nchini sura namba 276, kwa kuongeza kifungu kipya 18(a) na jedwali kwa lengo la kuanzisha tozo mpya inayoitwa Tozo ya Maendeleo ya Viwanda itakayotozwa kwenye thamani ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na zitakazotoka ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini hadhikizi vigezo vya uwasilia. Lengo la marekebisho haya ni kukuza uchumi wa nchi kwa kuongeza uzalishaji na uwekezaji ndani ya nchi na kuongeza na kuchochea mauzo ya nchi yetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 10 kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria ya Kodi ya Mapato sura namba 332 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 29, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 ili kuongeza tafsiri ya maneno; Mali za Kidigitali, mchimbaji asiye na leseni, maudhui ya kidigitali na mtengeneza maudhui ya kidigitali. Kama ilivyopendekezwa kwa kutumika kwenye sheria ili kuleta maana sahihi iliyokusudiwa. lengo la marekebisho haya ni kutoa tafasiri sahihi ya misamiati kama ilivyotumika kwenye sheria.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 30, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 ili kuondoa takwa la kulipa Kodi ya Mapato Mbadala kwa makampuni zinazochakata mazao ya chai yanayotengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za wazalishaji wa ndani wa chai ili kuondoa hasara zinazotokana na kushuka kwa bei ya zao la chai katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 31, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 11 ili kuweka takwa la mlipa kodi anayedai gharama za manunuzi za bidhaa na huduma wakati wa kukokotoa kodi ya mapato kudai gharama ambazo zitakuwa na kielelezo cha risiti ya kielektroniki ya kodi, isipokuwa pale ambapo muuzaji wa bidhaa ama huduma hiyo ni mtu au taasisi iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 19 ili kuongeza wigo wa mapato yatakayotozwa kodi ya asilimia 30 hadi 40 katika mwaka wa nne wa mapato na kuendelea kwa mlipa kodi anayepata hasara mfululizo. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Serikali kuongeza makusanyo ya kodi bila kuathiri haki ya mlipakodi kudai hasara alizozipata miaka ikipita kama ambavyo tumeeleza pale mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 33, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 56 ili kubainisha kuwa mabadiliko ya umiliki wa kampuni mkaazi uliyosababishwa na gawio la hisa mpya hautatozwa kodi ya mapato kwa mujibu wa kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufasaha na kuboresha usimamizi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 34, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 64 ili kujumuisha taasisi zinazofanya shughuli za uendeshaji wa afya na utunzaji wa mazingira kwenye wigo wa taasisi zinazokidhi sifa ya taasisi za hisani. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea huduma za hisani kwenye eneo la afya na utunzaji wa mazingira hususani kipindi hiki ambacho dunia inakabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 35, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 82 ili kujumuisha malipo ya ukodishaji wa vifaa vya ujenzi na mitambo kwenye wigo wa mapato yatakayotozwa kodi ya zuio. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa kodi ya zuio na kupanua wigo wa kodi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, inayofuata ni kuondoa taasisi za fedha mkaazi kwenye wajibu wa kukata kodi ya mapato kwenye malipo ya riba yatakayokwenda kwa taasisi za kifedha nje ya nchi na mfuko wa fedha usiyo mkaazi, kutokana na mkopo ambao taasisi ya fedha mkaazi imekopa kutoka taasisi ya fedha ama mfuko usiyo mkaazi ambayo imeingia mkataba na Serikali kutoa mkopo wa riba nafuu kwa taasisi za mkaazi wa kifedha kwa lengo la kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wananchi, isipokuwa tu pale ambapo taasisi hiyo ya kifedha mkaazi inamilikiwa au imemilikiwa na taasisi au mfuko huo usiyo mkaazi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 36, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 83 ili kutoza kodi ya mapato kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo yatakayofanywa kwa ajili ya ununuzi wa madini ya viwandani na madini ya metaliki isipokuwa chumvi na madini yenye thamani yanayouzwa na mmiliki wa leseni ndogo ya

uchimbaji wa madini, lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 37, inapendekeza kufanya marekebisho kifungu cha 83 kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kifungu kipya 83(b) ili kumpa mlipa kodi mkaazi asiye mkaazi au asiye mkaazi wajibu wa kuzuia kodi ya kiwango cha asilimia tano kwenye malipo yanayofanywa na mtengeneza maudhui mkaazi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi.

(b) Ubadilishanaji wa mali za kidigitali au inayowezesha ubadilishanaji wa mali za kidigitali, kuzuia kodi kwa kiwango cha asilimia tatu kwenye malipo yatakayofanywa kwa mlipa kodi mkaazi kutokana na mauzo ya mali ya kidigitali, lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 38, inapendekeza kufanya marekebisho kifungu cha 86 ili mfanyabiashara wa kati aliyouza mazao yatokanayo na Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Misitu ambayo yamekatwa kodi, makato yake kutambulika kwa malipo ya mwisho ya kodi ya mapato katika biashara yake inayouza mazao.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 39, inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 90 ili kuziondoa taasisi kwenye utaratibu mbadala wa kulipa kodi ya ziada ya mtaji unaomuhusu mlipa kodi ambaye hana kumbukumbu za gharama za mali. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha taasisi kutunza kumbukumbu na kuimarisha uhiyari wa utii wa sheria za kodi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 40, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 91 ili kuziwezesha taasisi za umma ambazo hesabu zake zimekaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ambazo zinawajibika kulipa kodi, kuwasilisha *return* za kodi ambazo ya

mapato baada ya miezi tisa tangu mwaka wa hesabu kufungwa baada ya utaratibu wa mieze sita.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 41, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 92 ili kumuondolea mlipa kodi binafsi ambaye siyo mkaazi mwenye mapato yatokanayo na ajira takwa la kuwasilisha *return* ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 42, inapendekeza kurekebisha kifungu cha jedwali la kwanza ili kuboresha madaraja na viwango vya kodi ya mapato kwa mlipa kodi binafsi anayefanya biashara ya usafirishaji wa abiria. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha usawa wa kodi na kuimarisha ulipa kodi kwa hiyari.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 43, inapendekeza kurekebisha jedwali la tatu la sheria ya kodi ya mapato ili kuongeza ufasaha katika aya ya pili kifungu kidogo cha (3), inayoweka utaratibu wa kudai ushuru wa uchakavu wa mwanzo *(initial allowance)* kwa asilimia 50 kwa mfanyabiashara atadai ushuru huo kwa awamu zilizo sawa yaani mwaka wa kwanza asilimia 25 na mwaka wa pili asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 11 na ya 12 inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ardhi Sura Na. 113 na Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya utozaji wa Kodi ya Majengo Sura Na. 289 ili asilimia 20 ya mapato inayokusanywa kutoka kwenye kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo ilipwe kwenye *account* za Mamlaka za Serikali za Mitaa ndani ya halmashauri husika. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kupata fedha za kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo kwa wakati ili kugharamia masuala ya ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi na kodi ya maje kwa ufanisi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 14, yenye Ibara ya 50 na hadi 55, inapendekeza kufanyia marekebisho katika Sheria ya Madini Sura Na.123 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 51, inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 59 ili kuweka takwa la wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini na wafanyabiashara wa madini kutenga kiasi cha dhahabu kwa ajili ya kuchakatwa, kuyeyushwa na kusafirishwa na kuuzwa nchini. Aidha, kiasi kitakachopaswa kutengwa kitabainishwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya madini kwenye kanuni kwa kuzingatia kuanzia kiasi cha asilimia 20 ya sehemu ya dhahabu inayozalishwa nchini kitapaswa kutengwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza akiba ya fedha ya kigeni nchini kwa kupunguza tatizo la uhaba wa fedha za kigeni. Vilevile hatua hii inalenga pia kuchochea ukuaji wa viwanda vya kusafirisha dhahabu na kuhakikisha vinapata dhahabu ya kusafisha ikiwa ni pamoja na hatua za kupata ithibati ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 52, inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 72(a) ili kuainisha masharti ya Sheria ya Madini na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ili kuitambua Benki Kuu ya Tanzania kama mnunuzi wa madini nchini. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha na kuongeza urahisi wa Benki Kuu ya Tanzania kununua dhahabu ili kuongeza akiba ya dhahabu ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 53 na 54, inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 87 na 89 ili kupunguza mrahaba unaotozwa kwenye madini ya dhahabu yatakayotozwa na Benki Kuu, yatakayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania kutoka asilimia sita hadi asilimia nne. Kuweka takwa la malipo ya mrahaba unaolipwa kwenye madini ya dhahabu yanayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania kuwa ni malipo ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 55, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90(a) ili kutoa msamaha wa kulipa ada ya ukaguzi ya asilimia moja kwa mtu atakayeiuzia dhahabu Benki Kuu ya Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za ununuzi wa madini na kuhamasisha uuzaji wa dhahabu Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 15, yenye Ibara za 56 na 57, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari Sura Na. 123 kwa kurekebisha jedwali la kwanza ili kujumuisha magari ya umeme pamoja na vyombo vingine vya moto kwenye wigo wa ulipaji wa ada ya usajili wa magari na vyombo hivyo vingine, lengo la marekebisho hayo ni kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 16, yenye Ibara za 58 na 59, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Leseni na Usajili wa Viwanda Nchini Sura ya 46 kwa kuongeza kifungu kipya cha 17(a) ili kuweka sharti la wamiliki wa viwanda vilivyosajiliwa au vyenye leseni kuingia mikataba ya utekelezaji na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 17, yenye Ibara 60 na 61, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Afya ya Mimea Sura Na. 133 kwa kuongeza kifungu kipya cha 35(a) ili kuipa Mamlaka na Taasisi ya Mimea jukumu la kukusanya ada kwenye huduma ya ukaguzi wa mimea, mazao ya mimea, bidhaa zilizo chini ya udhibiti zinazoingizwa nchini au kusafirishwa nje ya nchi. Aidha marekebisho haya yanakusudia kuainisha mgawanyo wa ada itakayokusanywa ambapo asilimia 70 itakuwa inakusanywa na inapelekwa mfuko mkuu wa maendeleo ya kilimo na asilimia 30 itakuwa inapelekwa mfuko mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 18 ya Ibara ya 62 na 63, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Bandari Sura Na. 166 kwa kurekebisha kifungu cha 67 ili kurejesha jukumu la kukusanya tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari *wharfage* kwa mamlaka ya usimaizi wa bandari yaani *TPA*.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 19, yenye Ibara ya 64 na 65, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Reli Sura Na. 170 kwa kurekebisha kifungu cha 68 ili kuongeza kiwango cha tozo ya maendeleo ya reli kinachotozwa na kwenye bidhaa zinazoingia kwa kutumika nchini kutoka asilimia 1.5 hadi asilimia mbili thamani ya

mzigo aidha asilimia 50 ya mapato yatakwenda kwenye mfuko wa maendeleo ya reli na ingine itakwenda kwenye mfuko wa dharura wa barabara.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 20, yenye Ibara 67 hadi 71, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta Sura Na. 220 ambapo Ibara ya 69 inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 4(a) ili kuainisha kuwa mapato yanayotokana na faida itakayotokana na kushuka kwa bei ya mafuta yatawekwa kwenye mfuko wa dharura uliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura Na. 439.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 70, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 ili kuanzisha tozo mpya ya ushuru wa barabara kwa faida itakayotokana na kushuka kwa bei ya mafuta na ili fedha hizo ziwekwe kwenye mfuko wa dharura.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 21, yenye Ibara ya 72 na 73, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Sura Na. 82 kwa kurekebisha kifungu cha 25, kubainisha kuwa Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote, utatumia pia katika kugharamia matibabu ya wanawake wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ushuru wa bidhaa cha asilimia mbili kinachotokana na vinywaji laini, vileo na vipodozi kupelekwa kwenye mfuko wa bima ya afya, kuainisha kiwango cha asilimia 100 ya mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye kileo cha *ethanol* kinachotambulika kwa *HS Code* 222071000 kutumika kama chanzo cha mfuko wa afya kwa wote.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 22, yenye Ibara 74 hadi 79, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Tasnia Sukari Sura Na. 251 kufanya yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 75, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 ili kuipa mamlaka ya bodi ya sukari kutoza na

kukusanya tozo yakuanzisha kamati kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 76, inapendekeza kuongeza kipengele cha 11(c) ili kuweka utaratibu wa bodi ya sukari kufanya tathimini ya gharama za uzalishaji. Kifungu kipya cha 11(d) kuweka sharti la wazalishaji wa sukari kutangaza majina ya wasambazaji wa sukari kwa kila mkoa na kipengele kinachofuata ni kuweka utaratibu wa Waziri kuanzisha kamati ya ushauri ambayo itashauri kuhusu masuala ya sukari.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 77, inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 13 ili kuweka mashariti ya usajili wa muda wazalishaji wa sukari na viwanda vidogo vidogo vya sukari.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 78, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 14 ili kuweka sharti la kutokutolewa kwa kibali cha kuagiza sukari hadi pale bodi ya sukari itakapojiridhisha kwamba uzalishaji wa sukari nchini upo chini ya mahitaji ya wakati huo.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 79, inapendekeza kuongeza kifungu cha 14(a) ili kuiwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuwa na mamlaka pekee ya kuagiza ndani ya nchi uhifadhi na kusambaza kwa matumizi ya ndani ya nchi wakati wa upungufu wa sukari.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 23, yenye Ibara ya 79, hadi 88 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura Na. 438 kwa kufanya yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 81, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 ili kutoa tafsiri ya msamiati; ukaguzi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 82, inapendekeza kuongeza kifungu cha 34 ili kuwezesha mlipa kodi kutuma nyaraka kwa Kamishina Mkuu kwa njia ya barua pepe.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 83 inapendekeza kuongeza kifungu cha 37, ili kuwezesha ritani za kodi za mashirika ya umma kuthibitishwa na angalau watu wawili.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 86 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 76, ili kuondoa makosa ya marejeo ya vifungu *(cross referencing)*. Lengo la kufanya marekebisho haya ni kuondoa utata wa tafsiri.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Nne yenye Ibara za 89 hadi 91 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408; Kuweka sifa za mtu kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Rufani za Kodi na kumwezesha Waziri kuwapa wajumbe wa Bodi ya Rufani za Kodi mamlaka ya kusikiliza rufaa ambazo hazitoki katika Mikoa walipoteuliwa. Ibara ya 91 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 22, ili kuweka ukomo wa muda wa siku sitini katika utatuzi wa rufani za kodi kwa makubaliano ya hiari.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tano ya Ibara za 92 hadi 102 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148. Naomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu za *Hansard* kama Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

(i) Mheshimiwa Spika, Ibara ya 93 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 2, ili kuongeza tafsiri ya misamiati "*gaming supply*";

(ii) Ibara ya 94 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 6, ili kutoa msamaha kwenye dawa za kutibu na kusafisha maji, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Vifaa na Mitambo ya kuchakata na kuhifadhi mazao ya nyuki;

(iii) Ibara ya 95 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 11, ili kuweka *H.S Code* zilizo sahihi kwa bidhaa za mtaji;

(iv) Ibara ya 96 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 29, ili kuongeza msamiati wa usajili kwa walipakodi wanaoomba kusajiliwa kabla ya kukidhi vigezo;

(v) Ibara ya 97 inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 51, ili kujumuisha huduma za *data* mtandaoni na watoa huduma wasio wakaazi kwenye wigo wa watoa huduma za kielektroniki;

(vi) Ibara ya 99 inapendekeza marekebisho ya *55B,* ili kutoza kodi ya kiwango cha asilimia sifuri kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye mauzo ya bidhaa za nguo zinazotengenezwa ndani;

(vii) Ibara ya 100 inapendekeza kuongeza vifungu vya *55C* na *55D,* ili kutoza kodi ya kiwango cha asilimia sifuri kwenye dhahabu itakayouzwa Benki Kuu;

(viii) Ibara ya 102 inapendekeza kurekebisha Jedwali la mafuta kwa kutoa msamaha wa kodi kwenye chepe na sururu zitakazotumika zenye *HS Code* 8201.10.00;

(ix) Ibara ya 100 inapendekeza kurekebisha Jedwali kwa kuongeza msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye chai itakayozalishwa nchini inayotambulika kwa *HS Code* 0902.30.00;

(x) Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ni kusamehe kodi kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yanayosafishwa mara mbili kwa kutumia mbegu zinazozalishwa hapa nchini.

(xi) Kusamehe kodi kwenye huduma za ndani za matengenezo ya ndege na uunganishwaji kwa ndege pamoja na vipuri yake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Sita yenye Ibara za 103 na 104 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi kwa kurekebisha kifungu cha 19 kwa kujumuisha gharama za vibarua wanaotumika katika utekelezaji wa miradi ya maji inayosimamiwa na mamlaka za maji.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua nyingine za mapato zipo katika Hotuba ya Bajeti na ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada huu, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali *(Government Notices)* kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji Sheria na mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha, ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2024 *(THE FINANCE BILL, 2024)* – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 (The Finance Act, 2024) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

1. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri ili kuuboresha Muswada huu.

2. Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na

mapendekezo mazuri ya Kamati. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa hapa Bungeni jana tarehe 26 Juni, 2024. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waandishi wa Sheria na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Aidha, nawashukuru wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao kuhusu Muswada huu.

3. Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi na nyinginezo ili kuwezesha utekelezaji wa kisheria wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 13 Juni 2024 na iliyopitishwa hapa Bungeni jana tarehe 26 Juni, 2024.

4. Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama ulivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho unakusudia kufanya marekebisho ya Sheria Ishirini na Tano zinazohusu mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali pamoja na taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Muswada huu umelenga kusaidia katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, hususan, katika sekta za kimkakati ikijumuisha viwanda, kilimo, ufugaji na uvuvi, uchukuzi na usafirishaji pamoja na sekta za elimu na afya ili kuboresha uzalishaji na kukuza uchumi wa jumla, kukuza ajira na hatimaye kupunguza ukali wa maisha ya wananchi. Hatua hizi zinalenga pia kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani ya nchi na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, Muswada huu unapendekeza marekebisho kwenye sheria nyingine mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi, ukusanyaji wa mapato ya ndani, kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali na kuboresha mazingira ya biashara.

5. Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho:-

(i) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342;
(ii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;
(iii) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439;
(iv) Sheria ya Korosho, Sura ya 203;
(v) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
(vi) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;
(vii) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
(viii) Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276;
(ix) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
(x) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;
(xi) Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Utozaji Kodi ya Majengo, Sura ya 289;
(xii) Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sura ya 407;
(xiii) Sheria ya Madini, Sura ya 123;
(xiv) Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124;
(xv) Sheria ya Leseni na Usajili wa Viwanda Nchini, Sura ya 46;
(xvi) Sheria ya Afya ya Mimea, Sura ya 133;
(xvii) Sheria ya Bandari, Sura ya 166;
(xviii) Sheria ya Reli, Sura ya 170;
(xix) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
(xx) Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161;
(xxi) Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251;
(xxii) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
(xxiii) Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408;
(xxiv) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na
(xxv) Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura ya 82.

**MAUDHUI YA MUSWADA**

6. Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Ishirini na Sita kama ifuatavyo:-

7. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, yenye Ibara za 1 na 2 inahusu masuala ya utangulizi hususan jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo itaanza kutumika tarehe 1, Julai 2024.

8. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, Tatu na Kumi na Tatu zinapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sura ya 342, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha, Sura ya 407 ili kujumuisha masharti yanayohusiana na marejesho na faida kama mbadala wa kutoza riba. Lengo la marekebisho haya ni kuziwezesha benki, taasisi za kifedha na kampuni zinazojihusisha na utoaji wa huduma ndogo za fedha zisizotoza riba kuweza kutoa huduma za mikopo pasipo kutoza riba.

9. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 kwa kurekebisha kifungu cha 35 ili kujumuisha vyanzo vipya vya mapato katika Mfuko wa dharura ambavyo ni asilimia 50 ya tozo ya maendeleo ya reli (Railway Development Levy), tozo ya ushuru wa barabara itokanayo na faida baada ya kushuka kwa bei za mafuta *(the windfall fuel profit toll)*. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Mfuko wa Dharura kuweza kugharamia matengenezo ya dharura ya miundombinu ya barabara inayoharibika kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

10. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Korosho, Sura ya 203 kwa kurekebisha kifungu cha 17A ili kuelekeza mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi kupelekwa Bodi ya Korosho kwa asilimia 100 kwa kipindi cha miaka mitano. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea maendeleo ya Sekta ya kilimo cha korosho na kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ruzuku na tafiti pamoja na kuongeza mchango wa zao katika ukuaji wa uchumi.

11. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya 14 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 124 ili kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye ada ya matangazo ya biashara ya michezo ya kubahatisha ili kupunguza madhara hasi ya michezo ya kubahatisha kwa jamii na kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa makusanyo ya kodi kwa ajili ya kugharamia Bima ya Afya kwa watu wasio na uwezo na makundi maalum hususan wanawake wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano;

(ii) Ibara ya 15 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 130 ili mzalishaji wa mwisho wa pombe kali aweze kujirejeshea ushuru wa bidhaa aliotozwa kwenye ununuzi wa malighafi ya uzalishaji pombe kali ya kiwango cha pombe zaidi ya asilimia 80 (ethyl alcohol of HS Code 2207.10.00). Lengo la marekebisho haya ni kuepusha mzalishaji wa mwisho wa mvinyo uliochanganywa na pombe kali au pombe kali zilizoorodheshwa chini ya Kundi Na. 2204 au 2208 la bidhaa (Heading 2208) kutotozwa ushuru wa bidhaa mara mbili kwa mujibu wa kifungu hicho cha 130 cha Sheria;

(iii) Ibara ya 15A kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha kifungu cha 137 ili kuainisha muda wa siku ishirini na tano kwa walipa kodi kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ritani ya ushuru wa bidhaa. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

(iv) Ibara ya 16 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 146A ili kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye kilevi kinachotambulika chini ya kundi la bidhaa la HS Code 2207 kwa mtu atakayeizalisha na kuitumia katika uzalishaji wa nishati ya viwandani au kwenye matumizi ya kitabibu au maabara. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza ufanisi

viwandani pamoja na kuimarisha uzalishaji wa dawa za kitabibu na huduma za kimaabara zitokanazo na bidhaa hii kwa gharama nafuu;

(v) Ibara ya 17 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 148 ili kuondoa maneno yanayoleta mkanganyiko kwenye kifungu hicho na kuongeza ufasaha wa utaratibu wa utozaji. Kifungu hicho kinaelekeza kwamba, pale ambapo mfanyabiashara anauza malighafi inayotozwa ushuru wa bidhaa kwenda kwa mzalishaji aliyesajiliwa (registered dealer) ambaye atazalisha bidhaa ya mwisho itakayotozwa ushuru wa bidhaa, yule muuzaji wa mwanzo wa malighafi hatapaswa kutoza ushuru wa bidhaa (excise duty) ili kuondoa uwezekano wa ushuru wa bidhaa kutozwa mara mbili kwenye bidhaa moja;

(vi) Ibara ya 18 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Nne ili:

(a) Kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 300 kwa kilo ya tomato sauce na tomato ketchup (HS Code 2103.20.00) na bidhaa nyingine husika zenye HS Code 2103.90.00 zinazotoka nje ya nchi;

(b) Kupunguza ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 63.80 hadi 56 kwa lita ya maji kwenye maji ya chupa yanayozalishwa nchini. Lengo ni kuchochea ukuaji wa viwanda vidogo vinavyozalisha bidhaa hiyo ili kupunguza gharama kwa mlaji na kuchochea matumizi ya maji safi na salama;

(c) Kutoza ushuru wa bidhaa kwenye bia isiyochujwa yaani Opaque Beer ya mfano wa kibuku na kundi lingine la aina hiyo ya bidhaa inayotokana na matunda mchanganyiko inayoingizwa kutoka nje ya nchi kwa kiwango mfuto cha shilingi 963.90 na shilingi 2,959.74 mtawalia kwa lita. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali ili kugharamia athari hasi zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo;

(d) Kutoza ushuru wa bidhaa kwenye pombe kali yenye kilevi zaidi ya asilimia 80 itakayozalishwa ndani ya nchi na itakayoagizwa nje ya nchi kwa kiwango cha shilingi 5,000 na shilingi 7,000 kwa lita mtawalia. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali na kulinda afya za walaji pamoja na kudhibiti ukwepaji wa ushuru wa bidhaa;

(e) Kutoza ushuru wa bidhaa wa shilingi 500 kwa kilo moja ya rangi za mafuta zitokazo nje ya nchi zinazotambulika chini ya kundi la bidhaa Na. 32.08 (Heading 32.08);

13. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Jedwali la Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196 kwa kurekebisha Jedwali ili kutoza ushuru kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula ya alizeti, mashudu yanayotokana na mbegu za alizeti zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha upatikanaji wa malighafi ya kuzalisha bidhaa za mafuta na sabuni nchini kwa bei nafuu pamoja na kulinda wazalishaji wa ndani. Aidha, kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye bia kimepunguzwa kuwa asilimia 5 na saruji kutoka nje ya nchi itatozwa asilimia 10.

14. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41 kama ifuatavyo;

(i) Ibara ya 22 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 26 ili –

(a) kuweka takwa la watu wanaotaka kufanya biashara ya kuuza na kusambaza tokeni zinazotumika kwenye mashine za michezo ya kubahatisha kuomba leseni. Lengo la marekebisho haya ni kutambua rasmi leseni ya kuuza na kusambaza tokeni; na

(b) kuongeza aina ya leseni kwa mtu yoyote anayetaka kufanya kazi kama wakala wa michezo ya kubahatisha. Lengo la marekebisho haya ni kutambua rasmi shughuli za uwakala wa michezo ya kubahatisha.

(ii) Ibara ya 23 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 73 ili kuzuia matumizi ya sarafu katika michezo ya kubahatisha. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uhai na muda wa matumizi ya sarafu;

(iii) Ibara ya 24 inapendekeza kuweka sharti la kuanza kutumika kwa marekebisho yanayopendekezwa katika Ibara ya 23 ambapo yataanza kuanzia tarehe 1 Aprili, 2025.

15. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276, kwa kuongeza kifungu kipya cha 18A na Jedwali kwa lengo la kuanzisha tozo mpya inayoitwa "Tozo ya Maendeleo ya Viwanda" itakayotozwa kwenye thamani ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na zinazotoka ndani ya Jumuiya ya EAC lakini hazikidhi vigezo vya uasilia. Lengo la marekebisho haya ni kukuza uchumi wa nchi kwa kuongeza uzalishaji na uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi, kutengeneza fursa za ajira na kulinda uzalishaji wa ndani kwa kuwa bidhaa husika zinazalishwa kwa wingi nchini.

16. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya 29 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 ili kuongeza tafsiri ya maneno "mali za kidigitali" "mchimbaji asiye na leseni" "maudhui ya kidigitali" na "mtengeneza maudhui ya kidigitali" kama yanavyopendekezwa kutumika kwenye Sheria ili kuleta maana sahihi iliyokusudiwa. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri sahihi ya misamiati kama ilivyotumika kwenye Sheria;

(ii) Ibara ya 30 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 ili kuondoa takwa la kulipa kodi ya mapato mbadala kwa kampuni zinazochakata mazao ya chai yanayotengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Lengo la marekebisho haya ni

kupunguza gharama kwa wazalishaji wa ndani wa chai ili kuondoa hasara zinazotokana na kushuka kwa bei ya zao hilo kwenye soko;

(iii) Ibara ya 31 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 11 ili kuweka takwa kwa mlipakodi anayedai gharama za manunuzi ya bidhaa na huduma wakati wa kukokotoa kodi ya mapato kudai gharama ambazo zitakuwa na kielelezo cha risiti ya kielektroniki ya kodi isipokuwa pale ambapo muuzaji wa bidhaa au huduma hiyo ni mtu au taasisi iliyo nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au muuzaji amesamehewa kutumia mashine ya kielektroniki ya kodi kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea ulipaji wa kodi wa hiari na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi;

(iv) Ibara ya 32 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 19 ili kuongeza wigo wa mapato yatakayotozwa kodi kutoka asilimia 30 hadi 40 katika mwaka wa nne wa mapato na kuendelea kwa mlipakodi anayepata hasara mfululizo. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Serikali kuongeza makusanyo ya kodi bila kuathiri haki ya mlipakodi kudai hasara alizozipata miaka iliyopita zitakazokuwa zimebakia kwenye miaka itakayofuata ya mapato;

(v) Ibara ya 33 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 56 ili kubainisha kuwa mabadiliko ya umiliki wa kampuni mkaazi uliosababishwa na gawio la hisa mpya hautatozwa kodi ya mapato kwa mujibu wa kifungu hicho. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufasaha na kuboresha usimamizi wa kodi;

(vi) Ibara ya 34 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 64 ili kujumuisha taasisi zinazofanya shughuli za uendelezaji wa afya na utunzaji wa mazingira kwenye wigo wa taasisi zinazokidhi sifa ya taasisi za hisani. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea huduma za hisani kwenye eneo la afya na utunzaji wa mazingira hususan kipindi hiki ambacho dunia inakabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi;

(vii) Ibara ya 35 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 82 ili kujumuisha malipo ya ukodishaji wa vifaa vya ujenzi na mitambo kwenye wigo wa mapato yanayokatwa kodi ya zuio. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa kodi ya zuio na kupanua wigo wa kodi;

(viii) Kuiondoa taasisi ya fedha mkaazi kwenye wajibu wa kukata kodi ya mapato kwenye malipo ya riba yatakayokwenda kwa taasisi ya kifedha ya nje ya nchi au mfuko wa fedha usio mkaazi, kutokana na mkopo ambao taasisi ya fedha mkaazi imekopa kutoka taasisi ya fedha au mfuko usio mkaazi, ambayo imeingia mkataba na Serikali kutoa mkopo wa riba nafuu kwa taasisi mkaazi za kifedha kwa lengo la kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wananchi, isipokuwa tu pale taasisi hiyo ya kifedha mkaazi inamilikiwa na au kumiliki taasisi au mfuko huo usio mkaazi;

(ix) Ibara ya 36 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 83 ili kutoza kodi ya mapato kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo yatakayofanywa kwa ajili ya ununuzi wa madini ya viwandani na madini ya metaliki, isipokuwa chumvi na madini yenye thamani yanayouzwa na mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji wa madini. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi;

(x) Ibara ya 37 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 83 kwa:-

(a) kuongeza kifungu kipya cha 83B ili kumpa mlipakodi mkaazi au asiye mkaazi wajibu wa kuzuia kodi kwa kiwango cha asilimia 5 kwenye malipo yanayofanywa na mtengeneza maudhui mkaazi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi;

(b) ubadilishanaji wa mali za kidigitali au inayowezesha ubadilishanaji wa mali za kidigitali, kuzuia kodi kwa kiwango cha asilimia 3 kwenye malipo yatakayofanywa kwa mlipakodi mkaazi kutokana na mauzo ya mali ya kidigitali. Lengo la marekebisho haya ni kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi;

Ibara ya 38 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 86 ili mfanyabiashara wa kati aliyeuza mazao yatokanayo na kilimo, ufugaji, uvuvi na misitu ambaye amekatwa kodi, makato yake kutambuliwa kuwa malipo ya mwisho ya kodi ya mapato yake katika biashara yake hiyo ya mazao.

(xi) Ibara ya 39 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90 ili kuziondoa taasisi kwenye utaratibu mbadala wa kulipa kodi ya ziada ya mtaji unaomhusu mlipakodi ambaye hana kumbukumbu za gharama za mali. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha taasisi kutunza kumbukumbu na kuimarisha uhiari wa kutii sheria za kodi;

(xii) Ibara ya 40 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 91 ili kuziwezesha taasisi za umma, ambazo hesabu zake zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na ambazo zinawajibika kulipa kodi, kuwasilisha ritani za kodi ya mapato baada ya miezi 9 tangu mwaka wa hesabu kufungwa badala ya utaratibu wa miezi 6 unaotumika kwa makampuni, kwani kwa mujibu wa utaratibu wa ukaguzi kwa mashirika ya umma taarifa ya ukaguzi huwa tayari baada ya kipindi cha miezi 6;

(xiii) Ibara ya 41 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 92 ili kumuondolea mlipakodi binafsi ambaye si mkaazi mwenye mapato yanayotokana na ajira takwa la kuwasilisha ritani ya kodi. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa wa utozaji baina ya walipakodi wakaazi na wasio wakaazi;

(xiv) Ibara ya 42 inapendekeza kurekebisha kifungu cha Jedwali la Kwanza ili kuboresha madaraja na viwango vya kodi ya mapato kwa mlipakodi binafsi anayefanya biashara ya usafirishaji wa abiria. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha usawa wa kodi na kuimarisha ulipaji kodi wa hiyari;

(xv) Ibara ya 43 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuongeza ufasaha katika Aya ya 2(3) inayoweka utaratibu wa kudai ushuru wa uchakavu wa mwanzo

(initial allowance) wa asilimia hamsini, kwamba mfanyabiashara atadai ushuru huo kwa awamu mbili zilizo sawa, yaani mwaka wa kwanza asilimia 25, na mwaka unaofuata asilimia 25;

17. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja na Kumi na Mbili inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289 ili asilimia 20 ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo ilipwe kwenye akaunti za mamlaka za serikali za mitaa ndani ya halmashauri husika. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha mamlaka za serikali za mitaa kupata fedha za kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo kwa wakati ili kugharamia masuala ya ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo kwa ufanisi na kwa wakati.

18. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne yenye Ibara za 50 hadi 55 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123 kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya 51 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 59 ili kuweka takwa la wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini na wafanyabiashara wa madini kutenga kiasi cha dhahabu kwa ajili ya kuchakatwa, kuyeyushwa, kusafishwa na kuuzwa nchini. Aidha, kiasi kitakachopaswa kutengwa kitabainishwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya madini kwenye kanuni, ambapo kwa kuanzia kiasi cha asilimia 20 ya sehemu ya dhahabu inayozalishwa nchini kitapaswa kutengwa. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza akiba ya fedha za kigeni nchini na kupunguza tatizo la uhaba wa fedha za kigeni. Vilevile, hatua hii inalenga pia kuchochea ukuaji wa viwanda vya kusafishia dhahabu kwa kuhakikisha vinapata dhahabu ya kusafisha ikiwa ni moja ya hatua za kupata ithibati za kimataifa;

(ii) Ibara ya 52 inapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 72A ili kuwianisha masharti ya Sheria ya Madini na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ili kuitambua Benki Kuu ya Tanzania kama mnunuzi wa

madini nchini. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha na kuongeza urahisi wa Benki Kuu ya Tanzania kununua dhahabu ili kuongeza akiba ya nchi ya dhahabu na fedha za kigeni;

(iii) Ibara ya 53 na 54 zinapendekeza kuongeza kifungu kipya cha 87 na 89 ili:-

(a) kupunguza mrabaha unaotozwa kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania kutoka asilimia sita hadi asilimia nne;

(b) kuweka takwa la malipo ya mrabaha unaolipwa kwenye madini ya dhahabu yanayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania kuwa ni malipo ya mwisho. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha uuzaji wa dhahabu kwa Benki Kuu ya Tanzania kwa lengo la kuongeza akiba ya nchi ya fedha za kigeni na kupunguza tatizo la upatikanaji wa fedha za kigeni. Aidha, marekebisho haya yanalenga kuleta usawa baina ya vituo vya kusafishia dhahabu na Benki Kuu ya Tanzania kwa kuwa tayari vituo hivyo vinanufaika na msamaha.

(iv) Ibara ya 55 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 90A ili kutoa msamaha wa kulipa ada ya ukaguzi ya asilimia moja kwa kwa mtu atakayeiuzia dhahabu Benki Kuu ya Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za ununuaji wa madini na kuhamasisha uuzaji wa dhahabu kwa Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, hatua hii itaongeza akiba ya fedha za kigeni na kupunguza tatizo la upatikanaji wa fedha za kigeni.

19. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano yenye Ibara za 56 na 57 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura 123 kwa kurekebisha Jedwali la Kwanza ili kujumuisha magari ya umeme pamoja na vyombo vingine vya moto kwenye wigo wa ulipaji wa ada ya usajili wa magari na vyombo hivyo vingine. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato ya Serikali, kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi na kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

20. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita yenye Ibara za 58 na 59 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Leseni na Usajili wa Viwanda Nchini, Sura ya 46 kwa kuongeza kifungu kipya cha 17A ili kuweka sharti kwa wamiliki wa viwanda vilivyosajiliwa au vyenye leseni kuingia mikataba ya Utekelezaji na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha. Aidha, sharti hili litawahusu watu na taasisi zote ambazo zimesajiliwa au zenye leseni chini ya Sheria husika na ambazo zimepewa vyeti chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania na kupewa misamaha mbalimbali ya kikodi ikiwemo unafuu wa kulipa kodi kwa kiwango cha asilimia sifuri wa kodi ya ongezeko la thamani, msamaha wa ushuru wa forodha chini ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki, msamaha dhidi ya masharti ya viwango vya forodha vya Afrika Mashariki.

21. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba yenye Ibara za 60 na 61 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Afya ya Mimea, Sura ya 133 kwa kuongeza kifungu kipya cha 35A ili kuipa mamlaka Taasisi ya Mimea jukumu la kukusanya ada kwenye huduma ya ukaguzi mimea, mazao ya mimea au bidhaa zilizo chini ya udhibiti zinazoingizwa nchini au kusafirishwa nje ya nchi. Aidha, marekebisho haya yanakusudia kuainisha mgawanyo wa ada itakayokusanywa ambapo asilimia 70 ya ada itakayokusanywa itapelekwa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, na asilimia thelathini itakayobaki itapelekwa Mfuko Mkuu wa Hazina. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya majukumu mbalimbali ya Serikali.

22. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane yenye Ibara za 62 na 63 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bandari, Sura ya 166 kwa kurekebisha kifungu cha 67 ili kurejesha jukumu la kukusanya tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari (wharfage) kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Aidha, mapato yanayotokana na tozo hii yatawekwa katika akaunti maalum ya TPA iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na matumizi yake yatafanyika baada ya omba na kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa

Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha TPA kupata fedha kwa wakati kwa ajili ya maboresho ya miundombinu ya Bandari.

23. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tisa yenye Ibara za 64 na 65 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Reli, Sura ya 170 kwa kurekebisha kifungu cha 68 ili kuongeza kiwango cha tozo ya maendeleo ya reli kinachotozwa kwa bidhaa zinazoingia na kutumika nchini kutoka asilimia 1.5 hadi asilimia 2 ya thamani ya mzigo. Aidha, asilimia 50 ya mapato yatakayotokana na chanzo hicho yatapelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Reli na asilimia itapelekwa kwenye Mfuko wa Dharura. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato yatakayotumika katika kuboresha na kujenga miundombinu ya reli na Barabara zilizoathiriwa na mvua za majanga.

24. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini yenye Ibara za 66 hadi 71 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220 kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya 69 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 4A ili kuainisha kuwa mapato yanayotokana na faida itokanayo na kushuka kwa bei ya mafuta yatawekwa katika Mfuko wa Dharura ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura 439 na yatatumika kwa ajili ya matengenzo ya miundombinu ya Barabara.

(ii) Ibara ya 70 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 7 ili kuanzisha tozo mpya ya ushuru wa barabara kwa faida itokanayo na kushuka kwa bei ya mafuta ili fedha hizo ziwekwe kwenye Mfuko wa Dharura. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza mapato yatakayotumika katika kufanya matengenezo ya Barabara.

25. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Moja yenye Ibara za 72 na 73 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 82 kwa kurekebisha kifungu cha 25 ili:-

(i) kubainisha kuwa Mfuko wa Bima ya Afya kwa wote utatumika pia katika kugharamia matibabu ya wanawake wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano;

(ii) kuainisha kiwango cha ushuru wa bidhaa cha asilimia mbili kinachotokana na vinywaji laini, vileo na vipodozi kupelekwa Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote kwa ajili ya kugharamia matibabu ya watu wasiojiweza pamoja na wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano;

(iii) kuainisha kiwango cha asilimia mia moja ya mapato yanaotokana na ushuru wa bidhaa kwenye kileo cha ethyl asili kinachotambulika kwa HS Code 2207.10.00 kutumika kama chanzo cha Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

26. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili yenye Ibara za 74 hadi 79 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251 kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Ibara ya 75 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 ili kuipa mamlaka Bodi ya Sukari ya kutoza na kukusanya tozo na kuanzisha Kamati kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake;

(ii) Ibara ya 76 inapendekeza kuongeza:-

(a) Kifungu kipya cha 11C ili kuweka utaratibu kwa Bodi ya Sukari kufanya tathmini gharama za uzalishaji;

(b) Kifungu kipya cha 11D ili kuweka sharti kwa wazalishaji wa sukari kutangaza majina ya wasambazaji wa sukari kwa kila mkoa;

(iii) Kuweka utaratibu kwa Waziri kuanzisha Kamati ya Ushauri ambayo itashauri kuhusu masuala ya sukari;

(iv) Ibara ya 77 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 13 ili kuweka masharti ya usajili wa muda kwa wazalishaji wa sukari, viwanda vidogo vya sukari;

(v) Ibara ya 78 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 14 ili kuweka sharti la kutotolewa kwa kibali cha kuingiza sukari hadi pale Bodi ya Sukari itakapojiridhisha kwamba, uzalishaji wa wa sukari nchini upo chini ya mahitaji kwa wakati huo;

(vi) Ibara ya 79 inapendekeza kuongeza kifungu cha 14A ili kuiwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kuwa na mamlaka pekee ya kuingiza ndani ya nchi, kuhifadhi na kusambaza kwa matumizi ya ndani ya nchi wakati wa upungufu wa sukari. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha upatikanaji wa sukari nchini na kuondoa uhodhi kwa baadhi ya wenye viwanda bila kuathiri dhamira ya Serikali ya kulinda viwanda vya ndani;

27. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tatu yenye Ibara za 79 hadi 88 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Ibara ya 81 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 3 ili kutoa tafsiri ya msamiati "ukaguzi wa kikodi" ili kuongeza mawanda ya ukaguzi wa kodi ili kujumuisha mapitio na ukaguzi. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata wa matumizi ya misamiati hiyo na kurahisisha usimamizi wa kodi.

Aidha, inapendekezwa kutoa tafsiri ya msamiati "Cargo Consolidator". Lengo ni kujumuisha "Cargo Consolidator" katika wigo wa kulipa kodi;

(ii) Ibara ya 82 inapendekeza kuongeza kifungu cha 34 ili kumwezesha mlipakodi kutuma nyaraka kwa Kamishna Mkuu kwa njia ya barua pepe au njia nyingine za kielektroniki. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha usimamizi wa kodi na kupunguza gharama;

(iii) Ibara ya 83 inapendekeza kuongeza kifungu cha 37 ili kuwezesha ritani za kodi za mashirika ya umma kuthibitishwa na angalau watu wawili;

(iv) Ibara ya 84 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 51 ili kuongeza ufasaha wa kifungu hicho kwa kubainisha mazingira ambayo yatampa uhakika Mlipakodi wa tarehe au siku ambayo pingamizi lake la kodi limepokelewa rasmi na Kamishna Mkuu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa hata kama hatakuwa amepewa uthibitisho wa maandishi juu ya kupokelewa kwa pingamizi lake;

(v) Ibara ya 85 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 73 ili kuruhusu Kamishna Mkuu kufanya marejesho ya kodi pale ambapo mlipakodi ameomba kwa maandishi marejesho ya kodi iliyolipwa kwa ziada. Lengo la marekebisho haya ni kurahisisha utaratibu wa marejesho ya kodi iliyolipwa;

(vi) Ibara ya 86 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 76 ili kuondoa makosa ya marejeo ya vifungu (cross referencing). Lengo la marekebisho haya ni kuondoa utata wa tafsiri ya kifungu husika unaoletwa na makosa hayo ya marejeo;

(vii) Ibara ya 87 kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufuta pendekezo la la kurekebisha Kifungu cha 86(1) lililokuwa linaweka ukomo wa faini ya juu ya kosa la kutokutoa risiti wa kiasi cha currency points 1000 (sawa na shilingi 15,000,000) na badala yake kuweka ukomo wa faini ya juu ya kosa hili kuwa currency points 200 (sawa na shilingi 4,000,000). Lengo la marekebisho haya ni kutoleta mkanganyiko katika ulipaji wa adhabu zitokanazo na kutotoa au kudai risiti.

(viii) Ibara ya 88 inapendekeza kurekebisha Jedwali la Pili ili kuongeza kiwango cha mfuto cha kukokotoa adhabu kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 20,000. Lengo la marekebisho haya ni kuhuisha kiwango cha faini kwa adhabu zinazotolewa chini ya sheria ili kuendana na thamani ya fedha.

28. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Nne yenye Ibara za 89 hadi 91 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408 kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya 90 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 4 ili:-

(a) kuweka sifa za mtu kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Rufani za Kodi. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha kupatikana kwa wajumbe wenye sifa na uzoefu wa kutosha katika kutekeleza majukumu ya kazi za mwenyekiti wa Bodi; na

(b) kumwezesha Waziri kuwapa wajumbe wa Bodi ya Rufani za Kodi mamlaka ya kusikiliza rufaa ambazo hazitoki katika mikoa walipoteuliwa.

(ii) Ibara ya 91 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 22 ili kuweka ukomo wa muda wa siku sitini katika utatuzi wa rufani za kodi kwa makubaliano ya hiari (amicable settlement) baina ya mrufani na mjibu rufani. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza ufanisi na kuharakisha utatuzi wa rufani za kodi zilizopo kwenye Bodi na Baraza la Rufani za Kodi.

29. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tano yenye Ibara za 92 hadi 102 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 kama ifuatavyo:-

(i) Ibara ya 93 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 2, ili kuongeza tafsiri ya misamiati "gaming supply" "online data services" na "serviced apartment" kama yanavyopendekezwa kutumika kwenye sheria. Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri sahihi ya misamiati hiyo kama ilivyotumika kwenye sheria;

(ii) Ibara ya 94 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 6 ili kutoa msamaha kwenye madawa ya kutibu na kusafisha maji na dira za maji kwa mamlaka za maji baada ya idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya maji. Lengo la marekebisho haya ni kufanikisha utoaji wa huduma ya maji safi na salama nchini.

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Vifaa na Mitambo ya kuchakata na kuhifadhi mazao ya nyuki.

(iv) Ibara ya 95 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 11 ili kuweka H.S Code zilizo sahihi kwa bidhaa za mtaji zinazopewa ahirisho la kodi (VAT deferment);

(v) Ibara ya 96 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 29 ili kuongeza masharti ya usajili kwa walipakodi wanaoomba kusajiliwa kabla ya kukidhi vigezo vya usajili kwa minajili kwamba watakidhi vigezo hivyo watakapoanza uzalishaji (intending VAT trader registration);

(vi) Ibara ya 97 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 51 ili kujumuisha huduma za data mtandaoni na watoa huduma wasio wakaazi kwenye wigo wa huduma za kielektroniki zinazotozwa kodi ya ongezeko la thamani. Lengo la marekebisho haya ni kutanua wigo wa kodi na kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia;

(vii) Ibara ya 98 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 55A ili kutoza kodi kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye mauzo ya mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Lengo la marekebisho haya ni kutoa nafuu kwa wakulima na kuchochea uzalishaji wa ndani;

(viii) Ibara ya 99 inapendekeza kurekebisha kifungu cha 55B ili kutoza kodi kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye mauzo ya bidhaa za nguo zilizotengenezwa ndani ya nchi kwa kutumia pamba iliyolimwa nchini. Lengo la marekebisho haya ni kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani vinavyochakata bidhaa za pamba;

(ix) Ibara ya 100 inapendekeza kuongeza vifungu vya 55C na 55D ili kutoza kodi ya kiwango cha asilimia sifuri kwenye dhahabu inayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania pamoja na viwanda vya ndani vyenye leseni ya kuchakata (refine) dhahabu. Lengo la marekebisho haya ni kuhamasisha wazalishaji na wasambazaji wa dhahabu kuiuzia Benki Kuu ili kukidhi mahitaji ya dhahabu, kwa ajili ya kuimarisha akiba ya dhahabu na fedha za kigeni pamoja na kukabiliana na uhaba wa fedha za kigeni. Halikadhalika kuwezesha

viwanda vya ndani vya uchakataji dhahabu kuzalisha dhahabu safi zilizoongezwa thamani na hivyo kuongeza mapato, ajira, technolojia ya uchakataji madini na kuimarisha uchumi;

(x) Ibara ya 100 inapendekeza kurekebisha Jedwali la kwanza kwa kuongeza msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa chai inayozalishwa nchini zinazotambulika katika HS Code 0902.30.00 na 0902.40.00.

(xi) Ibara ya 102 inapendekeza kurekebisha Jedwali ili:-

(a) Kufuta msamaha wa kodi kwenye chepe na sururu zinazotambulika katika HS Code 8201.10.00 na 8201.30.00. Lengo ni kupunguza misamaha isiyo na tija, kulinda mapato ya serikali na kupunguza matumizi yanayohusiana na utoaji wa misamaha ya kodi;

(b) kujumuisha magari pamoja na vifaa vinavyotumiwa na Jeshi la Wananchi (military and armed forces) katika msamaha. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha Jeshi la Wananchi kutekeleza majukumu yake ya ulinzi na usalama wa nchi. Aidha, msamaha husika utatolewa baada ya kupata uthibitisho wa Waziri mwenye dhamana ya masuala ulinzi ili kuhakikisha unatumika kwa manufaa ya Jeshi la Wananchi na si vinginevyo;

(c) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uingizwaji wa vifaa vya kiteknolojia kwa ajili ya kuwasaidia waamuzi (Video Assistant Referee equipment and accessories). Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha nchi inapata vifaa muhimu vya michezo kwa kuzingatia kuwa, Tanzania ni moja ya nchi mwenyeji zitakazohusika katika maandalizi ya michuano ya fainali ya kuwania kombe la mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027 na hivyo kunufaika na ongezeko la akiba ya fedha za kigeni, kukuza taswira ya nchi kimataifa na uwepo wa fursa kwa makampuni ya ndani kutangaza biashara zao. Aidha, msamaha huu utatolewa baada ya vifaa hivyo kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana ya masuala

ya michezo ili kuhakikisha kuwa msamaha huo unatumika kama ilivyokusudiwa na si vinginevyo;

(d) Kusamehe kodi kwa kipindi cha mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yanayosafishwa mara mbili kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini. Lengo la marekebisho haya ni kutoa unafuu kwa mlaji;

(e) Kusamehe kodi kwenye huduma za ndani za matengenezo ya ndege, uunganishaji na utengenezaji wa ndege pamoja na vipuri vitakavyonunuliwa au kuingizwa kutoka nje ya nchi na wazalishaji wa ndani. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea ukuaji wa sekta ya anga na utalii nchini;

(f) Kusamehe kodi kwenye madawa ya kutibu na kusafisha maji, ununuzi na uingizaji wa dira za maji na huduma ya uondoshaji maji taka. Msamaha huu unatolewa kwa mamlaka za maji safi na maji taka baada ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya maji. Lengo la marekebisho haya ni kufanikisha utoaji wa huduma ya maji safi na salama nchini;

(g) Kujumuisha trekta lenye ekseli moja linalotambulika kwa HS Code 8701.10.00 kwenye wigo wa zana na vifaa vya kilimo vinavyopata msamaha wa kodi. Lengo la marekebisho haya ni kuakisi mawanda ya bidhaa zilizosamehewa kodi pamoja na kuoanisha HS Code zilizomo kwenye viwango vya pamoja vya ushuru wa Jumuiya ya Afrika Mashariki vya mwaka 2017 na vile vilivyomo kwenye kitabu cha mwaka 2022.

30. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Sita yenye Ibara za 103 na 104 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura ya 82 kwa kurekebisha kifungu cha 19 ili kutojumuisha gharama za vibarua wanaotumika katika utekelezaji wa miradi ya maji inayosimamiwa na mamlaka za maji katika wigo wa kukokotoa kodi ya kuendeleza Ufundi Stadi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi na kuongeza ufanisi wa usambazaji wa maji nchini.

31. Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua nyingine za mapato zilizopo katika Hotuba ya Bajeti na ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada huu, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali (Government Notices) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika.

**HITIMISHO**

32. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

33. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri. Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, aje awasilishe maoni ya Kamati yetu ya Bunge. Mwenyekiti karibu. *(Makofi)*

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024. Naomba Taarifa yote kama ilivyowasilishwa iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Juni, 2024 Muswada wa Sheria ya Fedha ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni na kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) iliuelekeza Muswada huo kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kuufanyia kazi na kutoa maoni yake Bungeni. Aidha, kama zilivyokuwa Kanuni za Bunge Muswada huo uliwasilishwa rasmi kwenye Kamati tarehe 21 Juni, 2024 na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2024 unakusudiwa kufanya marekebisho ya Sheria 25 zenye lengo la; Kuboresha mfumo wa kodi, kuongeza mapato ya Serikali, kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, kulinda viwanda vya ndani, kuchochea uzalishaji wa sekta mbalimbali na kuimarisha usimamizi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegusa sekta mbalimbali hususani viwanda, madini, kilimo, mifugo, uchukuzi, fedha, afya, mazingira na michezo. Kamati ilipitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui na kupendekeza marakebisho katika maeneo yaliyohitaji maboresho. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023, Kamati ilikutana na Wadau *(public hearing)* kuanzia tarehe 23 hadi 25 Juni, 2024 ili kupokea maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, wadau wafuataao walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni. Naomba niwatambue Wadau kama ifuatavyo: *Tanzania Private Sector Foundation, The Spirit Industry, Prance International Trade Co.Limited, Urhome Company Limited (Good One), Geita Gold Refinery (GGR), Tanzania Human Rights Defenders Coalition , M.M Integrated Steel Mills Limited, Lodhia Industries, Tanzania Fishers Union, Simba Cement, Dangote Cement, Tanzania Sugar Producers Association,* Wadau Binafsi, *National Commercial Bank of Africa, Confederation of Tanzania Industries , Mount Meru Millers, Tanzania Sports Betting Association, Media Bay, Eliya Foods and Overseas Limited, Legal Human Rights Centre, Tanzania Commercial Poultry Association*, Umoja wa Shule Binafsi,

Waagizaji wa *Undenatured Ethyl Alcohol Tanzania, Multi- Colour Corporation, Tanzania Milk Association, Tanzania Chambers of Mining, AIM Trailers Manufacturing Limited, Tanzania Chamber of Commerce,* Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, *Tanzania Bankers Association* na Wadau wa Gesi Asilia. Pia, Kamati ilipokea maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wa tatu ambao ni Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya maandishi na barua pepe kutoka kwa Jukwaa la Hedhi Salama Tanzania, Watu Binafsi na *Tanuk Africa LTD*. Aidha, kwa mara ya kwanza Kamati ya Bajeti imepokea maoni kutoka Jumuiya ya Watanzania Waishio Nje ya Tanzania. Kama kuenzi mchango wa *Diaspora* katika kuhakikisha Taifa linapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea na kuchakata maoni ya wadau, iliandaa bangokitita lenye maoni ya Kamati kuhusu Muswada na kuliwasilisha kwa Serikali. Aidha, Kamati ilikutana na Serikali jana tarehe 26 Juni, 2024, ili kufanya majumuisho kuhusu maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri waliofika kwenye vikao hivyo ni Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Anthony Mavunde, Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri Madini na waliambatana na Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Wataalam mbalimbali kutoka Serikalini. Kamati inawashukuru kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Sheria ya Bajeti, Sura ya 439: Kamati ilikubaliana na mabadiliko yaliyopendekezwa katika Sheria hii yaliyokuwa na lengo la kuongeza vyanzo vya mapato ili kuwezesha Mfuko wa Dharura

*(Contingency Fund)* kugharamia matengenezo ya dharura ya miundombinu ya barabara inayotokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, Kifungu cha 35(1) kinarekebishwa ili kujumuisha vyanzo vipya vya mapato. Vyanzo hivo ni:-

(a) Tozo ya maendeleo ya reli;

(b) Mapato yatokanayo na tofauti kati ya kushuka kwa bei ya mafuta *(The windfall gains in fuel price decrease);*

(c) Asilimia moja ya matumizi ya Serikali kila mwezi; na

(d) Vyanzo vingine vitakavyopangwa na Waziri mwenye dhamana ya fedha.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa aya *(d)* kwa hofu kwamba kingeweza kutumika vibaya. Serikali iliridhia mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali ambayo yameletwa leo hii.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yenye lengo la kuainisha vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote ili kugharamia matibabu ya Watu wasiokuwa na uwezo. Hata hivyo, Kamati haikukubaliana na pendekezo lililopo kwenye Ibara ya 25*(c)* ya chanzo kinachotokana na bima ya vyombo vya moto kwa sababu kimsingi bima ni kinga dhidi ya majanga ikiwemo afya hivyo si busara kutoza chanzo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147; Kamati ilifanya uchambuzi na kutoa mapendekezo yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye ada ya matangazo ya biashara ya michezo ya kubahatisha; Serikali inapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye ada ya matangazo ya biashara ya

michezo ya kubahatisha. Mapato yatakayotokana na tozo hiyo zitaelekezwa katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Kamati inaiona ni jambo jema ambalo linaenda kufanikisha azma ya Serikali ya watu wote nchini hasa wale wasio na uwezo kuweza kupata huduma za kiafya bure.

Mheshimiwa Spika, Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia kumi kwenye thamani ya dau la kamari katika michezo ya kubahatisha na bahati nasibu ya Taifa; Serikali inapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye thamani ya dau la kamari. Hatua hii itasababisha wachezaji wa kamari walioko nchini kushawishika kucheza katika kampuni za nje ambazo hazijasajiliwa nchini kwetu. Ukizingatia hadi hivi sasa hatuna Bahati Nasibu ya Taifa, hivyo ni dhahiri kwamba uamuzi huu hautaleta manufaa yanayokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye Ethani inayotambulika kwa *HS Code* 2207, Serikali inapendekeza kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye ethani inayotambulika kwa *HS Code 2207* kwa mtu atakayezalisha na kutumia katika uzalishaji wa nishati ya viwandani, matumizi ya kitabibu au maabara. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba mapendekezo ya Serikali hayajabainisha ni kwa namna gani waagizaji na wazalishaji watakapokuwa wanauza ethani kwa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kama vile pombe kali watarejeshewa vipi kodi waliyokwishalipa wakati wa uingizaji au uzalishaji wa ethani.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa changamoto ya mlundikano wa marejesho, Kamati ilipendekeza kwamba ushuru wa bidhaa kwenye ethani inayotambulika kwa *HS Code 2207* ulipwe pindi mzalishaji wa ndani au mfanyabiashara anayeingiza ethani kutoka nje anapomuuzia mzalishaji anaetumia ethani kuzalisha bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Ushuru wa bidhaa kwenye ethani yenye kilevi zaidi ya asilimia 80; Ibara ya 18 aya ya *(f)* Serikali inapendekeza

kutoza ushuru wa bidhaa kwenye ethani yenye kilevi zaidi ya asilimia 80 inayozalishwa ndani ya nchi kwa shilingi 5,000 na shilingi 7,000 kwa lita kwa ethani itakayoagizwa kutoka nje. Ushuru unaopendekezwa kwa malighafi hii ni mkubwa kuliko bidhaa za pombe zinazozalishwa na ethani ambazo zinazotozwa ushuru wa shilingi 2,300 hadi 2,600 kwa lita. Hivyo, Kamati inapendekeza kufuta maneno Tsh. 5,000 na Tsh. 7,000 yaliyoko katika jedwali *column* ya sita na kuweka maneno Tsh. 2,500 na Tsh. 3,500 badala ya Tsh. 5,000 na Tsh. 7,000. Hatua hii itapunguza ushuru wa Serikali kutoka shilingi 5,000 inayopendekezwa hadi shilingi 2,500. Aidha, itapunguza shilingi 7,000 inayopendekezwa kwa bidhaa za nje hadi shilingi 3,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276; Katika Sheria hii Serikali inakusudia kuanzisha Tozo ya Maendeleo ya Viwanda *(Industrial Development Levy)* kwa baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini. Hatua hii ni ya kupongeza kwa sababu ni mbinu ya ziada ya kuvilinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani usio sawa wa bidhaa zinazotoka nje na kuchochea mauzo nje ya nchi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali fedha zitakazotokana na tozo hiyo zisaidie vilevile kuendeleza sekta ya viwanda nchini hasa vile viwanda vidogo na vya kati. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa bidhaa zinazotozwa kodi hii kwa kuangalia hasa zile bidhaa zinazozalishwa nchini kwa wingi. Kamati ilipendekeza bidhaa za *clinker* ziongezwe kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332; Sheria hii inafanyiwa marekebisho mbalimbali ambayo ni:-

(i) Kuongeza tafsiri ya maneno, “mali za kidigitali” “mchimbaji asiye na leseni” “maudhui ya kidigitali” na “mtengeneza maudhui ya kidigitali”. Hii ni kutokana na kuwa maudhui ya kidigitali sasa kwenda kutozwa kodi ya zuio ya asilimia tatu na tano na hivyo kutanua wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za utozwaji wa kodi. Hivyo, Serikali iliona ni vema kuweka tafsiri ya misamiati husika ambayo awali haikuwepo. Kamati inaipongeza

Serikali kwa kuendelea kutanua wigo wa kodi ili iweze kukusanya zaidi kwa kufikiria uanzishwa wa kodi mpya na kutoza maeneo yanayoibukia.

(ii) Kuondoa takwa la kulipa kodi ya mapato mbadala kwa kampuni zinazochakata mazao ya chai yanayotengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo inaenda kunusuru sekta ya chai nchini ambayo kwa sasa inakabiliana na changamoto ya kushuka kwa bei ya zao la chai kwenye soko na hivyo wazalishaji kupata hasara.

(iii) Kujumuisha Taasisi zinazofanya shughuli za uboreshaji wa huduma za afya *(advancement of health)* na utunzaji wa mazingira kwenye wigo wa Taasisi zinazotoa huduma za hisani *(Charitable Organizations)* ili ziweze kupata nafuu ya ukokotoaji wa Kodi ya Mapato kulingana na matakwa ya Sheria. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo itachochea na kuvutia huduma za hisani kwenye maeneo husika. Serikali ione umuhimu wa kuongeza pia huduma zenye sura za taasisi hisani kama vile huduma za kisheria ili kuongeza upatikanaji wa huduma hizo kwa wingi ukizingatia kuwa kwa asilimia kubwa huwa zinatolewa bure.

(iv) Kuruhusu michango ya 15% inayolipwa na Taasisi za Serikali kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kuwa miongoni mwa sehemu ya gharama za Taasisi kwenye ukokotoaji wa kodi ya mapato *(deductible expenditure)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho hayo ambayo imekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa taasisi na mashirika ya Serikali ambapo ilikuwa inaonekana kama zinatozwa kodi mara mbili. Kupitia marekebisho haya, sasa mashirika na taasisi husika yanaenda kubakiwa na mapato mengi ikilinganishwa na hapo awali.

(v) Kutoa msamaha wa kodi ya zuio kwenye malipo ya riba kwa taasisi ya fedha mkaazi inapolipa Taasisi au Mfuko uliopo nje ya nchi. Ili Taasisi iliyopo nchini iweze kupata msamaha huo ni lazima iwe imepata mikopo nchini kwa riba ya chini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Seriali ambayo yana nia njema ya kuvutia mitaji kwenye sekta ya kibenki nchini hata hivyo, iliitaka Serikali kutoa tafsiri ya maneno *'low interest rate'* na Serikali ilipokea ushauri huo. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuondoa mapendekezo yafuatayo katika Muswada: -

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 37 inayopendekeza kifungu kipya cha 83 D, kinachokusudia kuanzisha Kodi ya Zuio ya asilimia mbili kwenye malipo yatakayofanywa na wafanyabiashara wa kati *(Middlemen)* kutokana na ununuzi wa bidhaa za kilimo, ufugaji, uvuvi na misitu. Kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza mwaka 2021/2022 wakati pendekezo hilo lilipoanzishwa kwa mara ya kwanza, Kamati ilishauri Serikali kufuta Kifungu hiki na Serikali iliridhia. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 38 ya Muswada inayopendekeza kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya zuio ya asilimia mbili kwenye malipo wanayolipwa na watu binafsi kama vile wapagazi, wapishi, waongoza watalii na huduma ya kubeba mizigo kwa watalii. Kamati iliona ni busara pendekezo hilo likaondolewa ukizingatia kuwa bado sekta hii inaimarika kufuatia janga la Uviko-19. Kamati iliishauri Serikali kufuta kifungu hiki na Serikali iliridhia. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuelekeza mapato ya ziada *(windfall profit)* kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Barabara. Hata hivyo, Kamati haikukubaliana na uanzishwaji wa ushuru shilingi 382 kwa kila kilo ya gesi asilia inayotumika kwenye magari. Kamati imefikia uamuzi huu kwa kuzingatia kuwa sekta ya gesi bado ni changa na inaendelea kukua taratibu na hadi sasa haijaweza kutumika kikamilifu nchini kutokana na gharama za kufunga mifumo ya kutumia gesi pamoja na uhaba wa vituo vya kujazia gesi. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kuondoa pendekezo hili na Serikali iliridhia. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vinavyotumika kuunganisha mfumo wa gesi ili kupunguza gharama za kusimika mfumo huu kwenye magari ambayo kwa sasa gharama za ufungaji zinakadiriwa kuwa kati ya shilingi milioni mbili hadi tatu kiwango ambacho ni kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251. Ili kuweza kufanya maamuzi katika mapendekezo ya Serikali kuhusu Sheria hii Kamati ilikutana na Bodi ya Sukari, Wazalishaji wa Sukari pamoja na Wawakilishi wa Vyama vya Wakulima wa Sukari kutoka Wilaya ya Kilombero. Baada ya uchambuzi wa kina Kamati ilipendekeza kwa Serikali nakuridhia kama inavyoonekana kwenye mabadiliko yafuatayo: -

(i) Kifungu cha 75 kinachofanya mabadiliko katika kifungu cha 4(2) aya ya (e) iliyokuwa inaanzisha tozo katika mabaki ya miwa;

(ii) Kufuta na kuandika upya Kifungu kipya cha 11(c) katika ibara ya 76 ya Muswada ili jukumu la kufuatilia gharama ya uzalishaji liwe la Bodi ya Sukari kuliko inavyopendekezwa ambapo jukumu hilo walipewa wenye viwanda; na

(iii) Kufuta Ibara 76 inayoongeza Kifungu cha 11(d) kinachoweka masharti ya kuwataka wazalishaji wote kutangaza wasambazaji wa bidhaa yao ya sukari mikoa yote nchini. Utaratibu huu unaenda kinyume na misingi ya biashara huru na kuongeza gharama kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, Ili kuhakikisha kwamba mabadiliko haya hayaathiri uzalishaji wa sukari kwa viwanda vya ndani, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

*(i)* Katika kipindi chote Serikali kuhakikisha kiasi cha sukari kinachoagizwa ni pengo kati ya uzalishaji na mahitaji si zaidi; *(Makofi)*

(ii) Kuhakikisha *NFRA* inajengewa uwezo wa kiutawala na kifedha kwa ajili ya kununua sukari na kujenga miundombinu ya kutunza na kusambaza sukari nchini;

(iii) Kuweka mazingira yanayolinda uzalishaji wa ndani ili kutetea ajira za wakulima na Watanzania walioko kwenye sekta ndogo ya sukari; na

(iv) Kuhakikisha Bodi ya Sukari inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Rufani za Kodi; Kamati imefanya uchambuzi katika mabadiliko yanayopendekezwa katika Sheria hii na kubaini kwamba yana malengo makuu matatu: -

(i) Kuwezesha Wajumbe wa Bodi ya Rufani na Mahakama ya Rufani ya Mkoa kuruhusiwa kusikiliza mashauri katika mkoa mwingine endapo hauna wajumbe wa kutosha;

(ii) Kubainisha sifa za Mwenyekiti wa Bodi na Mahakama ya Rufani; na

(iii) Kuweka ukomo wa siku ambazo shauri linaweza kushughulikiwa nje ya mahakama kwa hiari *(amicable settlement)*.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano Kamati ilitaka Serikali kufanya mabadiliko katika Ibara ya 90 inayofanya mabadiliko katika Kifungu cha 4(3) kwa kuongeza masharti kwamba Makamu Mwenyekiti awe na sifa sawa na Mwenyekiti. Aidha, Kamati iliitaka Serikali kuweka ukomo wa siku 90 na kuondoa ruhusa ya nyongeza ya siku 10 ili kupunguza muda wa kushughulikia mashauri nje ya Mahakama. Serikali ilikubali pendekezo hili na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41; Serikali inapendekeza kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 26 cha Sheria hii ili kubadilisha mfumo wa matumizi ya sarafu kwenye michezo ya kubahatisha na badala yake kutumia *token*. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uhai na muda wa matumizi wa sarafu. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Ibara ya 24 kwa kuongeza muda wa utekelezaji wa Sheria hiyo kutoka tarehe 1 Januari, 2025 hadi tarehe 1 Aprili, 2025 ili kutoa muda wa kutosha kwa wenye kampuni kufanya maandalizi. Serikali iliridhia ushauri wa Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ambazo Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali; Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu mabadiliko yaliyopendekekwa katika sheria 15 baada ya kujiridhisha na nia pamoja na maudhui yake. Sheria hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha Sura ya 342;
(ii) Sheria ya Benki Kuu Sura ya 197; na
(iii) Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Sura ya 407.

Mheshimiwa Spika, pia tulikubaliana na mabadiliko katika Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi Sura ya 82. Pia tulikubaliana na mabadiliko katika Sheria ya Bandari Sura 163. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabadiliko katika sheria hii yanakusudia kurejesha jukumu la kukusanya Tozo ya Miundombinu ya Bandari *(wharfage)* kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Makusanyo hayo yatawekwa katika Akaunti Maalumu ya *TPA* iliyopo Benki Kuu. Hatua hii ni kuiwezesha *TPA* kupata fedha kwa wakati kwa ajili ya maboresho ya miundombinu ya bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumekubaliana na mabadiliko ya Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari Sura 124 na Sheria ya Madini, Sura ya 123. Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa mabadiliko kwa malengo makuu mawili: moja, ni kuwezesha Benki kuu kununua dhahabu na kuitunza kama dhahabu fedha na pili ni kuwezesha viwanda vya ndani vya kuchakata, kuyeyusha na kusafisha dhahabu nchini kupata malighafi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tulikubaliana kuhusu Sheria ya Leseni ya Usajili wa Viwanda Nchini, Sura ya 46. Vilevile tulikubaliana kuhusu Sheria ya Ardhi Sura 113 ya Sheria za Serikali za Mitaa, Utozaji wa Kodi za Majengo Sura 239. Pia tulikubaliana kuhusu Sheria ya Uzalishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi Sura 193.

Mheshimiwa Spika, pia tulikubaliana kuhusu Sheria ya Reli Sura 170. Vilevile, tulikubaliana kuhusu Sheria ya Afya ya Mimea Sura ya 133; pia tulikubaliana kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria hii ambayo yana malengo yafuatayo: -

(i) Kutoa tafsiri ya maneno *'Tax Audit'* ili kuondoa mkanganyiko uliojitokeza wakati wa utekelezaji;

(ii) Kuweka utaratibu wa mapokezi ya nyaraka kwa Kamishana wa Mamlaka ya Mapato kwa kutambua namna nyingine ya uwasilishaji wa nyaraka;

(iii) Kuweka utaratibu wa kuwatambua Mameneja, Wakuu wa Vitengo vya Fedha au Uhasibu yeyote mwenye *CPA* kama watu wanaoweza kufanya marejesho ya kodi kwa mashirika, taasisi au kampuni ambazo Serikali inamiliki kwa 100%;

(iv) Kuondoa utata wa siku ipi inatakiwa kuanza kuhesabika kwamba Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania anapopokea pingamizi la kodi; na

(v) Kufanya mabadiliko ya *currency point* ili kiwango kilichopo kiendane na wakati na kulinda thamani ya fedha wa sasa kwa sababu kiwango kilichopo ni cha mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani nayo hiyo tulikubaliana nao (Serikali) na pia tulikuwa tumekubaliana kuwa kuaninisha *HS code* zote kutokana na mabadiliko ya Kitabu cha *HS Code* cha Jumuiya ya Afrika Mashariki *(The East Africa Tarriff Book)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yanayolenga kuongeza mapato pamoja kuchochea uzalishaji wa bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tulikubaliana na kuhusu Sheria ya Korosho Sura 2023. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye hii kwa lengo la kuelekeza mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi *(Cashew nuts Export Levy)* kwenye Bodi ya Korosho kwa 100% kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia Julai 2024 hadi Juni, 2029. Hatua hii itasaidia kuchochea maendeleo ya kilimo cha korosho kwa kutoa ruzuku ya pembejeo pamoja na kufanya tafiti za zao hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huu unaolenga kuimarisha zao la korosho na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni nchini. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba kuna nidhamu katika matumizi ya fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla ni pamoja na Serikali kufanya tathmini ya hatua za kikodi inazozichukua kila mwaka kwa kodi za ndani na Kodi ya Ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Serikali haina utaratibu wa kufanya tathmini ya matokeo ya hatua za kikodi zinazochukuliwa kila mwaka ili kuangalia endapo zina manufaa hasi au chanya kwa uchumi na uzalishaji viwandani. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kila mwaka kufanya tathmini ya kina ya athari hasi na chanya zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya mwaka uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kufanya mabadiliko ya ukusanyaji wa ada na tozo kwa kuwa na mifumo ya ukusanyaji. Serikali imekuwa ikifanya mabadiliko ya ukusanyaji wa tozo na ada mbalimbali bila kuandaa mfumo wa ukusanyaji. Hatua hii imekuwa na athari katika makusanyo kwa sababu kwa baadhi ya tozo zinachelewa kukusanywa hadi miezi saba baada ya mwaka wa fedha kuanza. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kabla ya kufanya mabadiliko yoyote kuandaa mifumo ya ukusanyaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wadau kwenye mabadiliko ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki. Kamati imebaini kwamba kuna ushirikishwaji hafifu wa wadau katika mabadiliko ya Sheria na hivyo wadau kushindwa kuwasilisha kwa wakati changamoto na maoni ya kikodi za Sheria hiyo. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuwashirikisha wadau mapema kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya Sheria hiyo katika Jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika, kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Hamad Chande, Naibu Waziri wa Fedha; Dkt. Natu Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Ndugu Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato; Ndugu Elijah Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati Bajeti kwa umakini na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu. Naomba majina yao yote yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivyokuwa kwenye taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho si kwa umuhimu, nimshukuru Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc,* Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli hii ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**27 JUNI, 2024**

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2024 (THE FINANCE BILL, 2024) – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 20 Juni, 2024 Muswada wa Sheria ya Fedha ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni na kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) uliuelekeza Muswada huo kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa ajili ya kuufanyia kazi na kutoa maoni yake Bungeni. Aidha, kama zilivyo Kanuni za Bunge, Muswada huo uliwasilishwa rasmi kwenye Kamati tarehe 21 Juni, 2024 na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande, (Mb) kwa niaba ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024, unakusudia kufanya marekebisho ya sheria ishirini tano (25) yenye lengo la kuboresha mifumo ya kodi, kuongeza mapato ya Serikali, kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, kulinda viwanda vya ndani, kuchochea uzalishaji wa sekta mbalimbali na kuimarisha usimamizi wa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegusa sekta mbalimbali hususan Viwanda, Madini, Kilimo, Mifugo, Uchukuzi, Fedha, Afya, Mazingira na Michezo. Kamati ilipitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujielimisha maudhui na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yalihitaji maboresho. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ilikutana na Wadau *(Public Hearing)* kuanzia tarehe 23 hadi 25 Juni, 2024 ili kupokea maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada huo.

**Mheshimiwa Spika,** wadau wafuatao walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa maoni. Naomba niwatambue Wadau hao kama

ifuatavyo: Tanzania Private Sector Foundation (TPSF), The Spirit Industry, Prance International Trade Co.Limited (Nice One), Urhome Company Limited (Good One), Geita Gold Refinery (GGR), Tanzania Human Rights Defenders Coalition (THRDC), M.M Integrated Steel Mills Limited (MMI Steel), Lodhia Industries, Tanzania Fishers Union (TAFU), Simba Cement, Dangote Cement, Tanzania Sugar Producers Association (TSPA), Wadau Binafsi, National Commercial Bank of Africa (NCBA), Confederation of Tanzania Industries (CTI), Mount Meru Millers, Tanzania Sports Betting Association (TSBA), Media Bay, Eliya Foods and Overseas Limited, Legal Human Rights Centre (LHRC), Tanzania Commercial Poultry Association, Umoja wa Shule Binafsi (TAMONGSCO), Waagizaji wa Undenatured Ethyl Alcohol Tanzania, Multi- Colour Corporation (MCC), Tanzania Milk Association (TMA), Tanzania Chambers of Mining, AIM Trailers Manufacturing Limited, Tanzania Chamber of Commerce (TCC), Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT), Tanzania Bankers Association (TBA) na Wadau wa Gesi Asilia. Pia Kamati ilipokea maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wa Tatu ambao ni Mhe. Joseph Kasheku Musukuma, Mhe. Jumanne Kishimba, Mhe. Prof. Patrick Ndakidemi na George Mwenisongole.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Kamati ilipokea maoni kwa njia ya maandishi na barua pepe kutoka kwa Jukwaa la Hedhi Salama Tanzania (Tanzania MHH Coalition), Watu Binafsi na Tanuk Africa LTD. Aidha, kwa mara ya kwanza Kamati ya Bajeti imepokea maoni kutoka Jumuiya ya Watanzania Waishio Nje (Diaspora). Kamati inaenzi mchango wa Diaspora katika kuhakikisha Taifa linapata maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupokea na kuchakata maoni ya wadau, iliandaa bangokititа lenye maoni ya Kamati kuhusu Muswada na kuliwasilisha kwa Serikali. Aidha, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 26 Juni, 2024, ili kufanya majumuisho kuhusu maoni ya Kamati. Mawaziri waliofika kwenye vikao hivyo ni Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mb Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb Waziri wa Kilimo, Mhe. Jumaa Aweso, Mb

Waziri wa Maji, Mhe. Angela Jasmine Kairuki, Mb Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Anthony Peter Mavunde, Mb Waziri wa Madini, Mhe. Dkt. Steven Kiruswa, Mb Naibu Waziri Madini walioambatana na Makatibu wa Kuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na Wataalam mbalimbali kutoka Serikali. Kamati inawashukuru kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada huu.

## 2.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2024

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha kwa muhtasari masuala yaliyojiri kwenye kikao cha mashauriano kati ya Kamati na Serikali.

### 2.1. Sheria ya Bajeti, Sura ya 439

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na mabadiliko yaliyopendekezwa katika Sheria hii yaliyokuwa na lengo la kuongeza vyanzo vya mapato ili kuwezesha Mfuko wa Dharura (Contigency Fund) kugharamia matengenezo ya dharura ya miundombinu ya barabara iliyoharibika kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, Kifungu cha 35(1) kinarekebishwa ili kujumuisha vyanzo vipya vya mapato katika mfuko huo ambavyo ni:-

a) Tozo ya maendeleo ya reli (Railway Development Levy);
b) Mapato yatokanayo na tofauti kati ya kushuka kwa bei ya mafuta (The windfall gains in fuel price decrease);
c) Asilimia moja ya matumizi ya Serikali kila mwezi; na
d) Vyanzo vingine vitakavyopangwa na Waziri mwenye dhamana ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati ilipendekeza kufutwa kwa aya (d) kwa hofu kwamba kingeweza kutumika vibaya. Serikali iliridhia mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

### 2.2. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yenye lengo la kuainisha vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote ili kugharamia matibabu ya Watu wasiokuwa na uwezo. Hata hivyo, Kamati haikukubaliana na pendekezo lililopo kwenye **Ibara ya 25(c)** ya chanzo kitokanacho na bima ya vyombo vya moto kwa sababu kimsingi bima ni kinga dhidi ya majanga ikiwemo afya hivyo si busara kutoza chanzo hicho. Vilevile, hatua hiyo inaweza kuongeza gharama za bima za vyombo vya moto. Baada ya mashauriano, Serikali iliridhia pendekezo la Kamati na kufuta **aya c** katika Ibara ya 73 ya Muswada na marekebisho ni kama yanavyonekana katika jedwali la marekebisho.

### 2.3. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu mapendekezo ya Serikali kwenye Sheria hii na ilikuwa na maoni yafuatayo;

#### 2.3.1. Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye ada ya matangazo ya biashara ya michezo ya kubahatisha

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha **asilimia 10** kwenye ada ya matangazo ya biashara ya michezo ya kubahatisha. Kwa maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa kwenye Kamati ushuru huu hautahusisha matangazo ya kuuza biashara (Promotion) majaribio na bahati Nasibu ya Taifa. Mapato yatakayotokana na tozo hiyo zitaelekezwa katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Kamati inaiona ni jambo jema ambalo linaenda kufanikisha azma ya Serikali ya watu wote nchini hasa wale wasio na uwezo kuweza kupata huduma za kiafya bure.

#### 2.3.2. Ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia kumi kwenye thamani ya dau la kamari katika michezo ya kubahatisha na bahati nasibu ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha **asilimia 10** kwenye thamani ya dau la kamari. Hatua hii itasababisha wachezaji wa kamari walioko nchini

kushawishika kucheza katika kampuni za nje ambazo hazijasajiliwa nchini na hivyo Serikali kupoteza mapato yatokanyo na michezo ya kubahatisha pamoja na bahati nasibu ya Taifa. Ukizingatia hadi hivi sasa hatuna Bahati Nasibu ya Taifa, hivyo ni dhahiri kwamba uamuzi huu hautaleta manufaa yanayokusudiwa. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufuta kifungu kipya cha **6B** katika **Ibara ya 14** ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza. Baada ya mashauriano, Serikali iliridhia ushauri wa Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

**2.3.3.Msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye Ethani inayotambulika kwa HS Code 2207**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye ethani inayotambulika kwa HS Code 2207 kwa mtu atakayezalisha na kutumia katika uzalishaji wa nishati ya viwandani, matumizi ya kitabibu au maabara. Vilevile, kwa watumiaji wa matumizi mengine tofauti na matumizi tajwa wataendelea kutozwa ushuru wa bidhaa. Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba mapendekezo ya Serikali hayajabainisha ni kwa namna gani waagizaji na wazalishaji watakapokuwa wanauza ethani kwa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kama vile pombe kali watarejeshewa vipi kodi waliyokwishalipa wakati wa uingizaji au uzalishaji wa ethani.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondoa changamoto ya mlundikano wa marejesho, Kamati ilipendekeza kwamba ushuru wa bidhaa kwenye ethani inayotambulika kwa HS Code 2207 ulipwe pindi mzalishaji wa ndani au mfanyabiashara anayeingiza ethani kutoka nje anapomuuzia mzalishaji anaetumia ethani kuzalisha bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

**2.3.4.Ushuru wa bidhaa kwenye ethani yenye kilevi zaidi ya asilimia 80 itakayozalishwa ndani ya nchi na itakayoagizwa kutoka nje kwa kiwango cha shilingi 5,000 na shilingi 7,000 kwa lita mtawalia**

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 18 aya ya (f) Serikali inapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwenye ethani yenye kilevi zaidi ya asilimia

80 itakayozalishwa ndani ya nchi kwa shilingi 5,000 na itakayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa kiwango cha shilingi 7,000 kwa lita. Ushuru unaopendekezwa kwa malighafi hii ni mkubwa kuliko bidhaa za pombe zinazozalishwa na ethani ambazo zinazotozwa ushuru wa shilingi 2300 hadi 2600 kwa lita. Hivyo, Kamati inapendekeza kufuta maneno Tsh. 5,000 na Tsh. 7,000 yaliyoko katika jedwali *column* ya sita na kuweka maneno Tsh. 2,500 na Tsh. 3,500. Hatua hii itapunguza ushuru wa Serikali kutoka shilingi 5000 inayopendekezwa hadi shilingi 2,500. Aidha, itapunguza shilingi 7,000 inayopendekezwa kwa bidhaa za nje hadi shilingi 3,500.

### 2.4. Sheria ya Kudhibiti Uingizwaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276

**Mheshimiwa Spika,** katika Sheria hii Serikali inakusudia kuanzisha Tozo ya Maendeleo ya Viwanda *(Industrial Development Levy)* kwa baadhi ya bidhaa zinazoingizwa nchini. Hatua hii ni ya kupongeza kwa sababu ni mbinu ya ziada ya kuvilinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani usio sawa wa bidhaa zinazotoka nje na kuchochea mauzo nje ya nchi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali fedha zitakazotokana na tozo hiyo zisaidie vilevile kuendeleza sekta ya viwanda nchini hasa vile viwanda vidogo na vya kati. Aidha, Kamati iliishauri Serikali kuongeza wigo wa bidhaa zinazotozwa kodi hii kwa akuangalia hasa zile bidhaa zinazozalishwa nchini kwa wingi. Kamati ilipendekeza bidhaa za *clinker* ziongezwe kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 2.5. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii inafanyiwa marekebisho mbalimbali ambayo ni:-

i. Kuongeza tafsiri ya maneno, "mali za kidigitali" "mchimbaji asiye na leseni" "maudhui ya kidigitali" na "mtengeneza maudhui ya kidigitali". Hii ni kutokana na kuwa maudhui ya kidigitali sasa kwenda kutozwa kodi ya zuio ya **asilimia 3 na 5** na hivyo kutanua wigo wa kodi na kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi. Hivyo, Serikali iliona ni vema kuweka tafsiri ya misamiati husika ambayo awali haikuwepo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutanua wigo wa kodi ili iweze kukusanya zaidi

kwa kufikiria uanzishwa wa kodi mpya na kutoza katika maeneo yanayoibukia.

ii. Kuondoa takwa la kulipa kodi ya mapato mbadala kwa kampuni zinazochakata mazao ya chai yanayotengeneza hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo inaenda kunusuru sekta ya chai nchini ambayo kwa sasa inakabiliana na changamoto ya kushuka kwa bei ya zao la chai kwenye soko na hivyo wazalisahaji kupata hasara.

iii. Kujumuisha Taasisi zinazofanya shughuli za uboreshaji wa huduma za afya (advancement of health) na utunzaji wa mazingira kwenye wigo wa Taasisi zinazotoa huduma za hisani (Charitable Organisations) ili ziweze kupata nafuu ya ukokotoaji wa Kodi ya Mapato kulingana na matakwa ya Sheria. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo itachochea na kuvutia huduma za hisani kwenye maeneo husika. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kuongeza pia huduma zenye sura za taasisi hisani kama vile huduma za kisheria ili kuongeza upatikanaji wa huduma hizo kwa wingi ukizingatia kuwa kwa asilimia kubwa huwa zinatolewa bure.

iv. Kuruhusu michango ya **asilimia 15** inayolipwa na Taasisi za Serikali kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kuwa miongoni mwa sehemu ya gharama za Taasisi kwenye ukokotoaji wa kodi ya mapato (deductible expenditure). Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho hayo ambayo imekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa taasisi na mashirika ya Serikali ambapo ilikuwa inaonekana kama zinatozwa kodi mara mbili. Kupitia marekebisho haya, sasa mashirika na taasisi husika zinaenda kubakiwa na mapato mengi ikilinganishwa na hapo awali.

v. Kutoa msamaha wa kodi ya zuio kwenye malipo ya riba kwa taasisi ya fedha mkaazi inapolipa Taasisi au Mfuko uliopo nje ya nchi. Ili Taasisi iliyopo nchini iweze kupata msamaha huo ni

lazima iwe imetoa mikopo nchini kwa riba ya chini. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Seriali ambayo yana nia njema ya kuvutia mitaji kwenye sekta ya kibenki nchini hata hivyo, iliitaka Serikali kutoa tafsiri ya maneno *"low interest rate"* na Serikali ilipokea ushauri huo. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho lililowasilishwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kuondoa mapendekezo yafuatayo katika Muswada:-

i. **Ibara ya 37** inayopendekeza kifungu kipya cha **83 D**, kinachokusudia kuanzisha Kodi ya Zuio ya **asilimia 2** kwenye malipo yatakayofanywa na wafanyabiashara wa kati (Middlemen) kutokana na ununuzi wa bidhaa za kilimo, ufugaji, uvuvi na misitu. Kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza mwaka 2021/22 wakati pendekezo hilo lilipoanzishwa kwa mara ya kwanza, Kamati ilishauri Serikali kufuta kifungu hiki na Serikali iliridhia. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

ii. Ibara ya 38 ya Muswada inayopendekeza kufanya mabadiliko katika kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya zuio ya **asilimia 2** kwenye malipo wanaolipwa watu binafsi kama vile wapagazi, wapishi, waongoza watalii na huduma ya kubeba mizigo kwa Watalii. Kamati iliona ni busara pendekezo hilo likaondolewa ukizingatia kuwa bado sekta hii inaimarika kufuatia janga la Uviko-19. Kamati ilishauri Serikali kufuta kifungu hiki na Serikali iliridhia. Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali.

**2.6. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura ya 220**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuelekeza mapato ya ziada (windfall profit) kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Barabara. Hata hivyo, Kamati haikukubaliana na uanzishwaji wa ushuru **shilingi 382** kwa kila kilo ya gesi asilia

inayotumika kwenye magari. Kamati imefikia uamuzi huu kwa kuzingatia kuwa sekta ya gesi bado ni changa na inaendelea kukua taratibu na hadi sasa haijaweza kutumika kikamilifu nchini kutokana na gharama za kufunga mfumo wa kutumia gesi pamoja na uhaba wa vituo vya kujazia gesi. Hivyo, Kamati iliishauri Serikali kuondoa pendekezo hili na Serikali iliridhia. Marekebisho ni kama yanavyonekana katika jedwali la marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuondoa kodi kwenye vifaa vinavyotumika kuunganisha mfumo wa gesi ili kupunguza gharama za kusimika mfumo huu kwenye magari ambazo kwa sasa gharama za ufungaji zinakadiriwa kuwa kati ya **shilingi Milioni 2 hadi 3,** kiwango ambacho ni kikubwa.

### 2.7. Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251;

**Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kufanya maamuzi katika mapendekezo ya Serikali kuhusu Sheria hii Kamati ilikutana na Bodi ya Sukari, Wazalishaji wa Sukari pamoja na wawakilishi wa vyama vya wakulima wa Sukari kutoka Wilaya ya Kilombero. Baada ya uchambuzi wa kina kamati ilipendekeza kwa Serikali na Serikali iliridhia kufanya mabadiliko yafuatayo: -

i. Kufuta ibara ya 75 inayofanya mabadiliko katika kifungu cha 4(2) aya ya (e) iliyokuwa inaanzisha tozo katika mabaki ya miwa;

ii. Kufuta na kuandika upya kifungu kipya cha 11C katika ibara ya 76 ya muswada ili jukumu la kufuatilia gharama ya uzalishaji liwe la bodi ya sukari kuliko inavyopendekezwa ambapo jukumu hilo walipewa wenye viwanda; na

iii. Kufuta ibara 76 inayoongeza kifungu 11D kinachoweka masharti ya kuwataka wazalishaji wote kutangaza wasambazaji wa bidhaa yao ya sukari mikoa yote nchini. Utaratibu huu unaenda kinyume na misingi ya Biashara huru na kuongeza gharama kwa wazalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha kwamba mabadiliko haya hayaathiri uzalishaji wa sukari kwa viwanda vya ndani, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

i. Katika kipindi chote Serikali kuhakikisha kiasi cha sukari kinachoagizwa ni pengo kati ya uzalishaji na mahitaji na si zaidi;

ii. Kuhakikisha NFRA inajengewa uwezo wa kiutawala na kifedha kwa ajili ya kununua sukari na kujenga miundombinu ya kutunza na kusambaza sukari nchini;

iii. Kuweka mazingira yanayolinda uzalishaji wa ndani ili kutetea ajira za wakulima na Watanzania walioko kwenye sekta ndogo ya sukari; na

iv. Kuhakikisha Bodi ya Sukari inatekeleza majukumu yake kwa Ufanisi kuliko ilivyo hivi sasa.

**2.8. Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi katika mabadiliko yanayopendekezwa katika Sheria hii na kubaini kwamba yana malengo makuu matatu: -

i. Moja, ni kuwezesha wajumbe wa Bodi ya Rufani na Mahakama ya Rufani ya Mkoa mmoja kuruhusiwa kusikiliza mashauri katika mkoa mwingine endapo hauna wajumbe wa kutosha;

ii. Pili, ni kubainisha sifa za mwenyekiti wa Bodi na Mahakama ya Rufani; na

iii. Tatu, ni kuweka ukomo wa siku ambazo shauri linaweza kushughulikiwa nje ya mahakama kwa hiari "*amicable settlement*".

**Mheshimiwa Spika,** baada ya majadiliano Kamati ilitaka Serikali kufanya mabadiliko katika **Ibara ya 90** inayofanya mabadiliko katika **kifungu cha 4(3)** kwa kuongeza masharti kwamba Makamu mwenyekiti awe na sifa sawa na Mwenyekiti. Aidha, Kamati iliitaka

Serikali kuweka ukomo wa **siku 90** na kuondoa ruhusa ya nyongeza ya **siku 10** ili kupunguza muda wa kushughulikia mashauri nje ya mahakama. Serikali ilikubali pendekezo hili na marekebisho ni kama yanavyonekana katika jedwali la marekebisho.

### 2.9. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya mabadiliko katika kifungu cha 26 cha Sheria hii ili kubadilisha mfumo wa matumizi ya sarafu  kwenye michezo ya kubahatisha na badala yake kutumia tokeni. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uhai na muda wa matumizi wa sarafu. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko katika **Ibara ya 24** kwa kuongeza muda wa utekelezaji wa Sheria hiyo kutoka tarehe 1 Januari, 2025 hadi tarehe 1 Aprili, 2025 ili kutoa muda wa kutosha kwa wenye makampuni kufanya maandalizi. Serikali iliridhia ushauri wa Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

## 3.0. SHERIA AMBAZO KAMATI IMEKUBALIANA NA MAPENDEKEZO YA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na Serikali kuhusu mabadiliko yaliyopendekekwa katika sheria 15 Baada ya kujiridhisha na nia pamoja na maudhui yake. Sheria hizo ni kama ifuatavyo:-

### 3.1. Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha Sura ya 342, Sheria ya Benki Kuu Sura ya 197 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Sura ya 407.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na mabadiliko yaliyopendekezwa katika Sheria hizo yenye lengo la kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za fedha kwa kuziwezesha benki, taasisi za kifedha na kampuni zinazojihusisha na utoaji wa huduma ndogo za fedha zisizotoza riba kuweza kutoa huduma za mikopo pasipo kutoza riba. Vilevile, mabadiliko hayo yana lenga kutambua huduma nyingine za kifedha ambazo zilikuwa hazitambuliki kwa sheria zilizopo hivi sasa  na kuruhusu benki zisizo toza riba kufanya biashara kwa kutumia akaunti zao au akaunti za wateja kwenye hati zinazotumika kuzalisha.

### 3.2. Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, Sura ya 82

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko katika Sheria hii yanakusudia kutoa msamaha wa kodi ya kuendeleza Ufundi Stadi kwa vibarua wanaotekeleza miradi ya Maji. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji nchini.

### 3.3. Sheria ya Bandari, Sura ya 166

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko katika sheria hii yanakusudia kurejesha jukumu la kukusanya Tozo ya miundombinu ya bandari (wharfage) kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA). Makusanyo hayo yatawekwa katika Akaunti Maalumu ya TPA iliyopo Benki Kuu, na matumizi yataidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha TPA kupata fedha kwa wakati kwa ajili ya maboresho ya miundombinu ya Bandari**.**

### 3.4. Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii inafanyiwa mabadiliko ili kutambua magari, pikipiki na vyombo vingine vya moto vinavyotumia umeme kwa lengo la kuvijumuisha katika wigo wa ulipaji wa ada ya usajili wa magari kwa kuzingatia kanuni za usawa za utozaji wa kodi na kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

### 3.5. Sheria ya Madini, Sura ya 123

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii inapendekezwa kufanyiwa mabadiliko kwa malengo makuu mawili moja ni kuwezesha Benki kuu kununua dhahabu na kuitunza kama dhahabu fedha na pili ni kuwezesha viwanda vya ndani vya kuchakata, kuyeyusha, na kusafisha dhahabu nchini kupata malighafi hiyo.

### 3.6. Sheria ya Leseni na Usajili wa Viwanda Nchini, Sura ya 46

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko yanayopendekezwa ni kuweka sharti kwa wamiliki wa viwanda vilivyopewa misamaha ya kodi chini ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania pamoja na Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki, kuingia mikataba ya kiutendaji na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha. Lengo la mabadiliko haya ni kuhahakisha kwamba wawekezaji au wamiliki wa viwanda

wanafikia malengo yaliyokusudiwa wakati wanapewa misamaha hiyo.

### 3.7. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria ya Serikali za Mitaa ya Utozaji wa Kodi ya Majengo, Sura ya 289

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko yanayopendekezwa katika sheria hizi yana lengo la kubainisha mgawanyo wa mapato yatokanayo na Kodi ya majengo na Kodi ya Ardhi. Utaratibu unaopendekezwa ni **asilimia 20** ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye vyanzo hivyo kubaki serikali za mitaa na **asilimia 80** kupelekwa Mfuko Mkuu. Awali kiasi chote kilipelekwa Mfuko Mkuu na Serikali za mitaa kurejeshewa **asilimia 20**. Hatua hii itasaidia Halmashauri za Serikali za Mitaa kupata mgao wake kwa wakati kuliko ilivyo hivi sasa.

### 3.8. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kuweka tozo ya **asilimia 10** kwenye mafuta ghafi ya kula ya alizeti na mashudu yanayotokana na mbegu za alizeti pamoja na mbegu za alizeti zinazosafirishwa kwenda nje ya Jamhuri ya Muungano. Lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha malighafi hizo zinapatikana kwa wingi nchini ili kuzalisha mafuta ya kula, kuondoa changamoto ya uhaba wa mafuta pamoja na chakula cha wanyama.

### 3.9. Sheria ya Reli, Sura 170

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza kiwango cha tozo ya maendeleo ya reli kutoka **asilimia 1.5 hadi asilimia 2.** Mapendekezo haya yanakusaidia kuongeza mapato ya Serikali ili kurekebisha miundombinu ya barabara zilizoathiriwa na mvua za El-Nino. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na ongezeko la tozo hiyo kwenye bidhaa muhimu.

### 3.10. Sheria ya Afya ya Mimea, Sura ya 133

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yanayoenda kuipatia Mamlaka ya Mapato Tanzania mamlaka ya kukusanya tozo ya kusafirisha mazao nje ya nchi na tozo za kuingiza mazao nchini. Vilevile, marekebisho hayo

yanaenda kuanisha mgawanyo wa tozo hiyo ambapo **asilimia 70** ya tozo itapelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo na **asilimia 30** itapelekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Marekebisho hayo yanalenga kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo na kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya majukumu mbalimbali ya Serikali. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo inaenda kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

### 3.11. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusu mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria hii ambayo yana malengo yafuatayo: -

(i) Kutoa tafsiri ya maneno *"Tax Audit"* ili kuondoa mkanganyiko uliojitokeza wakati wa Utekelezaji;

(ii) Kuweka utaratibu wa mapokezi ya nyaraka kwa Kamishana wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kutambua namna nyingine ya uwasilishaji wa nyaraka;

(iii) Kuweka utaratibu kuwatambua Mameneja, Wakuu wa Vitengo vya Fedha au Muhasibu yeyote mwenye CPA kama watu wanaoweza kufanya marejesho ya kodi kwa Mashirika, Taasisi au Kampuni za umma ambazo Serikali inamiliki kwa **asilimia 100**;

(iv) Kuondoa utata wa ni siku ipi inatakiwa kuanza kuhesabika kwamba Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania amepokea Pingamizi la Kodi; na

(v) Kufanya mabadiliko ya "*Currency Point*" ili kiwango kilichopo kiendane na wakati na kulinda thamani ya fedha wa sasa kwa sababu kiwango kilichopo ni cha mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mabadiliko haya kuwa na nia njema Kamati inaitaka Mamlaka ya Mapato kuhakikisha kwamba watumishi wake katika wakati wote wanazingatia maadili wakati wa utendaji kazi wao.

**3.12. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kuhusu mapendekezo ya Serikali kuhusu sheria hii na kubaini ina malengo yafuatayo:-

i. Kuongeza tafsiri ya maneno mbalimbali ili kuondoa mkanganyiko katika wa matumizi;

ii. Kuendeleza kutoza kwa kiwango cha **asilimia 0** bidhaa za nguo, mafuta ya kula na Mbolea zinazozalishwa ndani;

iii. Kutoa msamaha kwa madawa yanayotumika kusafisha maji;

iv. Kuanzisha utaratibu wa kutoza kwa kiwango cha **asilimia 0** dhahabu inayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania pamoja na viwanda vya kusafisha dhahabu vya ndani ili kuhakikisha serikali inapata dhahabu na kuitunza kama dhahabu fedha; na

v. Kuwianisha HS Code kutokana na mabadiliko ya kitabu cha HS Code cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (The East Africa Tarriff Book).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Kamati yanayolenga kuongeza mapato pamoja kuchochea uzalishaji wa bidhaa.

**3.13. Sheria ya Korosho Sura ya 203**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye hii, kwa lengo la kuelekeza mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi (Cashewnuts Export Levy)

kwenye Bodi ya Korosho kwa asilimia 100 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia Tarehe 1 Julai 2024 hadi Tarehe 30 Juni, 2029. Hatua hii itasaidia kuchochea maendeleo ya kilimo cha korosho kwa kutoa ruzuku ya pembejeo  pamoja na kufanya tafiti za zao hilo. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huu unaolenga kuimarisha zao la Korosho na hivyo kuongeza mapato ya fedha za kigeni nchini. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba kuna nidhamu katika matumizi ya fedha hizo.

## 4.0. MAONI YA UJUMLA

**4.1.** Serikali kufanya Tathmini ya Hatua za Kikodi inazozichukua kila mwaka kwa kodi za ndani na Kodi ya Ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Serikali haina utaratibu wa kufanya tathmini ya matokeo ya hatua za kikodi zinazochukuliwa kila mwaka ili kuangalia endapo zina manufaa hasi au chanya kwa uchumi na uzalishaji viwandani. Hivyo,Kamati inaitaka Serikali kila mwaka kufanya Tathmini ya kina ya athari hasi na chanya zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya mwaka uliopita.

### 4.2. Kufanya Mabadiliko ya ukusanyaji wa Ada na Tozo mbalimbali bila kuwa na mifumo ya ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikifanya mabadiliko ya ukusanyaji wa tozo na ada mbalimbali bila kuandaa mifumo ya ukusanyaji. Hatua hii imekuwa na athari katika makusanyo kwa sababu kwa baadhi ya tozo zinachelewa kukusanywa hadi miezi 7 baada ya mwaka wa fedha kuanza. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kabla ya kufanya mabadiliko yoyote kuandaa mifumo ya ukusanyaji kwanza.

### 4.3. Ushirikishwaji wa Wadau kwenye Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kuna ushirikishwaji hafifu wa wadau katika mabadiliko ya Sheria hiyo na hivyo wadau

kushindwa kuwasilisha kwa wakati changamoto na maoni ya kikodi za Sheria hiyo. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuwashirikisha wadau mapema kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya Sheria hiyo katika Jumuiya.

## 5.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Akson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) pamoja na Mhe. Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge. Aidha, napenda kuwashukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Mb na Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande, Mb, Naibu Waziri wa Fedha, Dkt. Natu Mwamba Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Ndg. Alphayo Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ndg. Elijah Mwandumbya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu. Kamati pia inawashukuru wadau wote kwa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa umakini na ushirikiano wao katika kuchambua Muswada huu na kuweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua Wajumbe yao kama ifuatavyo wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb :-

1. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb — Mwenyekiti
2. Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb — Mjumbe
4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb — Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb — Mjumbe
6. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb — Mjumbe
7. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb — Mjumbe
8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb — Mjumbe
9. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb — Mjumbe
10. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb — Mjumbe

11. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb — Mjumbe
12. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb — Mjumbe
13. Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb — Mjumbe
14. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb — Mjumbe
15. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb — Mjumbe
16. Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb — Mjumbe
17. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb — Mjumbe
18. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb — Mjumbe
19. Mhe. Omar Ali Omar, Mb — Mjumbe
20. Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb — Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** mwisho si kwa umuhimu, nimshukuru Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
**27 Juni, 2024**

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa uwasilishaji huo, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge ninayo hapa majina ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kuhusu Muswada huu wa Fedha. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na nikawa wa kwanza kuchangia kwenye

Muswada huu ambao umepita kwenye Kamati ambayo mimi ni mmoja wa Wajumbe.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninakupongeza kwa namna unavyotuongoza kwenye hivi vikao vyetu, pia naishukuru Serikali ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa sikivu na ninashukuru sana kwa ushauri unaotolewa na Wizara hii ya Fedha ambao inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Chande pamoja na uongozi mzima wa Wizara kwa kuwa wasikivu. Naamini kwamba wanatoa ushauri mzuri kwa Mheshimiwa Rais na pia wamekuwa watu wanaoweza kuwasilisha hoja inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, pengine huu muswada unakuja umechelewa kidogo. Siku tano, sita au saba za kujadili muswada mzito kama hivi na ambao una wadau wengi wanaotaka kuchangia ili kuona kwamba nchi yetu inakuwa na *fiscal policy* ambayo ni nzuri na ambayo inajenga mazingira sahihi ya kuongeza tija na kuongeza pato letu la Taifa, nafikiri ungekuja mapema kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hamna siri kubwa hapa kwa sababu vitu vingi unakuta kwamba kwenye nchi jirani, ambao wako kwenye jumuiya yetu wanakuwa tayari wameshatoa miswada hii na inajulikana kwamba ni vitu gani vinakuja, lakini hapa kwetu miswada inakuja *late* kidogo na ile Kamati inakuwa haipati nafasi ya kutosha kusema kweli ya kuchakata na kusikiliza wadau wote ambao wangetaka kutoa mawaidha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, niseme hivi, nia ya muswada huu kusema kweli mimi naamini ni kuweka mazingira ya kukusanya fedha ambazo itaweza kutosheleza ongezeko kwenye bajeti yetu ili kuziba ile nakisi ili nakisi ile isiende kwenye kutafuta mikopo zaidi na tuifute kupitia njia zetu za kawaida za kodi na njia ambazo siyo za kodi.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, kwa mantiki kwamba tumeshapitisha *Appropriation Bill* jana, ile sheria ya jana tuliyoipitisha, mimi nafikiri ina maana kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote wataungana na sisi kuunga mkono Serikali ili waweze kwenda kutumia muda uliobaki kuanza sasa kutengeneza mazingira ya kutekeleza haya mambo ambayo wameonesha hapa.

Mheshimiwa Spika, pia, nisichelee kusema kwamba, ukisoma huu muswada utakuta kwamba bado ile nadharia ya *tax calendar* haijawa *consistent*. Ni kweli kuna maeneo ambapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha hajagusa na amezingatia kwamba kuna *calendar* Fulani ya miaka miwili, mitatu asiguse lakini inaonekana bado kuna maeneo kama Kifungu 97, 98, 99 cha *Value added Tax* wameweka muda wa mwaka mmoja tu, kwamba, wametoa msamaha au wame-*extent rate* ya *VAT* lakini kwa kipindi cha mwaka mmoja, haitoshelezi. Ni vizuri kuwa na miaka miwili au mitatu ili wawekezaji waweze kuwa na mwelekeo wa kuona kwamba wanaweza waka-*predict* ni kitu gani kinakwenda kutokea katika maeneo ya *VAT* na kwenye *exercise duty* na kadharika, kwa hiyo naomba hiyo nadharia iendelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa ujumla utaona kwamba huu muswada ni mzuri kwa mambo matatu au manne. Kwanza, utaona kwamba kodi hizi zilizoguswa zinalenga kulinda viwanda vya ndani. Nafikiri hiyo ni nadharia nzuri na uki-*go through* utakuta kwamba kuna nia hiyo ya kufanya vile. Pili ni kupunguza hamasa za jamii kutumia bidhaa ambazo zinaumiza au zinakuwa kama kilevi kama hii michezo ya kamari, wamejaribu kuzingatia hilo na ni kitu kizuri na ndiyo *essence* ya kuwa na *exercise duty*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kuna kupanua wigo wa walipakodi. Bahati mbaya hiyo haijaelezwa vizuri sana lakini ukiangalia utaona kwamba wanajaribu kushika na wengine. Kama kule kwangu walikuwa wametaka kushika wale wanaopandisha watu Mlima Kilimanjaro, waanze kulipa *withholding tax*, bahati nzuri Kamati ikasema hapana, hao bado hawafikii hata *minimum wage*. Ukichukua mapato yao ukagawanya kwa miezi 12 haifiki *minimum*

*wage* kwa hiyo utakuwa umewaonea na bahati nzuri Serikali imesikiliza, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba hiyo ya kuwezesha Benki Kuu kununua dhahabu ni jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge hawa wamekuwa wanalisemea kila mara na ninaamini kwamba hili nalo ni jambo zuri. Duniani kote sasa hivi nchi nyingi zinakazana kujenga hifadhi au *reserve* ya *gold* kwa sababu hizi sarafu nyingine kama dola au nini, watu wanaanza kuzitilia mashaka kwa sababu hatujui itakuja ya *Brex*, itakwenda ya China au itakwenda wapi, kwa hiyo watu wanaona ili kujikinga na huu mtikisiko unaoweza kutokea endapo dola itapoteza nguvu yake ya kuwa ni *world reserve currency*, basi itaweza kuleta matatizo kama unayo *reserve* kwenye *currencies* nyingine. Kwa hiyo *gold* ni kitu kizuri hata kama inakuwa ni ngumu kununua lakini tuinunue, natumaini Serikali imeweka njia ya kupata *gold* ya kutosha. Benki Kuu inataka kununua kila mwaka tani sita, sasa tani sita hazipatikani kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwa ujumla kwamba, mimi naamini mapato ya Serikali hii yanaweza yakaongezeka sana sana lakini jawabu lake ni mfumo. Mifumo hii tunayoijenga ya ukusanyaji kodi na mifumo ya kufuatilia mizigo inayoingia nchini mpaka kwenye ma-*godown* tunayoijenga, ni mifumo ambayo itatuwezesha hata hauna haja ya kuongeza sana kodi au kugusa kodi kila wakati. Nafikiri tukijenga mifumo hii vizuri, tutafikia mahali ambapo Mheshimiwa Mwigulu atakuja na *balance budget*.

Mheshimiwa Spika, *balance budget* maana yake ni kwamba, hatagusa chochote kwenye kodi. Atasema tunabakia na kodi hizi hizi tutakusanya vizuri kwa hiyo tunaendelea na mfumo kama ulivyokuwa katika mwaka uliopita. Kitakachojitokeza tu ni kwamba, kwa sababu vile vyanzo vinakua basi na ukuaji wa mapato ya serikali utakua kulingana na bajeti itakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, niseme hivi, kuna mambo kama matatu mimi nafikiri niyaseme ambayo ni muhimu sana. Hii ya kukubali hatimaye kuunda *contingency fund*, mfuko wa dharura, kitu hiki kiko

kwenye Katiba na tumekuwa tunaizungumza. Kuna wakati mimi nilisema kwamba sasa utakuwa na akiba ya dharura wakati unaenda kuomba msaada, *it does not make a lot of sense,* lakini sasa hivi tumeona umuhimu na ninashukuru kwamba Serikali imekubali, inaanzisha na imeweka vyanzo ambavyo ni bayana na vizuri. Hata ukiweka hiyo *one percent* ya *consolidated fund, one percent* tu ukiweka ni *four hundred ninety-four ninety-five billion*, ni fedha ambayo ukiiweka kwa namna fulani italeta mantiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka kushauri kwamba, sasa siyo tu kuanzisha, tutengeneze kanuni na dira ya mfuko huu kwamba itakuwaje. Kwamba, tutakusanya kiasi gani na tukifika mahali fulani tuseme sasa imetosha tusitenge zaidi tuwe tunasubiri na yenyewe inakuja kwa kuwekeza vizuri huu mfuko kwa sababu inaweza ikawekezwa kwenye, ikawa ina riba au *whatever* lakini *overtime* utakuwa ni mfuko mkubwa ambao unaweza ukahimili vitu vingi. Pia, baadaye unasitisha kuweka kwa sababu utakuwa ni mkubwa na unaweza ukajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizo kanuni zitengenezwe ili tujue utatumika kwenye mazingira gani, siyo kwamba utatumika kwenye mazingira ya El Nino, *no!* mazingira ya dharura ni mengi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa, muda umeisha.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Jesca, kabla hujaanza kuchangia, Waheshimiwa Wabunge kuna wageni ambao wameingia hapa ndani na wengine wanasubiri kuingia kwa hiyo tuwatangaze ili waweze kwenda kuendelea na mambo mengine.

YupoMgeni wa Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 17 wa Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa na Sekretarieti ya Wilaya ya Bunda, wakiongozwa na Katibu wa Chama cha Mapinduzi Ndugu Michael Chonya, Mwenezi wa Wilaya Ndugu Gaspar Charles na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Michael Kwela. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, ambao ni Wachezaji wa Timu ya mpira wa kikapu kutoka Mkoa wa Tabora. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 160 Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, ambao ni Wapigakura wake kutoka Ulanga Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni Mwalimu wa Shule ya Msingi Msandaka iliyopo Moshi Mkoa wa Kilimanjaro Ndugu Perpetua Michael Mmari. *(Makofi)*

Wanafunzi 95 na Walimu 4 wa Shule ya Sekondari Buigiri kutoka Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa ajili ya kufanya mabadiliko na kuondoa kile kifungu ambacho kilikuwa kimeweka faini ya kutotoa risiti mpaka milioni 15 na kuacha milioni nne, tunawapongeza sana kwa usikivu nafikiri ingetuletea kero ingawa bado kutakuwa na changamoto hasa kwa wale ambao watakuwa wana faini ambazo walitakiwa kulipa zikiwa ndogo chini ya hii milioni

nne, lazima kuwe na utashi ambao wale watu wetu wa *TRA* wataona namna. Mtu labda hakutoa risiti ya kitu labda cha shilingi 10,000 lakini tu kwa sababu hakutoa risiti anadaiwa milioni nne na mtu mwingine ambaye hakutoa risiti ya milioni 60 na yeye anadaiwa milioni nne. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba hapa utashi ili kuondoa migogoro isiyokuwa na sababu kwenye *industry* ya walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine pia tumekuwa tukitoa mapendekezo mengi sana kuhusiana na changamoto tunayopata kule kwenye *site* kuhusiana na hii *service levy especially* kwa wale watoa huduma kama wenye shule na wenye vituo vya afya, kidogo imekuwa ina changamoto kubwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba uone namna ambavyo utawasiliana na mamlaka ingawa hapa kwenye *amendment* haipo ya hizi Sheria za Serikali za Mitaa na wenzio kuona namna ambavyo mtatusaidia ili kuwe na utulivu *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye suala la bima ya afya. Muswada wa Sheria Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwenye marekebisho na mapendekezo yake Ibara ya 72, 73 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Sura Namba 82 kwa kurekebisha Kifungu Namba 25. Anaelezea kwamba nia ni kuona namna ambavyo tunaweza kuchangia Mfuko huo wa Bima ya Afya ambao utakwenda kugharamia matibabu ya wanawake, wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano. Kipengele kidogo cha pili anasema, kuanisha kiwango cha ushuru wa bidhaa za asilimia mbili kitakachotokana na vinywaji laini, vileo na vipodozi ili kupeleka katika Mfuko huo wa Bima ya Afya kwa Wote kwa ajili ya kugharamia matibabu ya watu wasiojiweza wakiwemo wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, mimi *interest* yangu kubwa iko hapa, tumesema tunakwenda kuleta bima ya afya kwa wote na tukiangalia katika *data* zetu za sensa, tulisomewa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, asilimia 76 ni watu chini ya umri wa

miaka 35 ambao inakwenda mpaka kwa watoto wadogo. Inaonesha kwamba tuna watoto wengi nchini na wengi wa watu hao ni ambao hawana uwezo wowote, lakini pia tuna idadi kubwa ya wazee kwa sababu pia *lifespan* imepanda.

Mheshimiwa Spika, kufikiria kwamba vyanzo hivi ambavyo tumekiweka hapa, ambavyo ni vipodozi na vilevi, asilimia mbili yake itakwenda kuchukua mzigo wa kuwatibu hawa watu tena wakawa na uhakika wa kutibiwa na kupata matibabu, ninaona ni kitu ambacho hakiwezekani. Yaani sisi kama Taifa leo tunafikiria kwamba tutategemea wanywaji au walevi ili watoto wetu wanapoumwa wawasaidie kuwatibu, wajawazito wetu wanapokwenda kwenye vituo vya afya au mahali popote kutibiwa tutegemee fedha zinazotokana na ulevi na tutegemee fedha zinazotokana na ulevi kuwasaidia baba zetu na mama zetu walioko vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi bima yangu kama Mbunge kwanza haimchukui mama yangu na haimchukui baba yangu, haijumuishi matibabu ya wazazi wangu. Sasa nikija kukatiwa hii bima nitatibiwa mimi na familia na watoto wangu. *Imagine*, mama yangu kaumwa kule kijiji, anakwenda hospitali halafu hela ya mlevi inamsaidia kumtibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama nchi, kama Taifa na kama viongozi, hebu tufikirie kwa kina tunadhani kwamba kweli wazazi wetu, wazee wetu wakatibiwe kutokana na mapato yanayotokana na ulevi.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, wazee wetu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpembenwe.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimpe taarifa mzungumzaji, anachangia vizuri sana lakini nataka nimwambie tu kwamba, Serikali inajaribu kuangalia vyanzo vya mapato kutoka katika maeneo tofauti ambavyo vinaweza kwenda kusaidia katika kuweza kutekeleza shughuli zake. Kwa hiyo, siyo kwamba fedha ya mlevi inakwenda kutumika, hapana. Isipokuwa Serikali wanachokifanya, wanaangalia vyanzo mbalimbali katika maeneo tofauti katika kuweza kukamilisha eneo hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, napokea kutokana na uzito wa mtu mwenyewe aliyeitoa, Mwakilishi wa Wananchi kutoka Kibiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninakubaliana nae kwamba Serikali inaangalia vyanzo tofauti tofauti vya makusanyo ya kwenda kutibu lakini kwenye chanzo hiki hapa ndiyo ambacho wenzetu Serikali wameona kitafaa. Yaani chanzo cha walevi, vileo na vipodozi, wamama waliojipaka poda na *angel face*, ndiyo tutegemee kwamba Mheshimiwa Waziri Mwigulu amefariki ghafla hatuombei, mke wake amebaki mjane akatibiwe na walevi! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hebu keti kidogo, Mheshimiwa Jesca, hizi fedha ulizozitaja hapo zina alama fulani? *(Kicheko)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, fedha gani?

**SPIKA:** Yaani hizi fedha ulizozitaja, hicho chanzo ulichokitaja fedha zina alama fulani, zikishakusanywa zina alama? *(Kicheko)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nikuambie, inasema hivi: Kuainisha kiwango cha ushuru wa bidhaa asilimia mbili kinachotokana na vinywaji laini, vileo, vipodozi. Ndiyo alama yake hiyo hiyo kwamba, huu mfuko utaingizwa na vyanzo hivi, alama ndiyo hiyo hiyo waliyoandika. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mimi nataka unieleweshe jambo moja, zikishakusanywa hizo fedha zinashida yoyote?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, shida haipo ila kwanza ni kidogo, yaani hii fedha kwamba tutegemee walevi wakauguze mama zetu, watoto wetu, wajawazito wetu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya jamani. Mheshimiwa Jesca kuna taarifa mbili zote zinataka kuja kwako lakini sasa Mheshimiwa Waziri amesimama kuashiria kwamba taarifa hii haiwezi kusubiri ufafanuzi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Jesca, ambaye nilivyomsoma yeye anachangia yuko rohoni zaidi ndiyo maana anataja hivi vitu lakini *common standards* za Mifuko ya Bima ya Afya vyanzo vyake huwa vinachukuliwa kwenye bidhaa iwe za kujipaka ama za kutumia ama chakula, ambazo kwa kitabibu zinasababisha magonjwa. Kwa hiyo, zile soda ambazo zinaweza kusababisha sukari, vipodozi ambavyo vinaweza

kusababisha magonjwa, vilevi ambavyo vinaweza kusababisha magonjwa, sigara inatozwa kule *in a way to discourage at the same time* unapeleka kwenye kutibia watu. Kwa hiyo, nautambua mchango wake uko rohoni lakini *best practice* inakuwa hivi na ninamuomba aunge mkono hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Waziri mkitukatisha tamaa kutumia hivyo sasa mtatoza wapi kodi? Mheshimiwa Msambatavangu, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu ameongea mambo ya rohoni lakini anithibitishie hapa, hizi bidhaa zinasababishaje ujauzito? Kwa sababu yeye amesema, duniani wanatoza kama vile wanatoza kodi kusaidia mifuko ya bima ya afya kwenye bidhaa zinazoleta madhara kwenye afya. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca....

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa Tarimo. Mheshimiwa Jesca ameuliza swali sasa Mheshimiwa Waziri hawezi kupata nafasi ya kukujibu. Lakini inasababishaje ni kwamba mtu akishatumia kwa maelezo sasa ya Mheshimiwa Waziri akishatumia hivi upo uwezekano mkubwa sana wa yeye kwenda kusababisha hicho ambacho umeuliza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Jesca kuna taarifa nyingine huku. Haya ngoja, taarifa ni moja baada ya nyingine. Mheshimiwa Jesca kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Matiko. *(Kicheko)*

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilikuwa nataka nimpe taarifa na ninashukuru Mheshimiwa Waziri amekuja tena pale pale. Nafikiri taarifa hoja tuijenge hivi, kwenye

vinywaji hasa vikali na vinywaji vingine ukiweka kodi, Mheshimiwa Waziri amesema hapa, dhumuni mojawapo ni kuwa-*discourage* wasitumie. Sasa taarifa hapa inakuja kwamba kama mmeiweka tena kwenye kitu muhimu sana, bima ya afya, kumbe mnajua watu wata-*withdraw* hawatakunywa pombe. Hii inamaanisha kuwa siyo *reliable source* ambayo tunaweka kama mapato; mmeweka kama pambo kama sio *reliable source* kwenda kutibu Watanzania mmeweka tu kufunika hatutapata hela za bima ya afya kama watu wa ku-*withdraw* kama alivyoiweka Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca unapokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa naipokea. Hiyo taarifa ndiyo imeenda shule sasa. Yeye anataka ku-*discourage* watu wasinywe, halafu watu wataendelea kuumwa magonjwa mengine, watu wataendelea kuwapa watu ujauzito watu watatibiwaje sasa wakati hawa wameacha pombe kwa kuwapa gharama kubwa ya pombe? Ndiyo maana mimi nimesema kuwa chanzo hicho hakitakiwi kufikiriwa na mchumi mkubwa kama Mheshimiwa Dkt. Mwigulu.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge taarifa zimekuwa nyingi sana. Mheshimiwa Tarimo.

**TAARIFA**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ujauzito si ugonjwa.

**SPIKA:** Hee! Mheshimiwa Jesca Msambatavangu unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naipokea, lakini ujauzito pia kunatokea ni matatizo ya afya lakini

naipokea taarifa yake kwa maana kwamba sasa unapomuweka mjamzito kuja kutegemea chanzo ambacho ni pombe ambayo wewe unawabana watu wasinywe pombe ili kumtibu mjamzito yani ndiyo hicho kitu ambacho mimi nilikuwa natakaa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa Mheshimiwa Mbunge umekimbia sana na hizi taarifa zimeshakuwa nyingi kwake, kwa hiyo tumuache amalizie sasa mchango wake. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha wajaribu kuangalia, kwa kweli hiki chanzo siyo *reliable.* Hiki chanzo kiroho kitatukosesha pia baraka kwenye hii nchi; hatuwezi kuacha wazee wetu sisi wakatibiwa na walevi.

Mheshimiwa Spika, lakini nyinyi mnawafahamu walevi walivyo. Kuanzia tarehe 01 Julai tutakuwa hatupiti humu, walevi watatuambia ninyi hamna lolote wake zenu wakiwa wajawazito sisi tunawatibu, watoto wetu tunawatibu nyie wenyewe wazee wetu tunawatibu, watu wenu wenye ulemavu tunawatibu.

Mheshimiwa Spika, naomba hili liangaliwe. Ahsante.

**SPIKA:** Napata picha tungeambiwa sehemu kubwa ya mishahara yetu inatoka huko kama ingekuwa, kama pengine huu mjadala ungekuwa tofauti kidogo kama tungeambiwa kukaa kwetu humu ndani pesa nyingi inatoka huko. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kutoa mchango wangu

katika Muswada huu wa Fedha. Kwa bahati njema mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti. Tulipata nafasi ya kuwasikiliza wawekezaji wa viwanda vya sukari; na tulipowasikiliza walitupa mkakati wao wa kuzalisha sukari ya kutosha katika Taifa letu katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika mwaka wa fedha 2024/2025 wamekusudia kuzalisha sukari inayofikia tani 600,000. Mwaka 2025/2026 wanakusudia kuzalisha sukari itakayofika tani 700,000. Kwa maana hiyo ikifika mwaka huo Tanzania itajitosheleza kwa mahitaji ya ndani ya sukari na kuuza sukari nyingine ya ziada katika nchi za Afrika ya Mashariki. Hili ni jambo la faraja sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu sisi kama Taifa tuna wajibu wa kuvilinda viwanda vyetu vya ndani kwa wivu mkubwa sana ili vitekeleze wajibu wao huo wa msingi; na hasa tukizingatia kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewekeza fedha nyingi sana katika sekta ya viwanda. Kwa mfano Kilombero, *TPC* Moshi, Mkulazi tumeweka fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, huku nyuma niliwahi kusema na leo narudia; kwamba Tanzania hatuna upungufu wa mipango iliyo bora na hatuna upungufu wa Sheria tatizo letu ni mambo mawili tu. Kwanza *mind set* (mtazamo), la pili ujasiri wa kufanya maamuzi magumu katika wakati sahihi. Haya ndiyo matatizo yetu kama Taifa. Kwa ushauri wangu, tuvipe uwezo Bodi ya Sukari na *NFRA* ili vitekeleze wajibu wao wa msingi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; Tanzania hatuzalishi mafuta, tunaagiza mafuta nje na tunatumia zaidi ya asilimia 70 ya fedha za kigeni kuagiza mafuta katika nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi. Kwa hiyo uamuzi wowote tutakaoufanya kama Bunge na kama Taifa kuifanya Nishati ya magari iwe nafuu ili magari yote ikiwezekana Tanzania tumie nishati. Huu utakuwa ni uamuzi wa kimapinduzi. Nafikiri hiyo ndiyo rai yangu kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo; tukifanya uamuzi huu wa kimapunduzi tutaokoa fedha za kigeni ambazo tunazitiitaji kuzipeleka nje, mfumuko wa bei utapungua sana kwa sababu magari yote yatakuwa yanatumia gesi, na kwa maana hiyo gharama za uzalishaji na usafirishaji zitapungua sana. Faida ya pili, fedha ya Tanzania itapata utulivu na thamani itaongezeka. Tatu tutakuwa tunaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mtetezi mkubwa sana wa nishati safi na salama.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali yangu; tufanye kila linalowezekana, tuwakaribishe wawekezaji watakaowekeza katika vituo mbalimbali vya nishati ya gesi katika mikoa yote ya Tanzania ili Watanzania walio wengi waingie kwenye uchumi wa nishati ya gesi. Tukifanya hivyo bila shaka uchumi wa Tanzania utaimarika sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho; ukiwasikiliza wafanyabiashara waliyofika katika Kamati ya Bajeti wanasema kwamba mfumo wetu wa kodi si rafiki sana; na utaratibu wetu wa kukusanya kodi kwa kusisitiza *EFD* unaleta mizozo isiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na wakapendeleza, na mimi nitasisitiza hapa kwa sababu naiona hoja katika pendekezo lao. Sisi Wajumbe wa Kamati ya Bajeti Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wetu si mara moja, si mara mbili tumekuwa tukiiambia Serikali iimarishe mifumo yetu ya ukusanyaji kodi. Kwa mfano kwa *TRA*, *TPA* na halmashauri mifumo isomane ili tudhibiti udanganyifu. Lakini tunaomba jambo hili halijafanyiwa kazi katika uzito unaostahiki.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tumekuwwa tukipendekeza kwamba wakati umefika wa kuacha utaratibu wa kutumia fedha taslimu, tutumie mifumo ya kisasa kama vile M-PESA, *credit card* na *Visa card* ili iwe rahisi kukusanya kodi inayostahiki. Huu utaratibu wa kufukuzana wafanyabiashara umepitwa na wakati ndugu zangu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwa mawazo yangu mambo haya matatu Serikali ikiyafanyia kazi nina matumaini makubwa sana tutaweza kuongeza mapato ya Serikali ili yaweze kukidhi matarajio ya Watanzania waliotupa dhamana ya kuongoza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na fursa ya kuchangia Muswada huu ulio mbele yetu wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan; kwa sababu kwenye mazingira na jografia yetu na nchi zinazotuzunguka bila shaka Watanzania wamekuwa wakifuatilia mambo yanayotokea. Hayapo hapa kwetu kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikileta Sheria ya Fedha ambayo ni shirikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia tena jambo hili ni la msingi sana, kwamba Sheria yetu ya Fedha ni sheria shirikishi. Wadau wanaanza wanasikilizwa kwenye *task force* ya Serikali wakishindwana huko wanakuja kwenye Kamati yetu ya Bajeti, Kamati ya Bunge lako. Kwa taarifa ambayo ameiwasilisha Mwenyekiti wetu wa Kamati tumesikiliza zaidi ya wadau zaidi ya taasisi zaidi ya makundi 40. Vile vile Kamati yako ya Bajeti imefanya mashauriano na Serikali kuhusu Sheria hii ya Fedha kwa takriban miezi mitatu. Ndiyo maana ninasimama hapa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali ya CCM kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Fedha ambao ni shirikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo mawili tu ya kushauri. Kwenye ukurasa wa 119 wa Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Bajeti ya

Serikali Kuu, kipengele cha (g) anasema kutoza ushuru wa forodha kwa asilimia 50 badala ya kiwango cha asilimia 35 au asilimia 25 kwenye chumvi inayotambulika kwa *heading* 2501. Lengo la hatua hii ni kulinda uzalishaji wa chumvi katika viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, hii *item* inayotajwa ya 2501 *ni raw material* inayoagizwa kutoka nje halafu inachanganywa na chumvi yetu ya ndani alafu ndiyo tunapata chumvi iliyo safi na iliyo bora kwa matumizi. *Raw material* hii inaagizwa na nchi za jirani pia kutoka nje wanaingiza kwenye viwanda vyao na wanaleta kwetu kwa kutumia ile sheria ya *root of origin* ya bidhaa. Kwamba bidhaa yoyote inayozalishwa ndani ya *East Africa* inatembea na kwenda pote.

Mheshimiwa Spika, sasa tukitoza hii, tukiongeza asilimia 50 hapa tutakuwa hatulindi viwanda vyetu badala yake tunavifanya vishindwe kushindana kwa sababu wenzetu hii *raw material* kule kwao hawaitozi. Sisi hapa tukiitoza maana yake tutafanya uzalishaji wetu uwe ghali na chumvi ikifika sokoni itakuwa ghali ya kwetu kuliko ambayo inatoka kwenye nchi za Afrika Mashariki. Hili ilikuwa ni jambo waliangalie. Ikiwezekana Serikali wapeleke maombi maalumu *East Africa* sisi tuondoe hii. Hii haitatusaidia zaidi ya kuua viwanda vyetu vya ndani na siyo kulinda.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada wetu ambayo inahusiana na *Amendments of the Excise Act. Cap* 147 kwenye lile jedwali (f) inapendekeza kutoza ushuru wa shilingi 7,000 kwa *ethanol* inayoingizwa kutoka nje. Kwenye hili tunalo kundi la wananchi wa Tanzania na wengi wakiwa ni vijana, na hili Serikali watuelewe, hasa tunapoongelea mambo yanayohusu vijana na wakizingatia takwimu za vijana kwenye sensa tuliyoifanya. Sisi Waheshimiwa Wabunge tusingependa jambo lolote linalogusa vijana lisichukuliwe uzito.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili vijana wetu wengi wamejiajiri kwa kuagiza hii *ethanol* kwa sababu hatuizalishi. Hapa ndani ya nchi tunazalisha *ethanol* kwa asilimia 30 tu ya mahitaji yetu, na asilimia 70 yote tunaiagiza. Kwenye eneo hili ni vijana ndio

waliojikita hapa; vijana wenye mtaji wa milioni 100, milioni 90, milioni 150. Ukiweka hii kwamba unataka kuikusanya kodi hii kwa *importer* tafsiri yake ni kwamba mtu anapoagiza bidhaa hii kijana wetu anapoagiza bidhaa hii ikifika bandarini atashindwa kuikomboa, atashindwa kukomboa kwa sababu patahitajika alipe fedha nyingi zaidi hii 7000 uliyoweka.

Mheshimiwa Spika, sisi ambacho tulitaka Kamati ya Bajeti hatukatai chanzo hiki ambacho Serikali inakwenda kukusanya zaidi ya bilioni 154. Tunachopishana na Serikali ni kwamba tunataka chanzo hiki kitozwe kwa *manufacture* wa pombe kule mwisho ili kwamba tuipitishe kwa mlaji iwe rahisi kuikusanya. Ukiweka kwa huyu mwagizaji unawafanya watu washindwe kuagiza hii kwa sababu mitaji yao itakuwa ni midogo kuliko fedha ya kukombolea. Hivi tunavyozungumza ipo mizigo ambayo iko njiani, iko baharini inatembea na meli inakuja.

Mheshimiwa Spika, halafu mtu anafika alitarajia akomboe kontela lake kwa milioni 90 leo anakuja anakutana na milioni 240...

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpembenwe.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, mzungumzaji anazungumza vizuri sana, na mimi nataka nimpe taarifa tu kwamba vijana hawa amabo wanafanya shughuli hizi wengi wao ni wa kawaida na wamekopa fedha benki na wanategeea kupokea mizigo yao ambayo ipo kwenye maji. Kitendo cha bei hiyo kuongezwa itakuje kuleta shida kubwa sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mheshimiwa Kwagilwa unapokea taarifa hiyo?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, naipokea Taarifa hii. Serikali wanachotakiwa kufanya kwa sababu bidhaa hii ni *very sensitive* na siyo kila mtu anafanya hii biashara kila mwenye kufanya biashara hii ripoti zake anazowasilisha kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mzigo anaoleta, kwa mzigo nani kamuuzia na viwango gani vimekwenda. Wao Serikali wawe *efficient,* yaani mapungufu yaliyopo katika kukusanya mapato kwenye taasisi zetu yasifanye wananchi wetu sisi wapate shida. Hii tunashauri.

Mheshimiwa Spika, na mimi sijui ni kwa nini Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wanapata ugumu kulielewa hili tunalolishauri Wajumbe wako na tumelishauri hili kwa miezi mitatu haiwezekani. Tunashauri jambo moja kwa miezi mitatu nyie hamlielewi hatukatai kodi hii kupatikana, kodi hii itapatikana lakini tunachosema wasitozwe hawa watu kwa sababu watakosa uweze, itakuwa ni gharama kwao kuagiza...

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, hawa wafanyabiashara wanaozungumzwa kwa mara ya kwanza kodi yao imeongezeka kwa 1000% kwa mara ya kwanza kwa hiyo atazamwe vizuri sana mahali hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mheshimiwa Kwagilwa unapokea taarifa hiyo?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaipokea Taarifa kama Kanuni yetu na Mheshimiwa Katani ni afande mwenzangu, kwa hiyo anaelewa pia anachokizungumza, yupo vizuri. Yote haya ninayopewa taarifa na Waheshimiwa Wabunge ni kuonyesha kwamba Waheshimiwa Wabunge tupo *serious* kwenye jambo la kulinda ajira za vijana wetu. Vijana hawa wana mikopo benki lazima tuwalinde na benki zetu tuzilinde.

Kwenda kinyume na hili nikuonesha kwamba watakwenda ku-*default* kwenye malipo yao kwenye mikopo lakini wanafamilia zinazowategemea na pana *chain* kubwa nyuma yao.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatokea wapi, nasikia sauti.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, maadamu Mheshimiwa Ruben amethibitisha kwamba Mheshimiwa Katani ni Afande mwenzake na tulienda nao Jeshini ni wazalendo wenzangu, mimi nataka kumuongezea mchango kwamba, kodi hiyo iliyovyoongezwa kwa hao wafanyabiashara wa vileo mimi naona inaweza ikawa sawa tu ili wafanyabiashara wasiagize pombe nyingi kutoka nje bali waongezewe uwezo kwa sababu watumiaji si ni hawa hawa Watanzania wanakunywa pombe, waongezewe uwezo wakajifunze namna ya kuzalisha pombe hizo hizo kama za nje, wazalishe kutoka kwenye nchi yetu ili sisi tutosheleze soko la ndani na tuwapelekee wale wenzetu ambao wanatuuzia pombe. Kwa hiyo, tutapata pesa nyingi za kigeni na kwa uzalendo huo huo Mheshimiwa Kwagilwa tulioenda Jeshini naomba upokee taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kwagilwa, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, nimweleweshe tu Afande mwenzangu Mheshimiwa Mbunge, hapa hatuongelei pombe, tunaongelea *ethanol* ambayo *alcohol content* yake ni zaidi ya asilimia 90, hii ukinywa unazikwa saa hiyo hiyo, hii siyo

pombe hii ni *raw material* ya kwenda viwandani, pombe itapatikana baada ya hii kuchakatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nisisitize jambo hili ni la msingi sana wala hatuna sababu ya kuvutana kwamba kodi hii tuliyokusudia kuipata tutaipata lakini tukaikusanye kwenye pointi ya mwisho, tusiikusanyie hapa katikati, tunakwamisha tu Watanzania bila sababu. Kumbukeni kwamba hatujaweza kutoa ajira nyingi zakutosha, pale mtu anapokuwa amepambana kupata mahala pa kujishughulisha tusipa-*disturb. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo nakushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja, naamini Waziri wa Fedha ni msikivu atalichukua hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo atafuatiwa na Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia na mimi niseme tu kuna mambo mawili ambayo ningependa kuyaangazia na sijui *practice* ikoje maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, bajeti yetu tunapitisha, kanuni inatutaka tarehe 30, lakini tukiipitisha tarehe 30 inatakiwa tarehe moja ianze kutumika, sasa jambo alilokuwa anaongea mzungumzaji aliyepita ni kwa sababu mtu aliyeagiza *ethanol* kama *raw material* ambayo nyingine iko bandarini nyingine meli itaingia kesho na keshokutwa atakutana na ushuru mara elfu moja, sasa hapo ndipo tatizo linapoanzia. Kwamba saa nyingine unakutana na ushuru ambao unaweza ukawa zaidi ya mzigo ulionao, sasa ni vizuri tuwe tunakipindi labda cha kusema kwamba sheria hii haswa inapokuwa imeongezeka sana iwe na muda wa lini ianze kutumika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilikuwa naomba nipate…

**MHE. RAMADHAN S. RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo, kuna taarifa sijui inatokea wapi?

**MHE. RAMADHAN S. RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, kwa Mheshimiwa Ramadhan niko huku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan.

**TAARIFA**

**MHE. RAMADHAN S. RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kwa mfano sasa ilivyo ni shilingi mia tano, kwa mfano kwa mfanyabiashara huyo kijana mdogo anayesemwa, akiagiza lita laki nne kwa mwezi atalipia shilingi milioni 200, baada ushuru huu kupita kwenda shilingi 7,000 kutoka shilingi 500 atatakiwa alipie *two billion shillings* kutoka shilingi milioni 200, huyo kijana anaitoa wapi *two billion shillings*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa, lakini nadhani hili wewe unaweza ukatupa mwongozo. Hivi Wizara inapokuwa imeleta hoja halafu kamati imeleta hoja pingamizi, sisi kama Wabunge tunasimama wapi? Mimi nilikuwa nadhani kamati ikileta hoja inayosema tofauti nilikuwa nadhani sisi tunasimama upande wa Bunge ambao ndio wa kamati, na hii ni kwenye hili la *ethanol,* utatuongoza, lakini pia kwenye ile kodi ya gesi kwa magari yaliyobadilisha yakatumia mfumo wa gesi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati kwa sababu ilikuwa kwenye ile Ibara ya 71 na Taarifa ya Kamati ukurasa wa 14 wamekataa kwamba ile kodi ya shilingi 382 kwa magari ya gesi ikataliwe kabisa. Sasa hebu tuongoze tutasimama wapi kwa sababu nadhani kamati zinafanya kazi kwa niaba yetu na Serikali iko upande mwingine. Sasa kama ndio hivyo, basi tunapoenda kuazimia sisi tukae upande wa kamati moja kwa moja hatuna haja

ya kuvutana kwenye haya mambo ambayo tayari kamati yenyewe imeshayakataa kwa niaba yetu.

**MHE.CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa hapa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**TAARIFA**

**MHE.CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, najaribu kujiuliza, kama hoja ni *ethanol* ambayo kama Mheshimiwa Mbunge anavyochangia na Waheshimiwa Wabunge waliopita, ni *ethanol* kuonekana kupandishiwa kodi.

Mheshimiwa Spika, hapa hapa nchini kwetu tuna bidhaa nyingi ambazo tukizitumia zinazalisha *ethanol.* Mfano tu kwenye gongo, gongo hairuhusiwi hapa nchini kwetu kwa sababu ina *ethanol* na *methanol,* sasa si ndio wakati rasmi ya kwamba gongo ihalalishwe na hawa wafanyabiashara wanaoongelewa wakazalishe *ethanol* nyingi ambayo sasa itumike hapa nchini, kwa sababu kwani ni lazima tuagize *ethanol* kutoka nje? Hatuwezi kuja na njia mbadala ambayo inaweza ikazalisha *ethanol* kwa wingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, siipokei, naomba niendelee na mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, pia nilitaka kuishauri Wizara katika kulinda baadhi ya vitu vya ndani, walishafanya kitu na kikafanikiwa. Kwenye ushuru wa magari walishaweza kufanya uchunguzi wakajua magari *model* fulani wakaweka bei na wakaweka kile cha kupigia hesabu kwenye *site* kimeondoa hayo matatizo. Sasa kuna vitu vingine bado hatujaweza, kuna baadhi ya vitu vinaagizwa kutoka nje vinashindana na ambavyo tunavyo ndani lakini ukiangalia bei

wanayotuletea wale wanaotuletea kutoka nje inakuwa haiendani kabisa na uhalisia.

Mheshimiwa Spika, Mfano tu, kuna sabuni inatoka Indonesia inaitwa Malaika ukiangalia hela inayokuja nayo na bei inayoingianayo sokoni ni dhahiri kabisa kuna udanganyifu mkubwa sana hapo katikati kwa sababu inakuja inakuwa bei rahisi kuliko sabuni zinazotengenezwa hapa na zinazotengenezwa East Africa. Maana yake ni nini, tunaomba kuwe na kitengo cha kwenda kuchunguza kama mnavyofanya kwenye magari kwamba tunajua Gari *Model* fulani ushuru wake utakuwa ni huu, kwisha kusiwe na mambo ya ku-*negotiate* sasa inatoka sabuni kwa sababu ina jina la Kiswahili inaitwa Malaika inatoka huko Indonesia ikija hapa inakuwa bei rahisi kuliko hata za hapa kwa sababu ya huo udanganyifu. Nilikuwa naomba pia niwashauri kwenye hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wizara na niwashukuru kwa kuliona hili kwenye ile Ibara ya 23, kwenye zile sarafu kutumika kwenye michezo ya kubahatisha, sio tu kwamba wao wame-*site* zaidi uchakavu lakini hata chenchi zilikuwa hazionekani madukani. Wale watu wakishaingiza zile mashine zao ambazo zinatumia hizo *coins, coins* zinapotea kwa sababu wao wanazikusanya kwa ajili ya kutumia kwenye maeneo hayo kwa ajili ya hizo kamari, kwa hiyo, nashukuru sana kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Spika, niipongeze tena Serikali kwenye ile Ibara ya 87(86)(1) pamoja na maelezo aliyoyatoa Waziri jana kwenye kamati mazuri sana kwamba ile kodi ya juu ya shilingi milioni 15 niwapongeze sana na nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuliona na kurudisha kwenye shilingi milioni nne angalau wafanyabiashara wapumue kwa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vuai alivyoongelea suala la *NFRA,* mimi nilikuwa na suala la kuongeza tu pale, *NFRA* tunaiwezesha kununua au kutoa vibali? Kwa sababu kama ni kununua na ku-*stock* litakuwa ni jambo zuri, kwa sababu jukumu lao ni kufuatilia kwa muda wanaweza kuwa na uwezo mzuri wa ku-

*manage*, lakini kama ni kutoa vibali mimi nadhani bado tutakuwa hatujatibu hilo tatizo na hilo tatizo linajirudia rudia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kuuliza, katika ile Ibara ya 69 na 70 ya ile hela ambayo itapatikana kutokana na mafuta kupungua bei ambayo inaenda kwenye mfuko wa dharula. Ni kwa nini iende kwenye mfuko wa dharula isiende moja kwa moja *Road Fund?* Kwa sababu nia yake ni kwenda kutengeneza Barabara. Tunajua hapo kwenye mfuko wa dharula kipindi ambapo inasubiri kuhamishwa lolote linaweza kutokea hayo ndiyo mambo ya *Escrow Account* na nini. Nilikuwa nafikiri kwa nini kama tumeshaamua hela itakayotokana na kushuka kwa bei ya mafuta kama alivyosema kwenye ile Ibara ya 69 na 70, kwa nini isiende moja kwa moja kwenye *Road Fund,* isiende moja kwa moja kama ni kwenye *TARURA*, kwa nini inaenda kwenye Mfuko wa Dharula halafu ndiyo ije ihamishiwe huko? Mimi naona hilo kidogo ni kuzunguka sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamisi Mgalu, Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Fedha. Kwanza kabisa kwa sababu kesho ndio siku ya mwisho ya Bunge letu hili la Bajeti, naomba nitumie nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Spika *the way* ulivyoliongoza hili Bunge kwa miezi mitatu na kwa ufanisi, na kwa kifupi umetulinda sana sisi Wabunge wenye mihemko, nikushukuru sana kwa jinsi ulivyotuvumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niipongeze sana Serikali hasa hasa kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha kwa kukubali kuondoa matumizi ya mashine ya *Electronic EFD* kwa wakulima, kwa kweli hili umewatendea haki wakulima.

Lakini kingine nipongeze Serikali na Mheshimiwa Waziri kwa kukubali kuondoa ile asilimia mbili ambayo mlitaka kutumia kama mbadala wa ile *EFD* kwa wakulima kwa sababu hawa wafanyabiashara wa kati wangeirudisha tu kwa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi hoja yangu ni moja, Ibara ya 98(55)(a) kinapendekeza Serikali iendelee kutoa msamaha wa kodi kwa viwanda vinavyozalisha mbolea hapa nchini. Ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi tulifanya hivyo kwenye vishikwambi, tuliondoa kodi tukiamini kwamba hivi vishikwambi vitashuka bei havijashuka bei, tulifanya hivyo kwenye taulo za kike tukaondoa kodi  tukiamini kwamba hao wanaozalisha taulo za kike zitashuka bei, sasa kwa miaka mitatu tangia 2022, 2023, 2024 hao wenye viwanda vya kuzalisha mbolea wamekuwa wakinufaika na hii misamaha ya kodi lakini hawajawahi kushusha bei ya mbolea na kama isingekuwa Mheshimiwa Rais Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kutoa ruzuku ya mbolea sijui leo tungekuwa wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mimi nikuombe hawa wenye viwanda ambao wanazalisha mbolea nchini wanapata *double profit*, kwanza wanaruzuku ya Serikali pili wana msamaha wa Serikali. Mimi niombe Serikali itoe bei elekezi ya mbolea inayozalishwa nchini, lazima kuwe na tofauti, maana yake sasa hivi hakuna tofauti kati ya mbolea inayoingizwa nje na mbolea inayozalishwa hapa nchini, wote wananufaika na msamaha wa kodi na bei ni ile ile moja.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini tunaendelea kuwapa msamaha wa kodi? Mimi naomba tutoe bei elekezi *otherwise* basi mwezi wa tisa sisi tutaleta tufanye mabadiliko ya sheria huo msamaha uondoke, kwa sababu sasa hivi wanatembelea nyota ya Mheshimiwa Rais hawajashusha mbolea na bado wanaendelea kunufaika na msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo nikushukuru tena, mimi mchango wangu umeishia hapa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, muda ukiruhusu Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege pia atachangia.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu kwenye *Finance Bill* ya Mwaka huu 2024 ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna alivyotutendea mema kwa kipindi chote cha Bunge hili la Bajeti kutupa afya njema na kushiriki shughuli mbalimbali za Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee pia nikupongeze sana Mheshimiwa Spika wetu kwa kuendesha Bunge hili kwa viwango, lakini pia kwa kuendesha Bunge hili kwa kutumia *4R, Reconciliation, Resilience, Reforms* na *Rebuilding* katika mambo mbalimbali ambayo yametuwezesha leo kufikia hapa na huku tukiwa tumeipigia bajeti yetu kura za kishindo 92%. *(Makofi)*

Mheshimmiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu tangu ameingia madarakani bajeti zote zilizofuatia hakuna bajeti ambayo imepata kura ya hapana. Hii inaonesha ni namna gani ndani ya Bunge makundi yote kwa namna moja au nyingine tunaona utekelezaji wa bajeti unavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia mambo machache kwenye hii *Finance Bill,* kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuja na mapendekezo kwenye Sheria hii ya Bajeti Sura 439 kifungu cha 37 ili kuwezesha mfuko wa dharula. Hii ni hatua ya kwanza kabisa, inaonesha Serikali imesikia kilio cha watanzania katika maeneo mbalimbali ya uharibifu wa miundombinu uliotokea kutokana na sababu ambazo ziko nje ya uwezo wetu sote.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa miundombinu, binafsi kupitia Wizara tuliyofanya *UWT* Taifa tumefika karibu kata 854 na hatukukwama popote, tumeona kazi nzuri ya *TARURA*, tumeona kazi nzuri ya *TANROADS* lakini kutokana na jambo la mabadiliko ya tabia nchi na namna ambavyo mvua zimekuwa nyingi uharibifu ni mkubwa. Lakini dhamira ya Serikali kuja na kifungu hiki binafsi kupitia kamati yetu tumeunga mkono na hasa iliposema asilimia moja ya matumizi ya Serikali kila mwezi. Pia hii ni mojawapo ya ku-*control mechanism* ndani ya Serikali ya kujibana kwenye matumizi na kupeleka kwenye mfuko huu, hongereni sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, naipongeza Serikali kwenye mabadiliko ya Sheria ya Korosho Sura ya 203(17)(a). Sisi *UWT* Taifa chini ya Mama Mary Chatanda na Mama Shomari tulifanya ziara kwenye mikoa inayolima korosho, Mikoa ya Kusini na Mkoa wa Ruvuma, tumeona kazi nzuri ya Serikali ya kusambaza pembejeo bure na ni kwa mara ya kwanza kabisa ndani ya miaka hii mitatu. Sasa hatua hii ya kuwezesha tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje na mapato yote kupeleka Bodi ya Korosho na ninavyozungumza hapa nataka nimpongeze Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho ametuunganisha wadau wa korosho kwenye *group* moja tunaangalia usambazaji wa pembejeo hii tunatoa maoni ni hatua ya mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara ya Kilimo na Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo imewekeza kwenye zao hili. Natambua changamoto za kwenye soko, lakini tuna imani, mikakati iliyowekwa zao hili litatoa mchango mkubwa hasa upatikanaji wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nataka niishukuru Serikali kwa mara ya kwanza iliwasilisha hapa jambo kubwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, ni jambo ambalo halijawahi kuwepo. Tunatambua ni jambo kubwa lakini kwa kuonesha dhamira ya kuanza kudunduliza kwenye mfuko huo ili ifikapo 2026 huduma zianze kutolewa ninaunga mkono mapendekezo ya kwenye ushuru

wa bidhaa ili mapato yapelekwe kwenye huo mfuko lakini kipekee kwa kuwagusa makundi ya watoto chini ya umri wa miaka mitano, kundi la wamama wajawazito na makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, kwenye ziara zetu maswali yanaulizwa kuhusu huduma ya mama mjamzito na mtoto chini ya miaka mitano kwenye makundi hayo, wanaamini kwamba Serikali ilisema huduma ni bure chini ya makundi hayo. Lakini kwa kuwepo chanzo hiki mimi naamini kwa sababu tangu tumepata uhuru chanzo hiki cha ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za bia, bidhaa za vipodozi kimekuwepo nyakati zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru sana hao wanaoitwa walevi, niwashukuru tunaojipodoa kazi yao ni nzuri kwa sababu imewezesha kwa namna moja au nyingine ku-*finance* bajeti ya Serikali na imefanya mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pia ninashukuru tozo ya maendeleo ya viwanda, hili ni jambo jipya lakini tunaiona dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba sekta ya viwanda inaendelea kukua. Kwa hiyo, ninashauri tu Serikali pesa hizi ijielekeze kwenye viwanda vidogo vidogo vilivyopo maeneo ya vijijini ili viweze kutoa mchango mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia nina ushauri kwenye suala zima la Sheria ya Madini, Sura 123(59) Serikali mmewekeza, mmetoa ushawishi, mmeshawishi wawekezaji kujenga viwanda vya kuchenjua dhahabu, tunacho pale Mwanza lakini kipo Geita kinachoongozwa na mwanamama Sara Masasi.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali, Kifungu kimekaa vizuri lakini kiangalie namna gani kitawezesha hasa hivi viwanda vya uchenjuaji dhahabu kupata malighafi ya kutosha. Viwanda hivi vimepata Ithibati ya Kimataifa, kwa hiyo, kwa kuwa tunachangamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni nina imani Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Serikali mkikaa vizuri na mkaangalia mchango wa viwanda hivi kwa sababu vipo na ninyi wenyewe ndio

mmeshawishi watu wamewekeza muwasaidie ili kifungu hiki kitekelezeke na ikiwezekana hata hayo madini ambayo yanatakiwa kusafishwa, kuuzwa hapa nchini iwe zaidi ya 20% kama ambavyo imependekezwa kwenye sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kwenye tasnia ya sukari. Serikali mlikuwa walezi kwa miaka mingi. Hata hivyo, ndani ya miaka hii minne kuanzia Awamu ya Tano mpaka sasa hivi Awamu ya Sita, Serikali na nyie mmepata Watoto wenu; Kiwanda Cha Mkulazi, mna-*share,* Kilombero na *TPS*. Naomba muongeze ulezi. Vilevile, katika kuilinda sekta hii ya sukari muongozwe na *4R (Reconciliation, Resilience, Reforms* na *Rebuilding),* ili tuone mchango wa sukari na nchi yetu ifike wakati iache kununua au kuagiza sukari nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, uwezo tunao, nia Serikali inayo, nguvu inayo na dhamira inayo. Baada ya kusema maneno hayo naomba kuunga mkono Muswada huu wa *Finance Bill.* Kila la heri Mheshimiwa Mwigulu na wenzako wote na pongezi sana Serikali, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, ikiwa muda utabaki Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, jambo la kwanza nasema ninaunga mkono haya mabadiliko ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaleta kwenye maeneo mbalimbali. Vilevile, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri hili suala la *ethanol* litatuletea kelele nyingi sana kwa vijana huko nje.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wameagiza mzigo uko bandarini na unakuja. Kama walivyochangia wenzangu, ongezeko la zaidi ya asilimia 1,000 linahatarisha sana ajira za vijana wetu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, hicho ndicho kile chanzo cha kwenda kuwatibu wajawazito na Watoto. Sasa Mheshimiwa Waziri aangalie namna ambavyo kinavamiwa kwamba, kisitumike, halafu itakuwaje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, mchangiaji ni Mwenyekiti Mstaafu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Iringa. Kwa hiyo, ninaheshimu hilo alilolizungumza.

Mheshimiwa Spika, ninasema tu kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha uliangalie hili jambo kwa ukaribu sana na timu yako. Suala la *ethanol* litatuletea vurugu, hususani unapozungumzia vijana wa Taifa hili na ni sekta binafsi, ambayo Mheshimiwa Rais anatamani ifanye vizuri. Kuongeza tozo hii kwa zaidi ya asilimia 1000 una *discourage* maendeleo ya sekta binafsi.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie jambo hili kwa ukaribu kwa sababu, linahusisha ajira za vijana, lakini pili linahusisha vijana ambao ni Watanzania wengi tunaowategemea kwenye nguvu kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**TAARIFA**

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe Taarifa mwanafunzi wangu, Mheshimiwa Sanga kwamba, vijana hao unaowatakia mema kwa kutaka matumizi ya *ethanol* yawe makubwa ndiyo wanaendelea kudhoofika. Pia, tunaweza tukapata malighafi ya kutengenezea pombe kutoka kwenye mazao ya korosho, mabibo na mazao ya miwa. Hivyo, viwanda vya ndani vikifanya vizuri kama ambavyo Serikali ya awamu ya sita inasisitiza tunaweza pia, kupata malighafi ya hizo pombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, unapokea hiyo Taarifa?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa sababu, ni Mwalimu aliyefundisha pale Makete, Shule ya Mwakavuta Sekondari kwa hiyo, ninakuheshimu sana. Hata hivyo, tafsiri ya *ethanol* isichukuliwe kama ni pombe tu.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Katani.

**TAARIFA**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, ieleweke wazi hapa kwamba, *ethanol* inayozungumzwa inajadiliwa sana na wengine kwenye sekta ya pombe. Hata hivyo, *ethanol* hii inapoingia ni asilimia mbili tu ya *ethanol* inayokwenda kwenye pombe. *Spirit* inayotumika hospitali na nini ndiyo inayotokana na zao hili. Kwa hiyo, ni kitu ambacho ni mtambuka kiangaliwe kwa mapana sana, isije ikabebwa kama pombe, ni *two percent* two ya *ethanol* inayoingia inakwenda kwenye pombe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, kaa kwanza. Nilikuwa naangalia hapa Taarifa ya Kamati, Ukurasa wa 10, inaeleza kuhusu, "Serikali

inapendkeza kutoza ushuru wa bidhaa kwenye *ethanol* yenye kilevi zaidi ya asilimia 80 itakayozalishwa ndani ya nchi kwa shilingi 5,000 na itakayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa kiwango cha shilingi 7,000 kwa lita".

Sasa naona michango mingi inazungumzia ile inayotoka nje ya nchi kana kwamba, ndiyo imepanda pekee. Hata hivyo, kwa taarifa hii iliyowekwa hapa inaonekana na ya hapa nchini imepanda. Sasa sina hakika watu wa kamati, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti, hebu tufafanulie vizuri hili, ili sisi tusio Wajumbe wa Kamati tuelewe vizuri.

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Uko sahihi ni kwamba, hiyo *ethanol* kuna ambayo inazalishwa nchini na ile inayotoka nje pia, imepandishwa kwa shilingi 5,000 kwa ile ya ndani na shilingi 7,000 kwa ile ya nje. Vilevile ukiangalia zaidi sisi kama kamati tulisema tupunguze kwa asilimia 50, ili iwe shilingi 2,500 kwa shilingi 3,500 pia, waangalie ni namna gani ambayo tuwasaidie hao vijana ambao wanafanya hiyo biashara na wana mitaji midogo. Ni kwamba, kwa mtu anayelipa shilingi milioni 80 sasahivi atakuja kulipa shilingi milioni 240 ambayo ni zaidi ya mitaji waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulitaka hii ambayo haitumiki kwenye pombe peke yake, kwani inatumika hata kwenye *sanitizer*. Kwa hiyo, tuliiomba Serikali iwasaidie vijana ambao wamejiajiri na isaidie viwanda vya ndani, ili viweze kuwa na manufaa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi la kamati ni kupunguza kwa asilimia 50.

**SPIKA:** Mwenyekiti, kwa sasa ya ndani ni kiasi gani?

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa ya ndani ni takribani shilingi 2,500.

**SPIKA:** Kwa hiyo, ya ndani ni shilingi 2,500 kwa sasa na ya nje kwa sasa ni kiasi gani?

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa sikumbuki vizuri, lakini kwenye taarifa ipo. Pia, tofauti yake ilikuwa ndogo sana kati ya ya ndani na ya nje, kwa sasa hivi ndiyo kuna tofauti kubwa. Hapakuwa na tofauti kubwa sana kwa sasa kati ya ndani na ya nje. Hata hivyo, kwenye taarifa yetu tumeonesha bei ya sasa na bei tunayoipendekeza.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Sanga. Taarifa ilikuwa imetolewa na Mheshimiwa Katani, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naipokea na ninajua utanilindia dakika zangu.

**SPIKA:** Hizi nilizokuwa naongea na Mwenyekiti, hizo usiwe na wasiwasi.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, sawa. Mheshimiwa Waziri ninakuomba, kwanza wafanyabiashara walioko nje suala kama hili hawakujiandaa nalo kwamba, kuanzia mwaka wa fedha tarehe 1, kuna mabadiliko ya kikodi kama hayo. Sasa linapokuja badiliko la asilimia 100 wengi watashindwa kuukomboa mzigo. Tutarudi kwenye hoja ya vitende na kontena zitaharibika pale.

Mheshimiwa Spika, ni vema muda mwingine Serikali ikatoa nafasi kwamba, watu wanaoagiza kuanzia mwezi fulani *at least* ndani ya mwezi mmoja ujao ndiyo mkafanya hilo jambo, lakini *at least* mkafanya kama ambavyo kamati inavyozungumza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ni Mheshimiwa Mnzava pale nyuma.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hivi huyu si amekwishapewa taarifa tatu au hazijafika? Hazijafika ee, haya Mheshimiwa Mnzava.

Samahani kuna Waheshimiwa Mnzava wawili humu Bungeni. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nimpe Taarifa mzungumzaji. Pamoja na mchango wake mzuri ninasisitiza zaidi kwenye ushuru wa *ethanol* inayoagizwa kwa sababu, kwa matumizi ya *ethanol* tuliyonayo sasa hivi kwenye nchi yetu kwa takwimu na taarifa za wadau, viwanda vya ndani vinazalisha kwa asilimia 30 tu, asilimia zaidi ya 70 zinatoka nje. Kwa hiyo, bado tunaihitaji sana kwa sababu, asilimia kubwa ya *ethanol* tunayoitumia inatoka nje kwa sababu, ya uwezo wa viwanda vyetu vya ndani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ninamuunga mkono kabisa wakili msomi Mheshimiwa Mnzava kwa hili analolizungumza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ninakuomba kwamba, hili jambo uliangalie kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Spika, ninaondoka kwenye hiyo hoja kwa sababu, ina taarifa nyingi sana, ninaenda kwenye hoja ya sukari. Kwanza naipongeza Serikali kwa mabadiliko ambayo inakwenda kuyafanya ya kwamba, *NFRA* sasa wanachukua jukumu la kuagiza sukari.

Mheshimiwa Spika, kwenye *Finance Bill* hapa wanazungumza kipengele cha mawakala. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ninakupongeza kwa sababu, mawakala wa sukari wamekuwa ni changamoto kwenye nchi yetu. Mathalani, kuna wakala mmoja anaongoza mikoa 11 yeye peke yake, sasa kwenye mabadiliko ya Sheria yalete kuwepo na mawakala wa sukari katika mikoa tofauti tofauti, ili kurahisisha Watanzania kupata sukari. Vilevile, hili pia,

linatusaidia sana kwenye ku-*control* bei ya sukari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakupongeza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikupongeze sana kwa haya ambayo mnakwenda kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, pili. Kumfanya *NFRA* kuwa ni muagizaji na mnunuzi wa sukari na kuipeleka kuwa ni sehemu ya usalama ni jambo zuri kwenye Taifa letu, ili tuondokane na mkanganyiko ambao umekuwa ukijitokeza.

Mheshimiwa Spika, pia, hii isitafsiriwe kwamba, Serikali inawabana wafanyabiashara. Wafanyabiashara hawa wana *space* ya kutosha kwa sababu, uzalishaji wa sukari nchini bado haujajitosheleza. Kwa hiyo, kwanza wao waongeze juhudi ya kuzalisha sukari. Pili Serikali imekuwa ikiwaunga mkono na kwa kusamehe kodi. Serikali imesamehe kodi kwenye viwanda hivi zaidi ya shilingi bilioni 200, maana yake ni Serikali inaunga mkono kwenye suala la uwekezaji nchini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ninakupongeza kwa hili jambo ambalo umekwenda kulifanya pamoja na Waziri wa Kilimo, ili kuhakikisha kwamba, tunailinda sukari yetu, tunawalinda Watanzania na tunalinda usalama wa chakula cha Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *wharfage* kwenye bandari. Mheshimiwa Waziri nakupongeza, *wharfage* mmeifanyia haki kwa sababu, watu wa bandari wana lengo zuri la kuendeleza bandari zetu. Hata hivyo, changamoto kubwa ilikuwa ni kwamba, fedha nyingi zilikuwa zinakusanywa na *TRA*. Mathalani, watu wa Bandari wamewaomba ninyi zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa zaidi ya miezi sita, hiyo hela ya kuwapa hamna. Vilevile, kitendo cha wao kukusanya fedha kinawasaidia watu wa bandari kufanya shughuli zao za maendeleo ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa ofisi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili suala la *wharfage* kukusanywa na bandari wenyewe linakwenda kutusaidia sana kuhakikisha kwamba, wenzetu wanaifanya kazi hiyo ya kukusanya fedha kwenye miradi ya kimaendeleo. Na isitafsiriwe kwamba bandari ni Dar es salaam tu, tuna Bandari ya Tanga, Mtwara na Bagamoyo; hizi

bandari zote ni lazima ziendelezwe na zitaendelezwa pale ambapo Serikali itakuwa imewaruhusu hawa watu wa Bandari *(TPA)* kukusanya tozo ya *wharfage* wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ukiliangalia suala la *wharfage* ni kwamba, wenzetu kwa mwezi wana uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 50 na ikawasaidia kwenye maendeleo yao. Pia, wana mkopo kutoka *World Bank* wa zaidi ya dola bilioni 345 na wana kazi ya kuulipa huo mkopo ambapo kupitia *wharfage* hizi wataweza kulipa.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono mabadiliko haya na ninamuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, na niungane na Kamati kwamba, suala la *ethanol* aliangalie kwa ukaribu sana kwa sababu, limebeba ajira za vijana wa Kitanzania, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niwe miongoni mwa wachangiaji kwa siku ya leo. Mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa hiyo, naomba niipongeze sana Serikali kumekuwa na *engagement* ya kutosha. Vile vile, ni vizuri pia, tujielekeze kama ni kanuni tuone wapi tutaboresha, ili Kamati ya Bajeti ipate muda zaidi wa kushauriana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida kuna baadhi ya mambo tulikubaliana na Serikali wakasema kwamba, wangeleta majibu. Hata hivyo, kwa jinsi muda ulivyokuwa hatukuwa na uhakika labda katika hiyo *schedule of amendment* yale ambayo tulikuwa tumekubaliana kimsingi kwa sisi kamati tumepeleka *matrix* na Serikali wakakubali ku-*maintain* hiyo *status,* ili yale tuliyokubaliana isiwe habari ya kuja kubadilika wakati mwingine.

Mheshimiwa Spika, maana wamekubali kwenye Bango Kitita, kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri alivyoisoma haioneshi kama

yale tuliyokubaliana wanayachukua. Naamini bado tuna fursa na tukitoka hapa tutakuwa na fursa ya kuhakikisha kwamba, tuna *align* yale mambo tuliyokuwa tumekubaliana kimsingi. Nadhani hilo litakuwa limekaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo naomba nichangie machache. Kwanza ni katika Sura ya 439 ya Sheria ya Bajeti ambayo kimsingi inakwena kuanzisha Mfuko wa Dharura *(Contingency)*.

Mheshimiwa Spika, kwanza hili ni takwa la kikatiba. Katiba inatutaka kama Taifa tuwe na mfuko huu na uwe na fedha. Sasa kwa siku za nyuma mfuko huu ulikuwepo, lakini haukuwa na fedha. Sasa kwa Sheria hii fedha inakwenda kuwekwa na itatumika, kwa ajili ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaweka sawa, tunapoongelea miundombinu hatulengi barabara peke yake ni pamoja na miundombinu mingine. Kwa hiyo, ni vizuri mfuko huu ukapanuka na ukatizama masuala mengine yote ambayo ni ya dharura, ili kama Taifa tuwe na sehemu ambayo tuna hakika kwamba, likitokea janga kabla ya kumkimbilia jirani, sisi kama Taifa, tuwe na fedha zetu ambazo tunazo tayari. Pia, zitakuwa zinachangiwa mwaka hadi mwaka na kitafika kipindi tutakuwa na fedha za kutosha kama Taifa. Kwa hiyo, hili naomba niipongeze kwa dhati Serikali kwa kuhakikisha kwamba, jambo hili linakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni Sheria ya Udhibiti Uingiza wa Bidhaa, Sura ya 276. Ninaipongeza Serikali tumekubaliana kwamba, katika hali ya kawaida ni lazima tulinde viwanda vyetu vya ndani. Tunavilindaje?

Mheshimiwa Spika, ni pale ambapo tunahakikisha zile bidhaa zote ambazo zinapatikana na tunajitosheleza ndani ya Taifa letu. Hatuna sababu ya kutoa mianya zikaingizwa bidhaa ambazo kwanza ni *substandard,* lakini pia, wanakuwa wameweka *subside* kwao. Kwa hiyo, kwetu sisi inakuwa kama *dumping*.

Mheshimiwa Spika, uko mfano mmoja. Sisi kama Taifa, Tanzania, tuna *clinker* ya kutosha na kuweza kupeleka nje ya nchi. Ukienda katika Kiwanda cha Dangote wana uzalishaji mkubwa wa *clinker* ambayo inatoa ajira kwa Watanzania *transporters* na vijana wanajiajiri. Kwa hiyo, hakuna sababu ya sisi kama Taifa kuacha kulinda hizi mali zetu tulizonazo halafu tukaruhusu *clinker* kutoka nje ya nchi South Africa, Saudia, zinakuja ku-*flood market* kiasi kwamba, viwanda vyetu vinakosa kutumia malighafi ambayo inatoa mnyororo mkubwa kwenye ajira.

Mheshimiwa Spika, pia siyo kwa Dangote peke yake, hata kile Kiwanda cha Twiga, Dar es salaam, iko *clinker* ya kutosha na hata ukienda huko Makanya, maeneo chungunzima ndani ya Tanzania tunayo *clinker* ya kutosha. Kwa hiyo, tulinde viwanda vyetu kwa wivu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niunganishe hili pamoja na Viwanda vya Serikali. Uko uwekezaji ambao umefanywa na Serikali kuanzia Mwaka 2020 baada ya Sheria ya kuhakikisha kwamba, inapotokea *gap sugar* viwanda ambavyo vinazalisha ndani vipewe nafasi ya kwanza katika kuagiza. Sasa kuna marekebisho ambayo yameletwa na Serikali, ili kama kuna mapungufu yaliyokuwapo tuyarekebishe, lakini bado tuhakikishe kwamba, baada ya miaka miwili au mitatu sisi tuwe *net exporter* wa sukari badala ya kuwa *net importer* wa sukari.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Uganda walikuwa na tatizo kama hili, wamefanikiwa na leo Uganda wana sukari nyingi zaidi kuliko matumizi yao. Kwa hiyo, tukiwa na sera ni vizuri tuilinde na tuhakikishe kwamba, uwekezaji unafanyika kwa sababu, watakuwa na uhakika kwamba, hicho ambacho kinazalishwa kitatumika kwanza kabla hatujaenda kwa majirani.

Mheshimiwa Spika, pia, ni vizuri kwamba, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, sisi kama kamati tulipopata fursa ya kuwasikiliza wakulima wa Miwa Kilombero wana *AMCOS* zaidi ya 17 na wana wakulima zaidi ya 10,000. Ule mnyororo wao wanavyoufanya na

wao ni washiriki mpaka kilo ya mwisho ya sukari inapokwenda kuuzwa. Kwa hiyo, wananufaika na ni vizuri jambo kama hili likapelekwa kwenye viwanda vingine, ili *out growers* wawe ni wanufaika katika mnyororo mzima wa sukari.

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la *wharfage* ambalo amepongeza Mheshimiwa Sanga, katika hiki kilichofanyika ni jambo jema. Siyo vizuri katika zile taasisi ambazo zinatakiwa zijiendeshwe kibiashara tukazichukulia sawa na taasisi ambazo zinatoa huduma za kawaida. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, tutakuwa tunajidanganya kama taasisi yetu kama *TANAPA*, Ngorongoro, tutataka ziendeshwe kwa kutumia *OC* ambayo hata wakati mwingine haifiki kwa wakati ndiyo maana tunapata vilio kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengi. Inafikia kipindi kuna wanyama wavamizi, wamekwenda, lakini hawana *OC*, wanaendaje ku-*rescue situation* kama hiyo?

Mheshimiwa Spika, naendelea kuiomba Serikali, kama ambavyo wamefanya uamuzi kwa Bandari, kwa siku za usoni wahakikishe na hizi Taasisi za Ngorongoro na *TANAPA* nao wanawezeshwa, ili waweze kufanya kazi zao za kimsingi kutokana na mapato ambayo wanayakusanya. Kubwa zaidi ni kuwe na *governance* ya kuhakikisha kwamba, kunakuwa na matumizi sahihi katika kile ambacho kinakusanywa kwa sababu, kama Taifa tuna uhitaji mkubwa sana wa fedha kwa hiyo, ni vizuri mambo haya tukayazingatia.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara, Sura ya 220, ambayo Serikali ilikuwa imependekeza kwamba, itoze shilingi 382 kwenye gesi asilia, ili ikawe chanzo cha mapato. Nashukuru Serikali mmeelewa kwamba, kwa kipindi hiki tulichonacho ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba, tunahimiza matumizi makubwa ya gesi asilia. Kwa sababu, gesi asilia tunapoinunua Tanzania hatutumii pesa za kigeni, tunatumia shilingi yetu. ni vizuri tuhakikishe kwamba, maeneo ya kuweza kujazia gesi yanakuwa mengi na hamasa ya kutosha, ili Watanzania wengi

tunufaike na rasilimali hii ambayo Mwenyezi Mungu hakukosea kuhakikisha Tanzania tunaipata.

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Dar es salaam wale vijana ambao wanaendesha Bolt na UBA wana-*convert* magari karibu yote kwenda kutumia gesi asilia. Sasa hiki ambacho kilikuwa kinawekwa na Serikali ilikuwa ni kama kuanza kurudi nyuma. Napongeza usikivu wa Serikali, tujipe *space* na tuhakikishe kwamba, Serikali wakati mnanunua magari nunueni ambayo ni *Hybrid* ambayo yanatumia mafuta na kwa kiasi kikubwa yanatumia gesi ambayo tunayo. Hatuhitaji *Forex,* kwa ajili ya kununua gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, naamini tukipata fursa tu-*engage* Serikali, ili Sheria hii ikawe ni Sheria bora ambayo inakwenda kuwasaidia Watanzania walio wengi. Baada ya Kusema hayo naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda kwa hivyo, tutaendelea tutakaporejea tena. Pia tutakaporejea Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao ni Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma, Mheshimiwa Nusrat Shaban Hanje, Mheshimiwa Mohammed Said Issa na Mheshimiwa Condesta Sichalwe.

Waheshimiwa Wabunge, michango inaendelea lakini wakati hayo yanaendelea ni muhimu upande wa Serikali wakapata nafasi ya kufafanua. Hata hivyo, hili la *NFRA* nafikiri pengine sijui kama kifungu kilisomwa hivihivi kilivyo, sijajua hofu inatoka wapi ikiwa *NFRA* kwa hapa kifungu kinavyosoma kinasema *"to cover sugar gap"* maana yake kukiwa hakuna *gap* sukari haitaagizwa. Pia, kama hivyo ndivyo kwanza hata kama hii *gap* ipo na sukari ipo hapa nchini na viwanda vinayo si *NFRA* itachukua kwao? Maana yake sokoni kutakuwa na *gap,* lakini wao wanayo. Kwa sababu mimi sielewi malalamiko yanatoka wapi wakati kama Sheria inasema *"to*

*cover sugar gap"* hii changamoto ya kwamba, viwanda vyetu vitarudishwa nyuma inatoka wapi?

Kwa hivyo, maana yake ni viwanda vyetu vikiweza kuzalisha ya kutosheleza itakuwa imetutosha, lakini tutavitaka tena vizalishe ya kuzidi, ili iuzwe nje. Pia, ya kuzidi, ili *NFRA* ikae nayo nyingine, ili inapotokea changamoto tuwe sukari.

Sasa hiki kifungu sijui kama ni tafsiri ama kimekuwa kigumu. Vilevile, hili suala la *ethanol* ambalo limezungumzwa hapa, Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kufafanua, lakini na lenyewe maelezo aliyoyasoma Mheshimiwa Waziri nilikuwa nayatafuta humu kwenye Muswada. Hapa ni kama vile hii *ethanol* inayoongezewa hiki kiasi cha fedha ni ile ya pombe. Maana hapa tumeambiwa *ethanol* ina matumizi mengine. Sasa maana yake ni yale matumizi mengine hayatakuwemo kwenye hii 5000 wala 7000. Sasa nimesema hivi kwa sababu, wengine watachangia mchana kwa hivyo, ni muhimu sana kuvitazama hivi vifungu, ili tuelewe kama Bunge, changamoto iko wapi wakati tunafanya maamuzi baadaye.

Ndiyo maana mwanzoni niliomba ufafanuzi kutoka kwa Mwenyekiti. Mwenyekiti hili pia, tunaomba ulitazame kwa sababu, jioni tutaingia kwenye zoezi la kutunga Sheria. Kama bado changamoto ipo baada ya kutenganisha kwamba, hii ni kwa ajili ya pombe na hii ni kwa ajili ya kitu kingine, je, bado changamoto ipo? Ili kama haipo Bunge liweze kwenda kwenye maamuzi tukiwa wote tuna uelewa unaofanana.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa sasa ni hayo, mengine tutaendelea nayo baadaye. Hata hivyo, hapa kuna wageni ambao wameingia hapa Bungeni baada ya yale matangazo ya awali kuwa yamekwishatolewa. Sasa niwatangaze hawa wageni:-

Kwanza ni wageni ambao tuliwatangaza kumbe hawakupata nafasi ya kuingia hapa ndani. Hawa ni wageni 18 wa Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, ambao ni Wachezaji wa Timu ya Mpira wa kikapu kutoka Mkoani Tabora. Karibuni sana, uzuri wake sijapewa

taarifa hapa kama mmekwishatolewa au bado mnaendelea, lakini nawatakia kila la heri. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 33 wa Mheshimiwa Katani Ahmed Katani ambao ni Makatibu Waenezi wa CCM wa Kata, wakiongozwa na Katibu Mwenezi wa CCM, Wilaya ya Tandahimba, Mkoa wa Mtwara, Ndugu Jafary Mwadili. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya Mafunzo ni wanafunzi 100 pamoja na Walimu tisa kutoka Shule ya Martin Luther ya Jijini Dodoma. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge wengine walikuwa tayari wamekwishatangazwa na hivyo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 7.07 Mchana, Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024**
***(The Finance Bill, 2024)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nianze kwa kusema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa hiyo nimeshiriki katika kupokea maoni ya wadau mbalimbali tokea ambapo tulielekezwa kufanya hivyo na tumeendelea kusikiliza maoni yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali inahitaji mapato kwa sababu majukumu ya Serikali ni mengi sana. Njia pekee ambapo mapato haya yanaweza kupatikana ni kwa njia ya kodi na njia nyingine ambazo zimewekwa. Katika kusikiliza maoni ya wadau nilibaini kwamba Watanzania siyo kwamba hawapendi kulipa kodi wanapenda kulipa kodi kwa sababu wanajua kodi ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo watu wengi walionekana wanapenda ni kwamba kodi hizi ambazo zinapangwa na Serikali na kuletwa hapa Bungeni tuweze kuzipitisha ziwe ni kodi ambazo wanaweza kumudu kuzilipa na vilevile wakishalipa waone kodi zao zinakoelekea nini zinafanya. Katika hili niweze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan huu mtindo wake wa kupeleka fedha kwenye kila jimbo na kila eneo, sasa inaturahisishia sana sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mimi nikienda Kata ya Masasi wamepewa shilingi milioni 583 nikawaambia kodi zenu mnazolipa ndiyo hizi hapa. Kwa hiyo hili jambo tukiendelea kuonesha itakuwa ni rahisi sana kuwahamasisha wananchi kuweza kupenda kulipa kodi, hata usimamizi wa hizi sheria ambazo tunatunga utakuwa mwepesi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningependa sana niisihi Serikali yangu iendelee kupeleka fedha hizi kwenye maeneo ambayo wananchi wataziona zinakokwenda itakuwa rahisi sana kwa sisi Wabunge kuhamasisha kupenda kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, vilevile hata ile mifumo inayotumika katika kusimamia hizi sheria ambazo tunazipitisha iwe ni mifumo ambayo ni

rahisi yaani kodi ilipike kirahisi tutumie zaidi mifumo ikiwezekana kuepusha kabisa kukutana kati ya mlipa kodi na mtoza kodi itakuwa nzuri sana. Vilevile baadhi ya maeneo ya sheria ambazo tunaweka kama kuna kosa fulani la ukwepaji kodi au vile vifungu ambavyo ni vya adhabu, ile adhabu isiwe kubwa kiasi cha kumshawishi yule mlipa kodi ambaye amekiuka sheria aweze ku-*negotiate* na Afisa anayehusika na kukusanya kodi. Kwa hiyo tuweke viwango ambavyo havitamsukuma mlipaji wa faini kwenda kujadiliana na mkusanya kodi tutapoteza mapato mengi yataingia kwenye mifuko binafsi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nipongeze sana Serikali kwa kuendelea kusisitiza huu Mfumo wa *Cashless*. Yaani kufanya malipo kwa kutumia mifumo hii nayo ni hatua nzuri sana ila niombe tu na hizi *EFD machines* ambazo zinatumika kwa ajili ya kutolea risiti zipatikane kirahisi ikiwezekana zitolewe bure. Serikali itafute kwa sababu ukitaka kupata mapato lazima uwekeze kama Serikali. Kama hizi mashine zitakuwa zinasumbua, kwa hiyo watu wengi wataendelea kufanya biashara bila kutoa hizi risiti za *EFD machines* hasa wafanyabiashara wadogo wadogo ambao ndio wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeanzisha Mfumo wa *NeST;* unataka kila kitu kiende kimifumo hii ni hatua nzuri sana lakini sasa turudi tuangalie na upatikanaji wa hizi mashine za *EFD* na tuendelee kutoa elimu ya kodi ikiwezekana kuanzia shule za msingi, sekondari na kwenye vyuo vyetu. Tuwafundishe Watanzania kuwa wazalendo wapende kulipa kodi na wajue kwamba kulipa kodi ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yetu. Tukifanya haya kwa kweli mambo yatakuwa mepesi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile jambo lingine lazima tuendelee kutunga hizi sheria na kuwa na sera ambazo kodi tunazozikusanya kuwe na namna kwamba hao walipaji nao waweze kutengenezewa mazingira ya kukua zaidi. Kwa mfano tulivyotunga Sheria ya Manunuzi na kusema kiwango fulani cha mikataba ya kazi lazima wapewe wazawa maana yake huu ni mkakati mzuri kwamba tunakusanya kodi lakini tunawawezesha na wale wanaolipa kodi

kupata mapato zaidi huu mfumo ni mzuri zaidi. Hata ile mikopo ya vijana kwenye halmashauri itawasaidia hawa kwenda kukuza biashara ili Serikali inavyoenda kusimamia sheria hii iweze kupata mapato kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nikijielekeza kwenye Ibara ya 45 ya Muswada wetu inazungumzia kurejesha 20% ya makusanyo yanayotokana na Kodi ya Pango la Ardhi kwenye Halmashauri. Hii ni hatua muhimu sana ni hatua nzuri itakwenda kushirikisha Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Serikali za Mitaa Watendaji wa Kata na viongozi wote wa ngazi ile katika kusimamia hizi sheria. Wataenda kukusanya kodi kwa nguvu zao zote na kwa moyo kwa sababu wakiona nao wanapata mapato. Ila tu niombe namna ilivyoandikwa pale inasema lengo la kurejesha hiyo 20% ni kwenda kuwezesha makusanyo ya kodi. Sasa uandishi ule na neno lililotumika pale ni *shall* maana yake *mandatory* ni sharti la msingi lazima iende hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika. kwa hiyo nilikuwa nashauri tungeifungua kidogo kwa sababu kuna Jiji kama Dodoma, Mwanza na majiji mengine makusanyo yao ni makubwa sana yanaweza kwenda kusaidia kulipa fidia na kuongeza miradi mingine ya kupanga na kupima ardhi zaidi ili wazalishe walipakodi wengi zaidi Serikali ipate mapato. Kwa hiyo nilikuwa naishawishi Serikali pale wasiweke tu kwamba kazi ya hii 20% ni kwenda kuwezesha makusanyo ya kodi kwa sababu ukiandika hivyo wale wataenda kujali *stationeries* kwa ajili ya ku-*print notice* na vitu vidogovidogo hawatafikiria kulipa fidia maeneo zaidi. Bahati nzuri nilivyoisoma tu hivi nikamtumia ushauri Waziri wa Ardhi naamini atakuwa amefanyia kazi kupitia simu yake ya mkononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kule kwenye kodi ya majengo na kwenyewe tuweke kodi ambazo wananchi wataweza kuzilipa, kwa sababu unavyosema unawarudishia wakurugenzi 20% watakwenda kufanya hii kwa moyo wote ila sasa vile viwango visiende kuwa viwango ambavyo vitaenda kuleta kelele, vitaanza kuwashawishi wengine kukwepa na malalamiko. Tufanye uthamini,

nilishasema hapa vyuo vya ardhi vinaweza kwa kutumia teknolojia ya *GIS* wakaenda wakachukua nyumba zote wakaingiza kwenye mifumo wakafanya uthamini taarifa zote zikawa pale. Kwa hiyo ukifanya tu *mouse click* unapata taarifa na unaweza kujua ni kiwango gani mwananchi huyu anapaswa alipe na kila mmoja atalipa kulingana na uwezo wake. Kwa mtindo huu tutapata makusanyo mengi usimamizi wa sheria utakuwa mwepesi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko pia Ibara nyingine ambazo zimelenga kwenda kukusanya mapato kwa ajili ya Mfuko wa Dharura. Nchi yoyote kuwa na fedha kwa ajili ya dharura iwapo litatokea jambo lolote ambalo huwezi kuliona sasa ukawana mahali pa kwenda kuchukua fedha na kurekebisha. Tumeshuhudia kwamba mwaka huu tumepata changamoto kwenye barabara zetu nyingi sana. Kwa hiyo kwa kukosa fedha za dharura imekuwa changamoto kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache kati ya mengi niliyokuwa nayo nitamke kwamba naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote niipongeze Serikali kwa Muswada huu na nitamke kwamba nimeunga mkono hoja hii lakini ningependa kutoa maboresho mawili matatu; la kwanza natambua juhudi ya Serikali ya kuwashirikisha wadau kuanzia kwenye *tax taskforce* hadi kufikia upande wa Kamati ya Bajeti wadau wamekuwa wakienda.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu sisemi una kasoro lakini una changamoto kidogo. Wadau wanapofika mbele ya *taskforce* wao wanapeleka maoni yao, wanapeleka maoni nini wanataka na nini

wanaiomba Serikali iweze kufikiria. Wanapokwenda mbele ya Kamati wakati huo yawezekana ni mapema kabla hata ya *Finance Bill* haijaanza kuchapishwa, wanasikiliza maoni ya Mheshimiwa Waziri wakati wakitoa bajeti *speech*. Sasa kipindi cha *Finance Bill* kutolewa, majadiliano na kuwasikiliza wadau nakiona kama ni kipindi kifupi sana na yawezekana kabisa hata majadiliano na Serikali; kati ya Serikali na wadau, Serikali na Kamati ni muda mchache sana watu wanakimbizana.

Mheshimiwa Spika, tumeona Kamati mara imetoka saa nne, mara imefanya nini, wamekimbizana sana. *Finance Bill* ni chombo kimoja kizito sana cha kutimiza matakwa ya Serikali kuweza kutafuta fedha kuweza ku-*finance* mipango yake kwa kipindi kile cha mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine wanatoa *Finance Bill* mwezi mmoja kabla ya mipango ya Serikali katika sehemu tofauti tofauti za kodi. Uganda nafikiri mwezi wa nne au wa tatu wanatoa, Kenya mwezi wa tano walitoa sisi kwa nini tusubiri mpaka Mheshimiwa Waziri asome hotuba yake na baada ya kuisoma *week before even less a week before* ndiyo *Finance Bill* iweze kutolewa?

Mheshimiwa Spika, mimi sioni kama tunaisaidia sana Serikali katika jambo kama hili na pengine hatulisaidii Bunge kuweza kupata muda wa kutosha kuweza kujadili vitu kama hivi. Ndiyo maana kuna wakati mwingine tunaweza tukatunga sheria wanaita *out of forgetfulness* kwenye taratibu za kisheria jambo liko Mahakamani linajadiliwa na linashindaniwa lakini bado Bunge huku tunaambiwa tutunge sheria kwenye jambo hilo, huku tukijua Kanuni za Mabunge lakini vilevile Kanuni za Kimahakama haziruhusu jambo ambalo linapelekwa Mahakamani likajadiliwe mahali pengine au likatungiwe sheria mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo nilikuwa ninataka nigusie kwenye *paragraph* 29 ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri juu ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148 na pale kwenye Ibara ya 93 Mheshimiwa Waziri anapendekeza kurekebisha Kifungu

cha 2 cha Sheria hiyo ya Sura ya 148 kwenye misamiati. Ameweka misamiati mingi sana lakini moja ya misamiati ni msamiati unaosema '*Gaming supply.*' Msamiati huu unashindaniwa katika shauri ambalo limefunguliwa Mahakamani kuna kesi shauri la pili namba 121 ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, sasa na jambo likiwa liko Mahakamani na halijapata ufumbuzi wa Mahakama ama halijaamuliwa. Wewe ni Mwanasheria na unajua kuna hii *concept* ya *less sub-judice* na kwa hali hiyo jambo hili linakatazwa kuzungumzwa ama kuamuliwa mahali pengine. Nilikuwa nashauri mambo kama haya yapate muda wa kutosha ili Serikali iweze ikaelezwa na ninayo taarifa kwamba jambo hili walielezwa Kamati lakini sijui matokeo yake yatakuwa namna gani. Hivyo nilikuwa najaribu kuzungumza kwamba kuwepo na muda mzuri wa kufanya majadiliano kama kuna jambo ambalo linaonekana halifai kuweza kujadiliwa na Bunge liweze likafahamu ili Bunge hili lisiingiliane na mihimili mingine na tukaleta mtafaruku.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, naam.

**SPIKA:** Hebu nielezee vizuri. Hilo lililoko Mahakamani ni kifungu gani?

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, kuna shauri; kifungu ambacho ninakizungumzia… Ngoja niangalie maana yake nilikuwa nakisoma hapa. Ni Mheshimiwa Waziri anafanya marekebisho katika Ibara ya maelezo yake, *paragraph* ya 29 na Ibara ambayo anataka kufanya marekebisho ni Ibara ya 93 kuhusiana na neno (msamiati) linaloitwa *gamming supply* ni hilo.

**SPIKA:** Haya nimeshaipata.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Sasa kesi iliyoko Mahakamani inahusu nini?

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, inahusu tafsiri ya neno *gamming supply* na kama itakupendeza naweza nikakutumia kwenye simu hiyo *statement of appeal*.

**SPIKA:** *Statement* ya nini?

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ni *statement* ya *appeal* yaani ni shauri ambalo limefunguliwa.

**SPIKA:** Haya sasa hapa mbele sishiki simu, hebu mpe msaidizi kwanza hiyo uliyonayo halafu ndiyo nijue kama…

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, mimi kwanza nimalize kwa kuunga mkono hoja nikae halafu ili niweze kumfungulia aje kuichukua, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nitakapoletewa tutaliweka sawa hili jambo ili isije ikaonekana kwamba kuna jambo la ziada linafanyika hapa.

Haya, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye hii *Finance Bill* iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu, changamoto kubwa tulizonazo kwa sasa ni pamoja na upatikanaji wa dola. Upatikanaji wa dola unatusumbua na ndiyo unasababisha mfumuko wa bei na vitu vingi kupanda. Kwa hiyo, sisi kama Wabunge kazi yetu kila tunapokuwepo, moja jukumu letu ni kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa nakumbuka hata juzi wakati nachangia kwenye Wizara ya Fedha nilisema kwamba kati ya eneo lingine linaloweza kutusaidia kupunguza mahitaji ya dola ni matumizi ya gesi. Nikasema ukichukua Mkoa wa Dar es Salaam, ukachukua Mkoa wa Lindi na ukachukua na Mtwara mahitaji yao ya mafuta ya magari yanalingana *almost* na mahitaji ya nchi nzima, kwa maana ya mikoa iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, sasa nikashauri nikasema kitendo cha Serikali kuweka 382, yaani kuongeza kodi maana yake na vituo tulivyonavyo (*gas station)* vitatu ni ku-*demoralize* watu ku-*convert* magari yatumie gesi, lakini nikasema hebu kwanza Serikali iiondoe hiyo. Vile vifaa vinavyotumika kwenye ku-*compute* gesi *to power*, gari dogo ni shilingi milioni mbili, siyo chini ya hapo na gari kubwa, kwa mfano mpaka sasa hivi *diesel* hawajaleta vifaa kwa sababu ya gharama ambapo gharama zake zinaenda karibu shilingi milioni nne.

Mheshimiwa Spika, sasa nikasema hebu hivyo vifaa vyote viondolewe kodi na tuone namna ya kurahisisha masharti, watu wengi wajenge vituo vya gesi, matokeo yake nusu ya fedha ambazo tungetumia kutafuta dola ili tuweze kununua *diesel* na *petrol* tunaweza kutumia gesi ambayo tunanunua kwa shilingi lakini sijaona Serikali imesema nini kuhusiana na hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili umeuliza hapa kabla haujaahirisha Bunge mchana, ukawa unashangaa kidogo kwamba hivi hii *NFRA* mbona hujaona tatizo, maana kazi yao wao ni kuagiza tu ile *sugar gap,* kwa maana ya ile sukari itakayopungua hiyo ndiyo kazi yao. Sasa nataka niulize labda Serikali inisaidie kufahamu, kwamba sasa hivi hivi tunavyozungumza viwanda vyetu vyote viko kwenye *operation* na wanazo sukari sasa kwenye stoo na wanauza, na bei ya viwandani wanauza kati ya shilingi 125,000 kwa mfuko wa kilo 50. Bei ya sukari iliyokuja *(imported sugar)* ambayo haina kodi wanauza kwa shilingi 115,000, sasa swali langu ni kwamba, leo hivi tunavyozungumza Waziri mwenyewe alikubali kwamba tani 70,000 hazijafika bandarini, ziko njiani zinakuja, lakini wakati huo tuna

tahadhari kama tani 200 hivi, tunazosema wakati wowote tukitaka tunaweza kuingiza, sasa hapo ndipo inapokuja kwamba, hivi sasa hivi tunapoleta tani 70,000 na wakati bei ya *NFRA* ni shilingi 115,000 na wakati bei ya viwandani ni shilingi 125,000 ni *obvious* kwamba watauza.

Mheshimiwa Spika, kwa nini hizi bei za viwandani 125,000, ni kwa sababu moja tu, wao wana kodi ya *VAT* ambayo wakiiondoa ikawa sawasawa na hii ya hawa ma-*importer* walioingiza bila kodi maana yake sukari yao itashuka mpaka shilingi 102,000. Kwa hiyo, sasa ukiangalia leo kwamba zote zikiwa hazina kodi, hawa watakuwa na shilingi 102,000 na hawa watakuwa na shilingi 115,000 sasa sijui nani mwenye gharama nafuu hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala langu, tatizo lililopo ni kwamba hatuna uhakika na hicho ambacho Serikali inakisema kwamba leo dhumuni la kuiweka *NFRA* ni kwa ajili ya kuziba *gap,* kwa sababu wakiamua wanaleta sukari kwa kiasi wanachotaka na ndiyo maana sisi wengine tukaangalia kwamba ile sheria iliyokuwepo ikisimamiwa na inajieleza vizuri wala kulikuwa hakuna haja ya kutafuta chombo kingine cha kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi sote tunafahamu, *NFRA* mahindi yenyewe ya wakulima yanawashinda kununua, sasa leo unatoka hapo tunasema *NFRA* watanunua hiyo *sugar gap* wataleta, watatunza halafu watasimamia *distribution,* hayo maghala yenyewe watakayotunza watayatoa wapi? Leo kwa bahati mbaya sana niseme…

**SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, ili tuende vizuri, hapo umesema kifungu hicho namna kilivyo, Serikali inaweza ikaagiza sukari kiasi chochote inachotaka. Si itakuwa umevunja hicho kifungu tunachotunga sasa hivi, ikiagiza kiasi chochote inachotaka badala ya *gap?*

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Umesema vizuri sana, ndiyo maana nasema hivi, yaani leo

tunavyozungumza sasa ambapo viwanda vyote vipo kwenye *operation,* kuna tani 70,000 Waziri alisema iko barabarani inakuja. Sasa hizo tani 70,000 zinazokuja maana yake ni kwamba, ndiyo maana matokeo yake sasa bei ya hao ma-*importer* waliopewa ni shilingi 115,000 na bei ya viwanda ni shilingi 125,000. Ukiondoa kodi watarudi kwenye shilingi 102,000, ndiyo bei yao. Kwa hiyo, leo viwanda tunavikaba koo kwa sababu vinatulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema kwamba kama huu utaratibu tumeupuuza, tafsiri yake ni kwamba, hata hiki tunachokifanya bado tutakipuuza, na nikaendelea kusema…

**SPIKA:** Ngoja, muda wako unalindwa usiwe na wasiwasi. Nataka kuelewa kwa sababu mwishowe tutatakiwa kufanya maamuzi hapa. Nataka kuelewa kwa sheria iliyopo sasa ambayo inataka huyu mwenye kiwanda ndiyo aagize sukari, ile sukari akiagiza huyu mwenye kiwanda yeye analipa kodi?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, iko hivi, wale wenye viwanda kikubwa wanachokifanya ni kwamba wanaagiza kiwango kile ambacho hakipo.

**SPIKA:** Ngoja, sheria yetu tunayotaka kutunga inasema ataagiza nini huyu *NFRA*?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, huyo mwenye kiwanda hata yeye akileta kwa sheria yetu ni kwamba wote hawalipi kodi.

**SPIKA:** Haya, endelea na mchango wako.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninachotaka kusema ni kwamba kati ya *crisis* moja ambayo tunaisubiri, maana wakati mwingine sisi tumezoea tu kufanya kazi kwa zimamoto, leo kwa sababu hawa wenye viwanda ambao kwanza na sisi kwa kudhani kwetu kwamba fedha walizo nazo ni zao, kwa taarifa yenu *investor* yeyote yule mkubwa utakuta

amekopa tena kwenye benki zetu za *local,* kwa hiyo fedha alizonazo ni zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo leo na wao wana mawili wanaweza kufanya, yawezekana nao tukiendelea hivi wakashindwa kupunguza bei na wakashindwa kuuza sukari. Kwa hiyo, matokeo yake wakishindwa kuuza maana yake tutarudi kulekule na tutafika mahala tena inawezekana na penyewe tukataka kuandamana kama ambavyo matatizo yamekuwa yakifanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niseme tu kwamba Serikali yetu inahitaji kuwa sikivu hata pale mahala ambapo tunadhani tumekosea tuweze kujirekebisha. Leo unapozungumza hata kama siyo *NFRA,* ukiangalia ile Bodi ya Sukari haya majukumu yote tunayoipa *NFRA* bodi ya sukari wangeweza kufanya, kwa sababu kazi yao kubwa walipaswa kufanya kazi ya kuratibu na kuangalia nani anaweza kuleta sukari, muda ukifika wanatangaza akaleta.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ni jambo ambalo nalisema kwa sababu najua kesho na keshokutwa litakuja kutusumbua na nayasema haya kwa ushahidi. Nakumbuka kipindi kilichopita nilikuwa kwenye Kamati ya Nishati na Madini, lilipokuja suala la *TANOIL* kununua mafuta nilisimama kidete nikaendelea kubisha nikawaambia jamani hizi fedha tunaingiza kwenye shimo lakini Serikali haikutaka kusikia mpaka mahala tulipofikia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, leo unakuta kazi kubwa ambayo tumeifanya ya kuvijenga viwanda ambavyo tumetoka mbali, tunafika mahala tunataka kuwa na *excess sugar* kwa ajili ya *export* halafu na sisi tunaanza kusema vinginevyo ambavyo kesho na keshokutwa inawezekana tukaingia matatizoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilidhani kwamba nitoe hayo kama maoni yangu ili kesho na keshokutwa tuweze kuulizana, kwa sababu hii nchi ni yetu na sisi sote ni Watanzania. Sisi kama Wabunge mojawapo ya jukumu letu kubwa ni kuishauri Serikali. Sasa

pale ambapo Serikali inafuata ushauri wetu ni sawa. Mimi nafika mahala najiuliza hivi hakuna utaratibu wa kuwa tunapitia ule ushauri tunaoipa Serikali inapofika mahala kwamba imekaidi na imekaidi maksudi tukawa na utaratibu fulani wa kuwa-*punish* ili hali kama hizo zisiendelee kujitokeza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, maana tofauti na hapo Serikali itakuwa kila siku inaendeleo kula hasara hata mahala ambapo tungeweza ku-*save*. Kwa hiyo, nilidhani kwamba na mimi nitoe mchango wangu kwa namna hiyo, *otherwise* kwenye maeneo mengine yote yako sawa, lakini kwenye lile suala la dhahabu, leo miaka michache tu iliyopita tulipambana sana na tulifurahi kuona tumepata *gold refinery* pale Mwanza na pale Geita, sasa leo zile *gold refinery* zimegeuka kuwa *white elephant,* huku tukijua kwamba zile *gold refinery* endapo zitafanya kazi tafsiri yake ni kwamba zita-*add value* kwenye dhahabu yetu, zikisha *add value* kwenye dhahabu yetu maana yake ni kwamba, ni rahisi sasa tukapata hizo *foreign currency* zaidi zikatusaidia ku-*solve* baadhi ya matatizo yetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo hakuna mtu anazungumzia kuhusiana na *gold refinery* na ilikuwa ni Serikali hii ndiyo iliyofurahia na ikaona *gold refinery* ni mkombozi kwa nchi yetu. Sasa haya yote ni mambo ambayo tunahitaji tuyaone na tuone namna ya kuisaidia nchi yetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mathayo Manyinyi mimi nataka kuelewa, kwa hiyo nisaidie kuelewa jambo hili. Hii Bodi uliyoitaja hapo na kwamba ndiyo inayopaswa kufanya hii kazi, hii changamoto tuliyoipitia hivi karibuni, hii Bodi ipo ama haijateuliwa?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, Bodi ya Sukari ipo.

**SPIKA:** Mbona tulipata changamoto kubwa sana, ilitokea nini?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, mengine ni stori ndefu lakini Bodi ya Sukari ipo na inafanyakazi. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mimi nataka kujifunza kwa sababu ndiyo nitasimamia kupitisha hii sheria hapa na sitaki baadae hayo unayoyasema unatabiri kule mbele yaje yanikute njiani, ndiyo maana nataka kujifunza. Bodi ipo na inafanya kazi?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, bodi ipo na inafanyakazi. Kwa hali halisi *sugar gap* hii ilikuwa *created* kwa sababu vibali vya kununua sukari vilitoka Januari, *gap sugar* ilikuwepo toka mwezi Novemba.

**SPIKA:** Vibali vilitoka Januari na Bodi ikiwepo?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, *yes.*

**SPIKA:** Haya ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwenye Muswada wa sheria hii muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye kwa zaidi ya miezi mitatu ametujalia afya njema na uzima tukifanya kazi walizotutuma Watanzania na sasa tunaelekea mwishoni. Tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jambo hilo lakini tunakushukuru na wewe na wasaidizi wako kwa mwongozo mzuri wa kuongoza na kuendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kama muda utaruhusu nitakuwa na mchango kwenye maeneo matatu. Eneo la kwanza ni sehemu ya 11 ya Muswada ambayo inazungumzia marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi. Wakati nasoma muswada kwenye eneo hili nikaangalia nikashtuka kidogo, sikushtuka sana baada ya kusoma taarifa ya Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya Bajeti ukurasa wa 23 kuna jambo linashtua kidogo. Moja ya jambo ambalo Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imebaini, taarifa inasema naomba ninukuu: "Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba, Serikali haina utaratibu wa kufanya tathmini ya matokeo ya hatua za kikodi zinazochukuliwa kila mwaka ili kuangalia endapo zina manufaa hasi au chanya".

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimesema hivyo? Mwaka uliopita au mwaka jana Juni tulifanya marekebisho kupitia Sheria ya Fedha, tukaongeza Kifungu cha 33(A) kwenye Sheria ya Ardhi ili kufanya makusanyo yanayokusanywa kama Kodi ya Ardhi *(Land Rent)* yaende kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwenye Muswada tulionao sasa tumefanya maboresho tena kwenye Kifungu hicho cha 33(A) tunaongeza maneno, "ili kusaidia asilimia 20 ya makusanyo yanayotokana na kodi ya ardhi yarudi kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya kwenda kusaidia shughuli za ukusanyaji wa mapato".

Mheshimiwa Spika, nashawishika kuamini inawezekana Serikalini kuna matatizo kidogo. Baada ya kupitisha Sheria ya Fedha mwaka jana, Wizara Fedha ilitoa Waraka Namba 1 wa Mwaka 2024; waraka ule ulipotoka dhumuni lake kubwa ilikuwa ni kuhamisha majukumu ya ukusanyaji wa kodi ya ardhi kutoka Wizara ya Ardhi kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, mkononi kwangu nina takwimu za ukusanyaji wa kodi ya ardhi kwa miaka tisa nyuma. Kipindi chote hicho kodi ya ardhi haijawahi kukusanywa chini ya 59%. Baada ya waraka huo wa mwaka jana kutolewa kwa mara ya kwanza kodi ya ardhi ilikusanwa kwa 44.4% ya lengo lililowekwa. Sababu kubwa

ilikuwa ni nini? Waraka huu ulileta mkanganyiko, kwamba sasa nani anakwenda kukusanya hii kodi ya ardhi kati Wizara ya Ardhi na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali yenyewe ndiyo iliamua kuwaondoa Maafisa Ardhi Halmashauri kuwaweka chini ya Wizara. Ziko Halmashauri mapaka leo ukifika *treatment* ya Maafisa Ardhi ni tofauti na Wakuu wa Idara wengine wa Halmashauri, kwa sababu wanawaona siyo sehemu ya watumishi wa halmashauri.

Mheshimiwa Spika, leo tunasema tumekuwa kliniki ya muda mrefu kwamba watu wanakusanya kodi ya ardhi lakini hawana uwezeshwaji, wawezeshwe. Badala ya ku-*solve* tatizo tunashukuru nia inaonekana kwamba mna nia ya ku-*solve* tatizo kurudisha 20%, lakini bado lazima tutegue hiki kitendawili, ni nani mwenye jukumu la kukusanya kodi ya ardhi kwenye nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma sheria kifungu cha 25 na cha 33 cha Sheria ya Ardhi, ukusanyaji wa kodi ya ardhi *(land rent)* siyo *property tax* ni jukumu la Wizara ya Ardhi. Siyo hivyo tu, ulipaji wa kodi ya ardhi ni miongoni mwa masharti ya umilikishwaji wa ardhi, ambapo hata mtu asipolipa kodi anakuwa na sifa za kufutiwa umiliki wa ardhi aliyokuwa nayo. Pia, mifumo ya kutambua wamiliki wa ardhi, mifumo ya TEHAMA imeunganishwa na kazi nyingine za kisekta chini ya Wizara ya Ardhi, kama kazi za upimaji, upangaji na uthamini, mfumo huu ni mmoja na mifumo ya TEHAMA inayotumika ni ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali kama lengo letu ni kweli kuongeza mapato na kufanya kazi hii ifanyike vizuri, kwa sababu kwenye sheria hatukugusa chochote kuhusu nani akakusanye na bado sheria iko wazi, Wizara ya Fedha rudini mkafute waraka wenu Namba 1 wa mwaka jana na wapeni Wizara ya Ardhi kazi ya kukusanya kodi ya ardhi ili nchi yetu iendelee kupata mapato kutoka kwenye ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ninalotaka kuchangia ni kwenye upande wa sekta ya maliasili na utalii. Kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 tulifanya marekebisho kwenye maeneo matatu kwenye sekta ya maliasili na utalii. Tulifanya marekebisho kwenye Sheria ya Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, tulifanya marekebisho kwenye Sheria ya Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)*, tunalifanya marekebisho kwenye amri ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* pia tukaenda ku-*reflect* marekebisho hayo kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, lengo likiwa ni kuiruhusu *TRA* kukusanya mapato kutoka kwenye taasisi hizi za uhifadhi chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, wakati wa bajeti za kisekta, tukiwa kwenye Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Serikali ililiambia Bunge kwamba wamekubaliana Serikalini unaletwa utaratibu kwamba taasisi za uhifadhi za *TANAPA* na Ngorongoro zikusanye mapato na kutumia zenyewe. Zitapeleka Serikalini gawio na kodi na michango kwenye ile mifuko mingine. Ilipokuja Bajeti Kuu na kwenye Muswada huu wa Sheria ya Fedha jambo hili halionekani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ulikuwa una faida zake, moja ya faida ambayo tulikuwa tunataka kuiona ni kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinakuwa na fedha kwa ajili ya kufanya kazi kibiashara. Wakipata changamoto wanazitatua kwa wakati lakini pia kwa utaratibu huu tulikuwa tunahuisha mifuko tuliyokuwa nayo kama Mfuko wa Wanyamapori na Mfuko wa Maendeleo ya Utalii *(Tourism Development Levy)*.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao Serikali imeamua kwenda nao sasa, kupitia Bajeti Kuu na Muswada huu wa Sheria ya Fedha jambo hilo haliwezekani tena. Naiomba Serikali kama tumeona hatuwezi natamani tungerudisha huo utaratibu wa kuwaachia wakusanye, kutumia na kupeleka mapato (gawio na kodi) Serikalini, hiyo ni *option* ya kwanza. Kama *option* hiyo haiwezekani tuweke utaratibu wa kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinapata fedha muda wote ili wakipata changamoto, haiwekani tuambiane ukweli nchi ya kwetu sote, Mama amefanya kazi kubwa sana kwenye utalii, *Royal*

*Tour* imeleta majibu na matokeo makubwa sana, hatuwezi kutangaza utalii wa nchi hii kwa kutegemea *OC,* haipo! Hatutatoka na hatutafika. Fanyeni utafiti wenzetu nchi nyingine wanafanyaje, Rwanda wamefanyaje na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutangaza utalii ni gharama, huwezi ukatangaza utalii kwa kutumia *OC*, huwezi kukarabati miundombinu ya hifadhi ikitokea dharura kwa kutumia *OC*. Niiombe Serikali, kama hatuwezi kuurudisha utaratibu huu basi mtuambie kwa wazi mtatuwekea utaratibu gani ili taasisi zetu hizi ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa na matokeo yaonekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita Serikali ilituahidi kwamba watajitahidi hata kwenye hii *OC* angalau watakuwa wanapeleka *OC* ya miezi miwili au mitatu kabla. Kuna wakati jambo hilo limeshindikana, taasisi zetu zimepata dharura kwenye hifadhi zetu, kwenye mapori yetu, na watendaji wetu na askari wetu wamepata mazingira magumu ya kufanya kazi kwa sababu hakukuwa na fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niiombe sana Serikali tumekwishapitisha bajeti, tutapitisha Muswada huu, wakaweke utaratibu mzuri, taasisi hizi ni za kwao, nchi hii ya kwetu sote, tunataka tuone matokeo, tutoke hapa tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nataka kulichangia, niishukuru Serikali, nimeona kusudio na mapendekezo ya kufuta kodi kwa vile viwanda vya chai ambavyo vimepata hasara kwa miaka mitatu mfululizo. Sekta ya chai imepitia changamoto nyingi sana, ni wakati sasa wa kuangalia, hakuna shida kama tutasamehe na *VAT* pia kwenye chai inayochakatwa humu ndani ya nchi yetu ili kufanya soko la chai liendelee kukua, faida ipatikane na ili wakulima wetu wapate mapato mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye marekebisho haya ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaipongeza Wizara ya Madini kwa kuleta Muswada humu ndani kwa ajili ya *BoT* kuweza kuruhusiwa sasa kwenda sokoni kununua dhahabu. Tumekuwa tukichangia kwa muda mrefu kuwaomba Serikali, kwamba badala ya kutunza pesa tutunze dhahabu.

Mheshimiwa Spika, ninayo maombi, nilikuwa kwenye hiyo Kamati na nipo mpaka leo; kwa kweli tulifurahia sana tulivyojengewa *refinery* ile ya Mwanza na ya Geita, na mpaka Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alikwenda pale. Hata hivyo kutokana na changamoto za biashara kiukweli tulichokuwa tunakitarajia sicho. Kwa sisi watu wa Geita kile kiwanda cha Mama Masasi tulitegemea kukusanya *CSR* nyingi sana pale; lakini sasa kutokana na changamoto za biashara limekuwa jengo la kulala popo tu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu, kwa sababu *BoT* wanaruhusiwa kuanza kununua dhahabu, niwaombe dhahabu yao kwa ajili ya kufanyiwa *refinery* ipite kwenye hizo *refinery* za Geita, hasa kwa Geita ambayo tunazalisha dhahabu nyingi, ili na sisi tuweze kukusanya na kumsaidia yule Mtanzania. Serikali itakapoonekana inafanya biashara na yule Mtanzania tunaweza kuvuta na watu wengine wakamuamini na wakaendelea kufanya naye biashara.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu sukari. Tunaipongeza sana Wizara kwa kuleta mabadiliko ya sheria kwenye eneo hili la sukari. Kwa wale Wabunge tunaotoka vijijini tangu tumeanza mjadala huu wa sukari Bunge letu limepata heshima kubwa sana

kwa sababu matatizo yote yanayotokea kuhusu sukari lawama kubwa inaangukia Serikali wala haimuangukii mtu mwingine. Sasa, niiombe Wizara isikatishwe tamaa, najua hii ni vita, kupambana na mabepari siyo kazi ndogo. Tutapigiana makelele humu ndani lakini hatimaye Watanzania hawataki kusikia matatizo ya sukari, wanataka kuona Serikali inachukua nafasi yake kuhusiana na suala la sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye hili; Mheshimiwa Waziri ikimpendeza, mimi ninafanya biashara, sijawahi kuona, yaani bodi ya sukari uliyokuwa unaiongelea hapa imejaa wafanyabiashara wale wale wanaotusumbua humu ndani. Sasa huku unakaa kwenye bodi halafu huku wewe uko kiwandani, nimwombe Mheshimiwa Waziri, avunje bodi na aweke watu wa kumshauri vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawezi kuwa na mtu anayeisumbua Serikali kwenye bodi, hii haiwezekani. Watamsikiliza huku wanamkwamisha upande wa pili. Weka pembeni, weka watu wazuri wenye taaluma, wenye nia nzuri waishauri *NFRA* iweze kuagiza sukari na tusipate tena matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upole ninachangia suala la *ethanol*. Mchana nilimsikia anauliza kwamba Wabunge wengi tumezungumzia *spirit* inayotoka nje, kwamba imewekwa shilingi 7,000 na ya ndani shilingi 5,000. *Spirit* ya nje na ya ndani zilikuwa hazina ushuru. *Spirit* ya ndani ilikuwa inalipwa *VAT* ya shilingi 10,800,000 kwa kontena la *40/20 feets* na *spirit* ya nje shilingi 10,800,000, bei moja. Sasa, kwa Tanzania hapa ni viwanda viwili tu ambavyo vinazalisha *spirit* kwa asilimia 20. Kiwanda cha kwanza Kilombero, kiwanda cha pili *TPC*, Moshi. Ukichanganya na gongo na hiyo michuzi ya korosho, hata tukiiruhusu, ndiyo utapata asilimia 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni lazima tujiulize, tumeshawa-*engage* watu viwanda zaidi ya mia mbili na kitu Watanzania wameweka hela zao, wamekopa. Haya, mtu anasimama anasema tutumie *spirit*

ya gongo na mihogo. Mpaka ukapata hiyo teknolojia ya kutengeneza gongo, yenyewe bado ni haramu, hivyo ni mpaka tuje tubadilishe sheria ndipo tuje kutengeneza *spirit* kwenye viwanda. Ninaomba tuache mizaha kwenye masuala ya muhimu.

Mheshimiwa Spika, *spirit* ukiangalia ilivyowekwa mimi nachelea kusema kuna mchezo umechezwa na watu wenye viwanda vikubwa ili kuwaondoa hawa vijana ambao wameanza. Hawa tunaowatetea humu ndani hawafiki hata 70. Hivi kweli wataalam waliingia mtaani kuona kwamba tukiwawekea vijana hawa wakiondoka turudi tena kutegemea wale wakubwa? Tunakwenda kutengeneza *cartel* nyingine kama ya sukari.

Mheshimiwa Spika, hawa vijana tunaowaongelea humu ndani hakuna anayeagiza zaidi ya kontena mbili, tatu. Kontena lilikuwa linauzwa, yaani gharama ya kulisafirisha mpaka hapa ni shilingi milioni 72, ukiweka na kodi ya shilingi milioni 10.8 unapata kama shilingi milioni 73. Vijana wanauza shilingi milioni 88, wanapata hela kidogo, sasa unamuongezea kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kama tutaruhusu hili liende, na Mheshimiwa atusikilize vizuri; maana yake ni kwmaba, *ethanol* ya ndani tu kontena lenye ujazo wa lita 25,000, ikienda kwa hiyo shilingi 5,000, kutoka shilingi milioni 10.8 umeweka kodi ya shilingi milioni 125. Ukijumlisha na *VAT* ni shilingi milioni 138. Kutoka shilingi milioni 60 kwa kontena la ndani, ukiweka na shilingi milioni 10.8 ni shilingi milioni 70.8 itakuwa takriban shilingi milioni 200. Hii itakuwa ni ongezeko la asilimia 600. Hizi ni hesabu za dizaini gani? Kwanini mimi kichwa changu Musukuma nisiamini kuwa hawa walioandaa hili suala wamezungukwa na kampuni kubwa ili waondoe vijana wafanye kazi watu wenye kampuni kubwa. Hii ni vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukileta *spirit* hapa unalipa *VAT*. Ukimuuzia yule mzalishaji yeye anaenda kulipa ile *excise duty* baada ya kuuza kwa mlaji, amekwishatengeneza anauza. Unamuwekea maskini wa kontena moja kwamba kabla hajauza alipe shilingi milioni 200, huu ni uchumi wa dizaini gani? Kwanini mnataka kuturudisha kwenye

mateso? Kumbukeni hawa vijana wameajiri watu na wao wenyewe wameajiri wamewakimbia kwenye *portal*; maana maombi sasa hivi ukitangaza kazi *portal* imejaa dakika kumi. Wamekimbilia kwenye kujiajiri, unakwenda unamrundikia kodi. Hata yale mapendekezo ya Kamati, ninaiomba Kamati na Bunge tuiache *spirit* kwa sababu ni *raw material* ibaki kwa kodi ya zamani kwa sababu hakuna tunachopoteza. Hii shilingi 10,000 unayoitaka kwa hawa vijana unaipata moja kwa moja kwa wale wazalishaji. Wanapomaliza kutengeneza wakiuza wanalipa ile ile shilingi 10,000. Kwa sababu lita moja inalipwa kama shilingi 3,900 baada ya kutengenezwa. Lita moja inachanganywa na maji lita mbili, analipa zaidi ya shilingi 10,000 na kitu. Kwanini tunakwenda kuwarundikia hawa vijana ikaja kusababisha tuwaondoe kwenye *game*? Kwa hiyo niombe sana, kwa kweli tufanye biashara tuwaache vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Unajua watu waliotoka madarasani halafu hawajafanya biashara kidogo hawaelewi. Yaani mtu mpaka kuja kusimama kuanza kuzalisha ameshafilisika hata zaidi ya mara tatu, haanzi na kupata. Kafanya utafiti yeye, ameona biashara inakubali, ameenda ku-*engage financial statement* kwenye benki, benki zinatoa mikopo, ghafla leo tumepiga *u-turn* kuwarundikia kodi ili waondoke kwenye biashara. Makontena zaidi ya 100 ya vijana yako kwenye maji. Mtu ana kontena tatu, badala ya kulipa shilingi milioni 20 unaambiwa ulipe shilingi milioni 400; utazitoaje? Tunarudia makosa yale yale ya vitenge. Vitenge vinaingizwa Tanzania na vinapelekwa Tunduma. Kwa sababu ya kodi tulizoweka halafu zinarudi kwa baiskeli, zimejaa Kariakoo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nakuomba sana, Serikali ya Mama Samia ni Sikivu, na wewe mwenyewe Spika wetu, na wenzetu upande wa mawaziri, upande wa Serikali. Kwa kweli hatuna tunachokipoteza kwa kuiacha kodi iliyokuwepo kuendelea kuchaji *VAT* halafu hii kodi ikadaiwe kwa mlaji wa mwisho baada ya mzalisaji kuuza, na hatupotezi hata shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, hizo hesabu zilizopigwa kwa kweli tuna imani kwamba baada ya kuongea maneno mengi sana sisi

Wabunge, tunamwomba Waziri na wataalam wake watusikilize kwa sababu sisi ni wawakilishi. Tunazungumza haya tukiwa na wadogo zetu, tuna watoto na wengine wamo humu wanafanya hizo biashara. Watuache tufanye biashara kwa amani kwa sababu tunalipenda taifa letu, tunalichangia na tunalipa ushuru; na hakuna inayopoteza. Huwezi ukamnyang'anya tajiri ushuru ukaja ukamrundikia maskini. *It means* Serikali haitaki kuzalisha matajiri wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze sana Serikali kwa kusikiliza maoni na mapendekezo ya wadau. Kwanza *actually* wamefanya *public hearing*, wameita wadau kuja kutoa maoni na wadau wamekuja. Pia, wamesikiliza maoni ya Kamati na maoni ya Wabunge. Kwa hiyo, maana yake wamepitia mchakato ambao unatuonyesha utayari wa Serikali kwenye kufanya urekebu wa sheria mbalimbali ambazo zinasaidia utekelezaji wa bajeti hii ambayo Bunge tumeipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo zuri, na hata ukiangalia watu huko nje wamepokea vizuri na ndiyo maana wamekuja kutoa maoni. Na mimi ninapongeza katika hayo ambayo tunayasema na ndiyo maana nilisema kwenye *reforms* unaweza ukaona namna ambavyo kuna mambo ambayo tumeyapigia kelele muda na yamefanyiwa kazi sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitazitaja baadhi ya sheria ambazo zimeletwa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho, na kwa kweli tumekuwa tukizizungumzia muda. Sheria ya Madini, Sura 123 ambayo inataka watu wanaoshughulika na sekta ya madini kuchakata ndani asilimia isiyopungua 20 ya mazao yao yanayotokana na madini ya Tanzania ambayo yatatusaidia kupata malighafi katika *refinery* zetu, viwanda vya kuchakata dhahabu na almasi na madini mengine. Kwa hiyo itatusaidia kubakisha ndani kwa kuwa kuna *trading*, *refining* na *melting* ambayo ni kitu ambacho tumekuwa tunakizungumza.

Mheshimiwa Spika, na mimi nasema hivi kwa sababu ninajua kuna vijana wenzangu wa Tanzania ambao watashiriki katika mnyororo wa thamani na tutaenda vizuri kama nchi, hakuna mtu atakayebakishwa nyuma. Pia ni fursa na vijana wengine waone. Kwa Serikali kuleta marekebisho haya maana yake wanatengenezea vijana wa Tanzania fursa ya kushiriki katika mnyororo wa thamani wa madini, hili nipongeze.

Mheshimiwa Spika, pia wameleta marekebisho katika tasnia ya sukari. Tunarudia tena kusema, katika marekebisho waliyoyafanya wameongeza kipengele ambacho wazalishaji na wasambazaji watatakiwa kutangazwa hadharani, kila mkoa tutajua nani ni *distributor*. Pia, watatangaza gharama za uzalishaji ili wakitutajia bei tulinganishe na gharama walizotumia kuzalisha. Hiki ni kitu kizuri na hakijawahi kutokea na hatuwezi kubeza kitu kama hiki ambacho kinaondoa *monopolization* kwa baadhi ya watu kushika sekta za muhimu, wakatingisha nchi. Kwa hiyo, hiki ninakipongeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili pia niwaombe sana Wizara ya Kilimo na Serikali. Hii ni kama tumeweka koma katika kuzungumza, tunaomba tutafute suluhisho la kudumu la ishu ya sukari. Pia, hii ikawe fundisho katika sekta nyingine na matajiri wengine wa biashara nchini katika zile bidhaa muhimu za Watanzania ili waache kuweka uhodhi kwenye masuala muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusifanye siasa kwenye maisha ya watu kwa sababu hiki unaweza kukiona ni kitu kidogo. Kwa hiyo, ikawe fundisho pia sehemu nyingine. Kama kuna Wizara nyingine ambayo wanaona kuna *monopolization* mahali, walete kwenye Bunge hili. Hii ndiyo tumewaonyesha kwamba Bunge hili lina nguvu na Serikali iko makini, walete tuje turekebishe sheria ili tuondoe uhodhi katika sekta za msingi za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia natoka Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo na Serikali imeweka msamaha wa kodi katika vifaa vya michezo, VAR ambayo inatuonyesha utayari wa Serikali kuelekea kwenye *AFCON 2027*. Hiki kitu pia ni cha kupongeza na hatuwezi kukiacha, kwa sababu tukizungumza tu humu kwamba tunataka kuboresha sekta ya michezo na Wizara ya Michezo na Tanzania tujiandae kuwa pengine na utalii wa michezo kwenye nchi ambazo zinazunguka Tanzania ili nchi nyingine pia ziweze kutumia viwanja vyetu basi viwanja vyetu viwe *packed*. Tukiongea tu hivi hivi bila kuweka kwenye sheria maana yake tunakuwa tunaongea tu lakini tukiona wameleta kama hivi tunaona kwakweli Serikali iko tayari na kwa kweli tunawaunga mkono na ni kitu ambacho ni cha kupongeza.

Mheshimiwa Spika, tarifa zinaonyesha kwamba nchi yetu inapoteza takriban shilingi trilioni 17.4 za kodi kila mwaka kwa sababu kadhaa ambazo zitazitaja. Katika nukta hii, nasema hivi kwa sababu tunapoteza hizi fedha. Unaona hizi sheria zote tumetunga? Tunataka tutafute fedha, mimi naamini kabisa Mheshimiwa Waziri anatafuta namna ya kutafuta fedha ili ahudumie bajeti ndiyo maana unakuta ana-*introduce* kodi hii analeta huku tunajadili tunamuambia hii hapana, hii sawa. Kwa hiyo, na yeye anatafuta namna ya kutafuta fehda. Hakuna mtu anamuonea mwenzie. Kwa sababu tunatafuta fedha na tunasema kuna upotevu wa takriban shilingi trilioni 17.4, kwenye sababu ambazo tunaweza tukazirekebisha. Kwa mfano, tunapoteza fedha katika *illicity financial flows* na pia katika *double taxation*, kutoza kodi mara mbili.

Mheshimiwa Spika, pia tunapoteza fedha katika mifumo ya ukusanyaji wa kodi, ndani. Kwa hiyo tunatunga kodi mpya. Tukiacha kuzuia mianya ya upotevu wa mapato, maana yake tutarudi tena hapa hapa *square one*. Niwaombe sana Wizara, tafadhali rekebisheni mifumo ya ukusanyaji wa kodi ndani ili wakati Watanzania wanajibana kuchangia kodi, kwa sababu ni lazima tulipe kodi; na ukisema hivi unaweza kuwa *very unpopular* kwenye hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba hakuna Serikali inaweza kujiendesha bila kukusanya kodi. Kama watu ni milioni 60, wanaolipa kodi wanaoleweka wako milioni tano tu, halafu hao hao wanaolipa kodi mifumo haiko vizuri, unawavunja nguvu ambao wanakubali kulipa kodi kwa hiari na wengine ambao wanatamani kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Wizara, tutumie teknolojia zote tulizonazo kuzuia upotevu wa mapato ya kikodi. Ninaona kuwa wamefanya marekebisho pia katika masuala ya sheria za ukusanyaji wa kodi na mashauri ya kodi; tunaomba sana, kwa sababu tunapoteza fedha nyingi ambazo zingetusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu pia wameleta marekebisho ya kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148, Ibara 17, Kifungu 51, huduma za *data* mitandaoni, kipengele kimejumuishwa kama sehemu ya kuongeza wigo wa walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, mimi niiombe Wizara kitu kimoja, kweli wametajwa wale *content creators*, watoa maudhui mitandaoni wamewekwa pale kwamba wameongezeka. Ila mimi niwaombe Wizara waende wakaweke kitengo *TRA* cha kufanya tafiti za kikodi. Kwamba ni kodi gani zina manufaa, kodi gani zina mantiki na kodi gani zinaendana na mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Tanzania ni eneo la kibiashara ya kidijitali kwenye kampuni kubwa za kiteknolojia. Kwa mfano, Tanzania ni *market place* ya *digital services* za ulimwengu. Kampuni

kubwa kama *Microsoft*, *Google*, sisi Tanzania tunatumia *search engine* zao, wanapata kutoka kwetu. Takwimu zinaonyesha kuwa tuna Watanzania milioni tisa mpaka sasa hivi wanatumia *Netflix*. Najua mnaijua *Netflix* Waheshimiwa. Ni huduma ambayo unavyolipia unaletewa mrejesho kwamba imepokelewa Netherlands, imepokelewa Amsterdam, sisi tunapata nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe, hiki kitu ninachokiongea ni sehemu mpya ya kupata kodi. Kwa sababu umeanza ku-*introduce* masuala ya *digital services tax*, ninaomba tushiriki kwenye *international tax organizations*, mashirika ya kimataifa ya masuala ya kodi, ili sisi pia tujadili. Hata kama tutakubaliana nao kwamba tutakachokilipa asilimia mbili inabaki Tanzania. Hivi, sisi hadi lini tutaendelea kuwa walaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama una Watanzania milioni tisa, na una uhakika kwamba kila mwezi wanalipia *Netflix* na huduma mbalimbali za kiteknolojia. Tunajua *booking.com*. Waheshimiwa mnajua *booking.com*? Watanzania wanatumia wakiwa kwenye anga la Tanzania. Hata wageni, *non-residents* wanatumia lakini wakiwa kwenye anga la Tanzania, sisi tunapata nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani tupate hizi, na hatuwezi kupata kama hatushiriki katika majadiliano ya kikodi ya kimataifa kwa sababu pia sisi siyo *member*, sisi siyo *member* katika *inclusive framework* ya masuala ya kikodi duniani. Nawaomba pia Waheshimiwa Mawaziri, lakini hata tukienda sehemu ambayo wanajadili *International Tax*, sisi tunapeleka watu wana uwezo kiasi gani ambao wanaweza wakajadili? Yaani kwamba ni *objective* kwenye masuala, wana uwezo kiasi gani? Kwa hiyo, tuangalie hizo ni sehemu mojawapo ambayo sisi, na hii kama *Zone Block* ya Afrika Mashariki, tunaweza tukaenda na msimamo mmoja ama hata kama ni *Block* ya Afrika, tunaweza tukawa na msimamo mmoja. Kwa asababu sisi Afrika ndiyo tunatumia mazao yanayotokana na *Giant Tech Companies* za ulimwengu, sisi ndiyo tupo kwenye mitandao *frequently*, asubuhi, mchana, jioni pamoja na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama nchi tuna-*benefit* nini kwenye hili? Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, tafadhali tusiache hii, tumia *resources* zako, tumia rasilimali zako, tumia Kitengo chako cha Utafiti wa Masuala ya Kikodi, wakuandikie wakuletee. Hii ni vita hata hivyo, hiki kitu ni vita kwa sababu hao ninaokwambia pesa inapokelewa Netherlands na wao wanategemea kama chanzo chao cha mapato. Sasa hatuwezi tukaenda hivihivi, mkiwa mna umoja, hata kama ni *block* ya Afrika, Afrika Mashariki mkaenda pamoja kwamba bwana hii hapa ndiyo hivi, tunataka na sisi tupate hata kama ni *percentage* fulani iingie kwenye nchi. Najua hiki kitu siyo mara ya kwanza kukisikia na nakuomba Mheshimiwa Waziri ukifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, nashukuru wameondoa, na mimi nilileta jedwali la marekebisho kuhusiana na tozo ya asilimia 2 kwa wakulima. Nimefurahi sana Serikali imefanyia kazi, wameondoa kwa sababu hata mimi nilileta jedwali kwa ajili ya kuiondoa kabisa. Sasa, ndiyo maana tunawaambia hivi vitu vingine vidogo vodogo mnaweza mkaachana navyo halafu mka-*deal* na hivyo vitu vingine vikubwa kwa sababu kwanza, mnakuwa mmempunguzia Mtanzania mzigo lakini mnaonesha namna ambavyo mmejipambanua.

Mheshimiwa Spika, tuna Wizara nzima ya masuala ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano lakini tuna Wizara nzima ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa hiyo, hiyo ni sehemu nyingine ambayo itakusaidia kukusanya kodi. Tusiogope kusema hadharani, watu wanatakiwa walipe kodi ila tuwe tu wengi ili tusi-*feel* yale maumivu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatia na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mheshimiwa Mohamed Said Issa ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipata nafasi niweze kuchangia kwenye *Finance Bill* hii.

Mchango wangu utajielekeza kwenye eneo moja tu, eneo la *ethanol*. Kabla sijaanza kuchangia, naomba kununukuu Taarifa na Maoni ya Kamati yetu ambayo yalikuwa yamewasilishwa; kwenye kipengele cha 2:3:3 kinasema hivi "msamaha wa ushuru wa bidhaa zenye *ethanol* inayotambulika kwa *HS Code* 22007, Serikali inapendekeza kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye *ethanol* inayotambulika kwa kodi hiyo. Kwa mtu atakayezalisha na kutumia katika uzalishaji wa nishati ya viwandani, matumizi ya kitabibu au maabara".

Mheshimiwa Spika, narudia, kwa mtu atakayezalisha na kutumia katika uzalishaji wa nishati viwandani, matumizi ya kitabibu na maabara. Vilevile kwa watumiaji wa matumizi mengineyo tofauti na matumizi tajwa, wataendelea kutozwa ushuru wa bidhaa. Naendelea, kwenye kipengele kinachofuata maoni ya Kamati 2:3:4 "ushuru wa bidhaa kwenye *ethanol* yenye kilevi zaidi ya asilimia 80 inayozalishwa ndani ya nchi na itakayoingizwa kutoka nje ya nchi kwa kiwango cha asilimia 5000 ndani na 7000 kwa kutoka nje", maelezo mengine yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, wazazi wangu walishawahi kuniambia kwamba hata kuyasikiliza mawazo ya watu ni darasa tosha pia. Nilipokuja hapa Bungeni nikajifunza kitu kimoja kwamba, nitatamani kusikiliza kila michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wanachangia. Toka tulivyoanza kuchangia kwenye Bajeti za Kisekta na hata Bajeti Kuu, asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge tulikuwa tunaishauri Serikali kwa nini kila bidhaa ambayo nyingine inaweza ikazalishwa hapa ndani ya nchi yetu, tunaaagiza kutoka nje kwa asilimia kubwa? Sababu hiyo nyingine ikaelezwa kwamba ndiyo inasababisha kwamba hata tuwe na upungufu wa dola nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hili naomba niipongeze sana Serikali kwa kusikia maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wakishauri, namna ambavyo wanaishauri Serikali kwamba siyo kila bidhaa tunapaswa kuagiza nje, zingine tunaweza tukazalisha humu humu ndani nchini kwetu. Serikali ikachukua hayo

mawazo, ikayafanyia kazi na ndiyo haya ambayo yameletwa hapa leo.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali imesema haitaweka kodi kwenye *ethanol* ambayo ni ya muhimu, kwa mfano ya kwenye maabara, ya kitabibu, shida iko wapi? *Ethanol* ambayo imeongezewa kodi hapa ni ile ambayo ni zaidi ya asilimia 80 na hata kwenye kamati unaona walikuwa wanasema hivi, Kamati ikabaini kwamba mapendekezo ya Serikali hayajabainisha ni kwa namna gani waagizaji na wazalishaji watakapokuwa wanauza *ethanol* kwa wazalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa kama vile pombe kali. Kwa hiyo, hapa Serikali ilichokuwa imelenga ni kwenye zile baadhi ya bidhaa ambazo ni kama pombe.

Mheshimiwa Spika, sasa tukasema, kama wako baadhi wazalishaji wa viwanda ndani ya nchi yetu ambao wanazalisha *ethanol* hiyohiyo na wakawekewe shilingi 5,000, kuna shida gani kama tuta-*discourage* hawa ambao wanaangiza kutoka nje, tukawapa motisha watu wetu ambao wanaangiza ndani. Ushauri wangu tu katika hili, kwenye ile shilingi 5,000 ambayo wamewawekea wazalishaji wa ndani, naomba wawapunguzie wawafikishie shilingi 3,000, lakini wale ambao wanaagiza kutoka nje, wenyewe wabaki hivyohivyo shilingi 7,000.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii pia kuwaomba vijana wa Kitanzania wenzangu ambao wanafanya biashara ya *ethanol*, kama wanaweza kukopesheka kwenye benki wakafanya hiyo biashara na ikaonekana *demand* ya *ethanol* ambayo ni zaidi ya 80% inahitajika hapa nchini, tunaomba watumie mikopo hiyo hiyo kufungua viwanda hapa nchini, wazalishe ili tuweze kutoa ajira kwa Watanzania wenzetu na wakizalisha, waweze kutoa nje wao ili tuweze kujipatia fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukawa tunaendelea kuhubiri Tanzania ya viwanda kama hata vitu vidogo tu ambavyo vinaweza kuzalishwa hapa nchini tunaviweza. Hawa ambao wamewekewa kodi ya shilingi 5,000 ndiyo haohao wakipunguziwa, ndiyo ambao

watazalisha kwa wingi, wata-*cover* hilo *gap* ambalo hapo panapungua. Lazima tujifunze kuvipenda vitu vya kwetu, *ethanol* inatoka kwenye mazao mengi mengi, mboga za majani zinaweza zikazalisha *ethanol*, matunda yanaweza yakazalisha *ethanol*.

Mheshimiwa Spika, karibu nafaka nyingi ambazo tunazalisha hapa nchini, zinaweza zikazalisha *ethanol* maadamu Serikali haijagusa *ethanol* ya kwenye matibabu na ya kwenye viwanda kama nishati. Mimi naunga mkono hoja, naomba ipunguzwe tu kwa wale ambao wanazalisha ndani ndiyo muwawekee shilingi 3,000 au ikiwezekana muwaachie ileile iliokuwa ya mwanzo, lakini wale ambao wanaagiza nje ya nchi, hata mkiwawekea shilingi 10,000 ni sawa tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana, Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, atafuatia na Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi Ulenge ajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Muswada huu ulio mbele yetu. Awali ya yote, nataka niweke wazi kwamba si-*intend* kuchangia au kuongelea masuala ya sukari kwa sababu ambazo ziko wazi, kwanza mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge inayoshughulika na Kilimo, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, umeshatoa maelekezo mapema kabisa kabla hata sakata hili halijaanza kwamba Kamati yangu ikutane na wawekezaji, wazalishaji na wadau wa Sekta ya Sukari mapema inavyowezekana na sisi tumejipanga kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, kwa nafasi yangu kama Mwenyekiti, nisingependa kuonekana na-*pre-empty*, ningependa niwe *open minded* kuwasikiliza wadau wa sukari, kwa maana hiyo nitachangia maeneo machache mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza napenda kusema, naipongeza sana Serikali kwenye eneo la chai kwamba limeweza sasa kwa kiasi fulani kutoa unafuu wa kodi ambayo ilikuwa inaongeza gharama. Wamefanya kwa mnajiri wa kuona kwamba wanapunguza gharama za uendeshaji na uwekezaji katika Sekta ya Chai.

Mheshimiwa Spika, nadhani tukielewa kwa nini chai ni moja ya zao kubwa la kimkakati katika nchi yeyote inayolima chai, tutaona kuna umuhimu wa kuisaidia na kulisaidia zao la chai zaidi ya hapo ambapo Wizara imepafikia. Nchi zote zinazolima chai haziangalii ku-*focus* kwenye chai itatengeneza kodi kiasi gani, zinaangalia chai ni zao ambalo linazalisha ajira nyingi sana kwenye maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, unapotaka kuondoa umaskini, unatakiwa uangalie mazao kama chai, miwa, kahawa na mengine mengi. Lakini haya mazao yanatofautiana kwa wingi wa watu ambao wanaajiriwa kwenye sekta hizo. Chai ni zao ambalo linaongoza dunia nzima na ukienda kwenye nchi nyingine kama Indonesia ambazo zinazalisha, Bangladesh, wao wameondoa karibu kodi zote kwenye zao la chai wanazipata kodi kwa kutumia tunasema *second level* kwa maana ya kwamba matumizi ya watu watakaopata fedha, watakwenda kununua vitu vingine, kwa hiyo, watakutana na *VAT*, watalipa, watakutana na mambo mengine, watalipa, kwenye chakula, watalipa. Lakini kwenye uzalishaji wa chai kwa kiasi kikubwa hakuna kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana dhima nzima ya bajeti hii na Mpango wa Nchi ni kutengeneza uchumi shindanishi, uchumi ambao utatumia *resources* zetu kutengeneza ajira zaidi ili tuweze kunufaika na kupata kwa kiasi kikubwa kupunguza umaskini kwa watu wetu wa maeneo ya vijijini. Tunaambiwa na wachumi wote, ukitaka kuendeleza nchi, *focus* vilevile kwenye maeneo ya vijijini na hasa kwenye eneo la kilimo. Kwa hiyo, niwaombe sana Kamati yetu ya Bajeti tunaishukuru, iendelee kuangalia maeneo na Serikali iangalie zaidi maeneo gani inaweza ikatoa unafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kamati yetu ya Bajeti imeongelea vilevile suala moja kwamba Serikali imeonesha kwamba haina mpangilio mzuri wa kufanya tathmini ya kikodi kila mwaka kwenye vile viwanda au maeneo ambayo sisi kama nchi tumetoa *duty remission* au *exemption* kwenye baadhi ya *importers* au *importers* wa mazao fulani fulani.,

Mheshimiwa Spika, sasa, jambo hili mimi kidogo limenishtua na ninadhani siyo jambo lenye afya, na Kamati yetu ya Bajeti imetoa *recommendation*, Serikali ianze utaratibu wa tathmini ya matokeo ya hatua inayozichukua pale ambapo inatoa kodi. Je, zinanufaisha? Uchumi wetu?

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru kwa mara ya kwanza tumeona kifungu ambacho wamekileta kwenye Bajeti na kwenye Muswada kinachoongelea kuwa na *performance contract* kwa wale ambao wanapata misamaha ya kodi ili kuona kwamba kama mambo waliyosema yanafanyika, waliyoyaahidi yatafanyika wakapewa *exemption* wanayafanya na wana-*achieve* zile *targets*. Ingawa bado hiyo ni *trick* kwa sababu kuna sababu nyingi sana ambazo mwekezaji anaweza akazisema ambazo zitamuondoa kuwa kwenye *liability,* lakini angalau ni *step* nzuri ya kuanzia kwa hiyo nawapongeza sana Wizara kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo mahususi nataka kuliongelea leo, kwenye haya masuala ya *duty remission*, kuna kiwanda kule Mbeya Songwe ambacho ni moja ya viwanda ambavyo kwa kweli kama nchi na kama tunaongelea uchumi shindanishi ambao utasaidia uchumi wetu na utasaidia kutupa kodi za mbele na utasaidia wakulima wetu, kuna kiwanda ambacho chenyewe kina-*specialize* kwenye ku-*produce item* inaitwa *liquid glucose*.

Mheshimiwa Spika, pengine kwa sababu ambazo Wizara wanazifahamu na *importers* wanazifahamu, watu wengi wameruhusiwa ku-*import liquid glucose* kutoka nje kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kuzalisha vyakula.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema, kwa wakati ambao jambo hili lilifanyika ambao ilikuwa ni mwezi Julai, kwa *GN* ya sasa hivi, na hii kitu inafanyika katika *Custom Management Act*. Kwa hiyo, mwanzo wa mwaka, kama Serikali, kama Wizara tunasema sisi tutaondoa, hatuta-*charge duty* kwenye maeneo haya, hivyo *liquid glucose* na yenyewe imekuwa *included*. Kwa hiyo, kwa siku za nyuma, inawezekana kulikuwa na sababu za msingi kwa nini walifanya kwa sababu ni lazima tupate kodi kwenye viwanda vingine au *products* nyingine ambazo zinatumia hiyo *product*. Sasa, tuna habari njema katika nchi yetu kwamba tuna wawekezaji waliweza kufanikiwa kujenga kiwanda kule Songwe ambacho kina *capacity* kubwa ya kuzalisha *liquid glucose*.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwamba *liquid glucose* Tanzania ina-*import* kwa mwaka *Metric* Tani 8,000. Lakini kiwanda hiki ambacho kipo na kimeanza uzalishaji, kinaweza kuzalisha tani 12,000 kwa hiyo, kuna zidio la karibu tani 4,000 ambazo zinaweza zikawa *re-exported*. Sasa, hoja ni hii, kiwanda hiki kimewekwa katika mazingira ambayo hayako sawasawa kwenye ushindani wa soko.

Mheshimiwa Spika, lakini cha pili ambacho ni kibaya zaidi, kiwanda hiki kina *impact* kubwa sana kwenye wazalishaji wa mazao ya mahindi. Kiwanda hiki kwa mwaka kita-*consume* mahindi zaidi ya 40,000 na gharama ya kutumia mahindi hayo itakuwa karibu shilingi 25,000,000,000 kwa mwaka, hiyo ni kabla ya kodi ambazo pengine watazilipa kwa kutumia wafanyakazi, kitaajiri watu karibu 300.

Mheshimiwa Spika, sasa, katika hali kama hii, tumeshakuwa na kiwanda, kinaweza kikafanya kazi na kinaweza kikazuia *importation* tuka-*save foreign currency*. Kuna kila haja ya Serikali na Wizara kuchukua hatua za haraka sana kufanya utaratibu ili sasa wale *importers* ni zaidi ya 12, wana-*import* kutoka nje, hawana sababu ya kwenda kununua hizo *products* hapa zenye ubora ambazo wanazinunua kwa bei nafuu zaidi iliyosababishwa na *duty remission* ya *10 percent* ambayo wao, wenzetu *locally* wanalipa *10 percent*, wao wanao-*import product* hiyo hiyo, wanalipa sifuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nchi, kama tuna-*walk the talk*, ni wakati sasa kuchukua hizo hatua. Nimeangalia *GN* ya *East African Community Custom Management Act* ya 2004, kwa kila mwaka hii *GN* inaisha mwezi Julai, kwa hiyo, mwezi Julai tarehe 15, hiyo *GN* inakwisha. Ni mategemeo yangu sasa kwamba kwa mwaka huu, Serikali haita-*renew* hiyo *GN*, tutasema na sisi tuna kiwanda, tunaweza ku-*export*, tunaweza ku-*fulfil local demand*, hatuna sababu ya kuendelea kutoa *duty remission* kwa wazalishaji wa *liquid glucose*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kwenye hilo, katika *East Africa* na *Sub-Saharan*, hicho ni moja ya kiwanda pekee kilichopo. Wenzetu hata nchi za Jirani kama Kenya, wana-*import glucose* kutoka China na kutoka Egypt. Kwa hiyo, Tanzania tumekuwa kwenye nafasi nzuri, tuna *competitive advantage* kwenye hii *product* moja kubwa ambayo inasaidia wakulima lakini inasaidia kodi za Serikali, lakini inasaidia ajira, lakini kuna *multiplier effect* kubwa sana kwa kiwanda hiki kufanya kazi kwa watu wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali, Wizara iliangalie jambo hili kwa umakini na niseme, wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, tayari wameshaliona hilo na walishawaandikia Wizara ya Fedha kwa barua ya tarehe 11 Juni, 2021. Lakini siyo wao tu, *TIC* na wenyewe wameliona hili, wamewaandikia Wizara ya Fedha tarehe 3 Mei, 2024 kwamba kuna hili jambo, kuna hiki kiwanda, sasa ni wakati wa kuzuia *duty remission* kwa makampuni haya yanayoingiza *glucose* toka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mohamed Said Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Mheshimiwa Juma Hamad Omar ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Fedha *(Finance Bill)*. Mimi michango yangu leo itakuwa ni midogo tu, nitaanza na suala la sukari, jambo hili napenda sana kuipongeza Serikali kwa kuleta Sheria hii. Kwa mtu yeyote ambaye alikuwepo Tanzania miezi sita iliyopita, lazima akubaliane na hoja hii. Kwa nini nasema hivyo? Ni ile shida ambayo waliipata Watanzania katika upatikanaji wa sukari.

Mheshimiwa Spika, tungekosa soda, usingesikia chochote hapa, tungekosa maji, usingesikia hapa, lakini tumekosa sukari, kelele nchi nzima zilikuwa kubwa, maana yake ni nini? Bidhaa hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuingizwa katika *National Food Reserve Agency (NFRA)* ni jambo la lazima na siyo *option* kwa sababu, jambo hili tusingeliingiza humu maana yake siku yoyote likitokea tena tunaweza kuona hata Serikali inaanguka. Kwa hiyo, mimi naipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo ninapenda kuchangia kwa kutoa mapendekezo. Jambo la kwanza ni suala la *costs of production;* mimi naona kwamba, hii bidhaa ya sukari mpaka sasa hivi bado haijatutendea haki Watanzania. Kwa nini nasema hivyo? Kwa nini sukari tunayoagiza kutoka nje, kwanza kule tunanunua halafu kuna *logistics* nyingi, hapa tuna *freight, insurance, duties* zote na tukifika hapa bei ambayo tunauziwa ni sawa na ile ambayo inazalishwa hapa, kwa nini sasa?

Mheshimiwa Spika, kule inakozalishwa *formula* za kuzalisha ni zile zile, viwanda vya kisasa tunavyo, kama *Bagamoyo Sugar* tunaoneshwa kwenye *TV* kila siku, yaani ni cha kisasa kabisa. Kwa nini sasa kule tunanunua sukari ya Brazil au Italy, lakini pamoja na gharama zote hizo ikifika hapa tuna uwezo wa kununua kwa bei nzuri na wananchi wakaridhika?

Mheshimiwa Spika, sasa mimi napendekeza kwamba, suala hili, viwanda hivi, vipewe *formula* maalumu ya kutuletea *costs analysis* zao kwenye Serikali yetu, ili kuweza kujua *price* ambayo watauziwa wananchi, ili tuweze ku-*benefit.* Ukienda kwenye nchi za jirani hapo unaweza kukuta sukari ni shilingi elfu moja mia tano tu, sisi tunafika eti Serikali inapendekeza shilingi elfu mbili mia sita, ambayo kule nje unaweza kuinunua kwa shilingi elfu moja mia tano, ambayo uzalishaji *procedure* ni zile zile au kuna kiini macho? Kwa hiyo, mimi napendekeza *costs analysis* iwepo na sisi sukari ishuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili. Kuna Ibara ya 76, Kifungu cha 11 kinachozungumzia kwamba, kuwepo na *agencies* kila Mkoa. Kwenye Kifungu hiki mimi nilipendekeza kwamba, iongezwe kwenye majiji yale makubwa ya kibiashara kama vile Dar es salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha wawepo *agents* zaidi ya mmoja. Kwa sababu, yale ni majiji yanahitaji huduma kubwa siyo kupeleka *agent* mmoja mmoja, hapo ninapendekeza iongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jingine ni suala la Wizara zetu hizi mbili. Tunapokuwa na *sugar gap* ni lazima kuwe na mashauriano ya hali ya juu kati ya Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo, ili kuona kwamba, kile kinachokwenda kufanyika ni sahihi. Siyo kwamba, Wizara ya Kilimo iamue kwa sababu, tumepeleka *NFRA* hapana, kuwe na mchakato mzuri ambao mwisho utafikia kwamba, itapewa ruhusa. Kwamba, sasa kuna *sugar gap,* kulingana na yale mazingira ambayo yameonekana pamoja na ripoti za wenye viwanda, ili kuweza kuona kwamba, viwanda hivi vimetendewa haki na hawakuchukua tu mchakato wa kubumba.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni suala la viwanda vyetu hivi. Ni bora kuwepo na kipengele kwamba, kila miezi minne vitoe ripoti ya *production,* ili Serikali ifahamu mapema kama kutakuwa na *sugar gap*. Kwa sababu, wakichelewa kutoa taarifa inawezekana hata hiyo *NFRA* ikaja kufeli na hatutegemi ije ifeli. Hapa tunajua sheria hii hairuhusu *NFRA* kuagiza tu bila *gap* kwa hiyo, jambo hili ni muhimu kutoa taarifa mapema, ili Serikali iweze kuchukua wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye mchango wangu wa pili, kwenye suala la faini. Kwanza mimi naipongeza Serikali kwenye *angle* moja, kutusikiliza sisi Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi. Sisi watu 393 hatuongei tu hapa Bungeni kwa matashi yetu binafsi, sisi tunawakilisha wananchi, wanatupa mawazo yao, ndiyo maana tuna kuja hapa tunasema.

Mheshimiwa Spika, ingawa mengine tunayasema, kama sisi, lakini ni kwa kuiangalia jamii. Kwa hiyo, tunaipongeza Wizara ya Fedha kwa kuondoa Muswada ule na kushusha faini ya juu shilingi milioni nne na faini ya chini shilingi milioni moja na nusu. Sasa hapa, mimi napendekeza suala la faini si suala ambalo kwanza lilitakiwa liingie kwenye vichwa vya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, suala la faini ni baada ya kutenda kosa, sasa kwa nini hawa *TRA* wanawasababishia wafanyabiashara watende kosa? Ninamaanisha ninavyosema hivyo, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa nikisafiri na Wabunge wengi humu huwa wanasafiri, nimeishakwenda nchi zaidi ya thelathini au zaidi. Sijawahi kukutana na kadhia ya kudaiwa risiti, tuseme wale hawakusanyi kodi? Bila shaka wanayo *formula* ya ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi napendekeza wenzetu hawa, Wizara ya Fedha, waende wakasome, wakajifunze kwenye nchi kama hizi ambazo ukienda kule huulizwi risiti. Tena cha ziada zaidi ni kwamba, unaponunua bidhaa, unapotoka pale *border,* yaani *airport,* unapeleka zile risiti wanaangalia kodi uliyolipa kule ndani, unarejeshewa, wana *comfort* ya juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hapa kwetu eti unadaiwa ni lazima uwe na risiti. Hebu twende Dubai pale, twende Indonesia, kila sehemu hata wenzetu majirani zetu Zambia hapo. Ukienda Zimbabwe uchumi wao upo chini, lakini hakuna jambo kama hilo. Jambo hili linawanyong'onyesha Watanzania na lina wafanya

wasiwe na *comfort* ya kufanya biashara na tena tumezungumza hapa kwamba, wafanyabiashara tunaowatoza kodi ni wale wa hali ya kati ambao wanahangaika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Musukuma pale, mfanyabiashara yule anaweza kufilisika. Hata mara tano anakopa anarudi, mara kachukua Kahama, mara kaingia mlango huu, sasa kwa nini hatuwafikirii watu kama hawa? Tuje na *formula* ambayo tutakusanya kodi zetu kubwa, kubwa kabisa, jambo hili halikubaliki.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe Mheshimiwa Mohamed, kama alivyosema ni kweli amezunguka nchi nyingi, lakini kwa wenzetu kule kile unachokinunua imekuwa ni desturi kwao hauwezi ukaondoka kama hawaja-*punch* risiti na wakupe, wewe uichukue uitupe nje, lakini ni lazima wakupe risiti. *So definitely* wao, labda useme tuendelee kuelimisha Watanzania, wawe na desturi kila mtu anaponunua kitu lazima atoe risiti na wasiwe na *room* ya *negotiations* kwamba, ukinunua kwa kiasi fulani nitakupunguzia sitakupa risiti.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa hiyo siipokei kwa sababu, haina afya na ninaweza kueleza ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kule kwa wenzetu kwa mfano, nimetaja nchi kama Dubai hapa. Wao wanajua wenyewe wanavyotoza kodi huko kwenye mipaka na juzi nilichangia hapa nikasema *TRA* fanyeni *calculation* zenu mkusanye kodi kule kwenye *border* zetu. Hata

kama mkituletea sheria hapa ya *import duty* kuwa, labda asilimia 30 *so right,* lakini mtakuwa mmeishakusanya kule.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pale Dubai *VAT* yao ni asilimia tano tu na vile wame-*encourage* watu wanaingia kwa wingi, mapato yao wanayapata wapi? Kwenye *VISA,* kila dakika mbili ndege zinatua pale, *VISA* dola mia, dola themanini kwa hiyo, tunaweza tukapata fedha kupitia kila sehemu tusijikite tu kwenye kodi, kodi kila sehemu. Kodi kweli ni chanzo cha mapato, lakini wakati mwingine tusione kwamba, huu ndiyo mrahaba peke yake, twende tutanuke.

Mheshimiwa Spika, jingine ni *point* yangu ndogo tu kwamba, suala hili la *cargo consolidation*. Hili lilikuwa ni jambo ambalo linasuambua sana kwenye nchi hii kwa sababu, wafanyabiashara wetu ndiyo hawa tunaowazungumza, wengi sana hawana uwezo. Uwezo wao ni mdogo, wanakua wanajichanga, kontena moja lina watu ishirini, lina watu kumi, sasa ilikuwa wanapata shida sana wanapokwenda kuchukua bidhaa zao kule.

Mheshimiwa Spika, yule ambaye ana-*clear* ile mizigo anapata usumbufu anapokwenda kuwapelekea mizigo yao wale wateja wake. Wakati ule hawezi kuandika kwenye *bill of lading* majina ya watu ishirini na yeye kontena lina watu zaidi ya ishirini. Jambo hili mimi nalipongeza na ninaiomba *TRA* ifanye vizuri, ili wananchi wetu sasa walete mizigo yao kwa mujibu wa uwezo wao, mwenye dola elfu tano, elfu mbili afanikiwe tuendeshe Tanzania yetu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Hamad Omar. Mheshimiwa Antony Peter Mavunde ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia huu Muswada wa Sheria ya Fedha. Awali ya yote namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa muda na wakati kama huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee na maalum kabisa naipongeza Serikali kwa kuja na hii *the windfall fuel profit toll* kwa maana ni chanzo ambacho hakitahusisha kabisa mlaji wa mwisho. Mlaji wa mwisho hawezi kuathiriwa ni wale wa uingizaji wa level za juu tu ndio ambao wataguswa na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa chanzo hiki cha mapato ninapongeza sana kwa kuja wazo hili. Ninaishauri Serikali iendelee kufanya tafiti, kutafuta vyanzo ambavyo vinaweza kuja kutuingizia fedha, lakini bila kumuongezea mzigo mlaji wa mwisho. Naipongeza sana Serikali kwa ongezeko hili la *the windfall fuel profit toll,* kwa ajili ya dharula kwenye miradi yetu ya barabara kwa lengo la matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali pia, kwa ajili ya chanzo hiki kwa sababu, wewe mwenyewe unajua namna ambavyo mabadiliko ya tabianchi yamekuwa ni majanga ya Taifa, siyo tu Tanzania, bali katika nchi mbalimbali hata kule kwenye Bunge la Dunia wewe mwenyewe unakabiliana na hoja nyingi za dharula, kwa ajili ya *issue* za mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, Serikali imefanya jambo la msingi kabisa kuhakikisha inakuja na chanzo hiki, kwa ajili ya kuikinga miundombinu yetu, kuweza kupata *protection measures* kabla na hata baada ya uharibifu mkubwa kuweza kufanyiwa maboresho makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja linalonipa ukakasi kuhusiana na chanzo hiki cha mapato ni je, ni cha uhakika kiasi gani? *Is it predictable?* Hivi unaweza ukasema mafuta yameshuka kwenye soko la dunia kwa dola mbili, mfano kwa pipa moja? Unaweza ukasema baada ya miezi sita au mwaka mmoja utakusanya fedha kiasi gani kutokana na chanzo hiki? *Can you figure out* kuhusiana na *quantification* ya kile ambacho utakipata kulingana na ongezeko la tozo hii? hili ndiyo ambalo linanipa wasi wasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa *quantification* ya kile ambacho tunaki-*predict* kiende kikaboreshe miundombinu yetu ya barabara. Ninasema hivi kwa sababu, majanga haya ya mabadiliko

ya tabianchi yamekuwa makubwa mno dunia nzima na sisi kwa hakika, kwa mujibu wa hali iliyotokea mwaka huu, tutegemee majanga zaidi mwakani. Kwa sababu barabara zetu zimekuwa dhaifu kwa hili ambalo limetokea kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, barabara zimekuwa dhaifu, zime-*deteriorate,* tunategemea msimu ujao wa mvua zitaharibika zaidi. Kwa maana hiyo tunahitaji chanzo cha uhakika cha kuhakikisha tunakwenda kuboresha miundombinu yetu baada ya majanga yatakayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, natambua kwa kila fedha za miradi zinazokwenda kwenye taasisi husika kuna ile asilimia tano, kwa ajili ya dharula, lakini kiuhalisia fedha ile imekuwa haiendi kama ambavyo imeandikwa katika kanuni, haiendi namna ile. Kwa hiyo, bado kama Taifa, tunahitaji chanzo sahihi cha mapato ambacho kitatuwezesha kujua baada ya miezi sita, baada ya mwaka mmoja, tunaweza kukusanya kiasi fulani cha fedha, kwa ajili ya kupeleka katika maboresho ya miundombinu ya barabara zetu baada ya mvua kubwa na majanga makubwa kuweza kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niishauri Serikali. Hivi inakuaje kwa mfano, najaribu kuwaza tu, katika miradi yote mikubwa ambayo labda tunapata fedha za wafadhili au za wahisani tukakubaliananao, wakati ule wanataka kutukopesha kwenye ile *loan agreement,* labda hata 0.5% ya hela ambayo wanatupa kama hisani au wanatukopesha itengwe, kwa ajili ya kuboresha miundombinu yetu kama fedha ya dharula. Kwanini nasema hivi?

Mheshimiwa Spika, nina hakika hata wahisani wenyewe hawatatamani kuingiza fedha zao katika miradi ambayo haiko *sustainable*, katika miradi ambayo inajulikana kwamba, baada ya majanga makubwa ya mvua itapoteza ile tunasema *value for money,* itakuwa haipo. Kwa hiyo, naamini kabisa kama watoa fedha, wafadhili sijui *donors* sijui wahisani hawa tukikubaliana nao, wakati wanatamani kutupa zile fedha zao au kutukopesha tuweke *at least* asilimia moja au nusu, kwa ajili ya fedha za dharula. Mimi

ninaamini hili litawezekana na litakuwa ni chanzo cha uhakika na itakuwa ni kitu ambacho ni *predictable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimeshuhudia hata kwenye lile daraja la Mfugale wale *JICA* waliotupa fedha bado wanafuatilia kila mwaka, ili kujua mmefanya *maintenance* kiasi gani? Kumetokea ajali hapa, inakuaje?

Mheshimiwa Spika, maana yake ni wanatamani kuona i*nfrastructure* ile inaendelea kudumu kwa mujibu wa kiwango cha usanifu ambacho kimefanyika pale. Kwa hiyo, kwa maana hiyo tukija kuwaambia hili tuwekeni, naamini kabisa tuwekeni asilimia hii, kwa ajili ya dharula zinazoweza kutokea kwenye miundombinu yetu. Naamini itawezana katika kuhakikisha tuna-*ensure sustainability* ya *infrastructure* zetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua namna gani madaraja yakikatika tunavyo-*paralyze* mambo mengi katika nchi yetu, kunakuwa hakuna tena *connectivity*. Ninyi wenyewe ni mashahidi, Madaraja ya Dumila na Mtanana yote yanapokuwa yamefungwa au yamefungika kutokana na mvua kubwa madhara yake tunayaona. Kwa hiyo, ni lazima tutafute chanzo cha uhakika cha mapato kuhakikisha tunaweza ku-*finance* mambo kama hayo ya dharula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika madaraja yetu mbalimbali yanatugharimu fedha nyingi mno kwa kutoa michanga kila mwaka baada ya mvua kubwa kunyesha. Kwa mfano, tunaona pale Jangwani, lakini bahati mbaya daraja lile lina *siltation* kubwa, haya madaraja kama la Mtanana na Dumila tunaweza tukatafuta namna ya kupunguza kutumia zile fedha za dharula kwa maana ya kwamba, Wizara ya Ujenzi ione haja ya kufikiria namna ya kuboresha madaraja yetu ambayo yamesanifiwa muda mrefu. Kunauwezokano kabisa wa kuongeza uwazi, ili kuruhusu *discharge* kubwa kuweza kupita kuliko ambavyo imekuwa huko kipindi cha nyuma kulingana na uongezeko kubwa la mvua zinazoongezeka kila mwaka kulingana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile licha ya kwamba, chanzo kilichotajwa hakina uhakika sana, lakini bado naishauri Serikali ihakikishe inakwenda kutengeneza kanuni ambazo zita-*guide* matumizi ya fedha hizi za dharula. Kwa mfano, inawezekana Mamlaka ya Hali ya Hewa imezungumza vizuri kutakuwa na mvua kubwa, mvua ambazo zitaleta maafa makubwa, lakini taasisi husika isifanye *protective measure* za kuhakikisha kwamba, maji yata-*flow* vizuri, wakawa hawajachukua hatua hizo, mwisho wa siku majanga yakitokea zitatumika fedha za dharula kuweza kufanya maboresho yale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo bila kutengeneza kanuni zitakazo-*guide* matumizi ya fedha hizi maana yake zitakuwa *abused,* chanzo hiki kitakuwa *abused.* Kwa mfano, mtu anaweza akakosa *room* labda wakati wa bajeti akawa hajatenga fedha katika bajeti ya kawaida, *end of the day* akaamua kutumia chanzo hiki kuweza kufanya kazi nyingine ambazo siyo za dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima kuja na miongozo *(regulations)* ambazo zita-*guide* matumizi ya fedha hizi. Vilevile kuhakikisha kwamba kama ilivyo kwenye Sheria ya Maafa, kunajulikana vigezo na masharti ni nini vina-*determine* kwamba hii ni kazi ya dharura? Ni nini ina-*trigger* kwamba hii inaitwa kazi ya dharura? Isije ikawa ni fedha chanzo kinawekwa halafu kinakwenda kutumika ndivyo sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kuishauri Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, *oh!* naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Hamad Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii ya kukupongeza kwa dhati tunapokaribia kumaliza kikao chetu cha bajeti. Ninakupongeza kwa sababu umewatendea haki Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani kama sikosei hicho kiti ni cha moto sana. Ni vigumu kuwatendea haki watu wote lakini umewatendea haki Wabunge, iwe Wapinzani au Chama Tawala, lakini kubwa zaidi ulilonifurahisha ambalo linafaa kupongezwa ni kwamba siku zote umekuwa katikati ku-*bridge the gap* baina ya Serikali na Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi hata hii leo asubuhi tumeona mfano umewakutanisha Wabunge wenye zao la chai pamoja na Waziri wa Kilimo na umefanya hivyo huko nyuma. Inabidi kufika mahali tukawa na *win-win situation.* Kwa hiyo nina hakika kesho tunaondoka Bungeni hakuna atakayesema ni mshindi. Sote ni washindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kweli mimi nimekubali kwamba wewe unafaa kuwa Rais wa Mabunge yote ya Dunia. Unafaa sana na *change* inabakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na *entire* timu ya Wizara ya Fedha. Nasema *honestly* mimi nimefanya kazi na Mawaziri wengi wa Fedha lakini sijapata kuona Waziri ambaye ni *doctor malleable* ambaye unaweza ukampa hoja zako na mkafikia *to amicable consensus.* Nasema Waziri unaupiga mwingi. Hata haya mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti lakini mengi ya mapendekezo ya Waziri kwa maana ya kurekebisha huu Muswada wa Fedha tumekubaliana nayo, isipokuwa machache sana. Nina imani *by the end* anakuja ku-

*wind up* Waziri, tutakuwa tumekubaliana *almost 98%* ya mapendekezo ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muswada huu ni muhimu sana kwa sababu unajenga hatma ya mwaka mmoja. Hakuna Serikali yoyote ya duniani ilikuwa inaendeshwa bila ya kodi. Mimi nasema siku zote, siri ya kodi ni mambo mawili. Moja, ni ku-*collect* kodi *with minimum inconvenience to the tax payers.* Hiyo tunafanya, tunakwenda kwenye *cashless economy.* Juzi nilikuwa nasema hapa kwamba, ukiangalia mtandao wa simu au simu zetu hizi, sasa hivi tunatumia simu kwa kulipa malipo, lakini ukiangalia zile *transfers* tunazofanya kwenye simu na hasa baada ya tozo nyingi kuondolewa. *Transfers* na *withdrawals* unakuta kwamba *transfers* zinazidi sana *withdrawals*. Sasa unafika mahali unasema *ahaa!* kweli simu sasa inatumika kama chombo cha miamala ya fedha na nafikiri tutafika mahali tutakwenda kwenye *cashless economy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze mambo matatu tu. Moja, ni suala la *contiguous fund.* Matakwa ya Katiba yanatulazimisha lazima tuwe na *contiguous fund.* Hiyo, *the question is undebatable* huwezi ukalijadili. Katiba inasema lakini kama hiyo haitoshi Sheria ya Bajeti Sura 439 inasema vile kuanzishwa kwa *contingency fund*. *But the question now rise* tunajiuliza, nini hasa maana ya *contingency*? Ina-*deal* na nini?

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu na kwa uzoefu wa nchi nyingi zinazoenda na Mfumo wa *Westminster model, contingency* ina-*deal* na *unforeseen emergencies. Unforeseen emergencies* maana yake ni nini? Tunasema ni nini? Ni mahitaji yasiyotabirika. Haya yako manne kama sikosei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nchi ikikumbwa na vita hatuwezi tukakaa tukasema kwamba, tutasubiri Bunge likutane ili lipambane na vita. Haiwezekani lazima kuwe na fungu *in the event* nchi imeingia katika vita, lazima uwe na fedha za kupambana na vita. Huwezi ukacha nchi inavamiwa wewe unasubiri Bunge lije. Kwa

hivyo, Waziri pale anapewa *mandate* ya kutoa fedha *from the contingency. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ya pili ni njaa, watu wetu wanapokuwa na njaa hiyo ni *unforeseen emergency*. Tatu, ni maradhi ya milipuko. Kwa mfano, Mungu atunusuru juzi hapa tulikuwa na *Covid*. Sasa Waziri kama huna *contingency* utapata wapi fedha? Pia nne ni tabianchi. Hayo mambo manne. Tabianchi *in the event of* mafuriko *and drought* unatumia pesa *from the contingency*.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa utaratibu wa Nchi nyingi za *Westminster Model, contingency fund* inakuwa ni *5% of the total nominal budget,* lakini hapa tunapendekeza *one percent* nadhani hiyo ni ndogo. Mimi sina tatizo la vianzio ambayo Waziri Muswada umependekeza vianzio vile vinne, lakini nina tatizo la ile *Section* (Ibara) ya 37 au 37 kama sikosei. Maana yake tunafanya marekebisho katika Ibara ya 35 na 37. Ibara ya 37 inapendekeza vianzio mimi sina tatizo nayo, lakini 35 inasema kwamba fedha za *contingency* zitatumika katika kutengeneza barabara zilizoharibika kutokana na *El-Nino* iliyotukumba kuanzia Mwaka 2023 – 2024, lakini hilo ni tatizo mojawapo tu, *anything can happen* kutokana na haya mambo manne niliyokutajia. Kwa hiyo lazima tuwe na mfuko maalumu ambao utakuwa na fedha nyingi. Nchi nyingine zinasema *5% of the total nominal budget,* sisi hatusemi hivyo lakini basi kwa sababu kuna vile vyanzo vinne ambavyo nilielekeza nadhani hapa tunakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ninalotaka kuzungumza ni suala la *TPA*. Tumefanya marekebisho katika Sheria ya Bandari Sura 166 kifungu cha 6 na 7 ambacho kifanya *TPA* iweke fedha zake kwenye *special account* ambapo inakuwa *administered* na *BOT*. Nasema hilo ni jambo jema, lakini wema huo huo wa jambo kwa nini hatufanyi kwenye *Ngorongoro Conservation Area Authority (NCCA)* na *Tanzania National Parks*? Nafikiri tungefanya katika mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, nasema kwa nini tufanye hilo? Kwa sababu na leo nitatoa *surprise* moja hapa ambayo tunafaa tufanye, kwa nini? Kama kuna sekta ambayo inatuingizia fedha za kigeni ni sekta mpya ya utalii. Baada ya *Royal Tour* ya Mama hamwezi kuamini leo nimefanya *google search* nimekuta ukilinganisha nchi mbili, sitaki niseme hii nchi nyingine ambayo ilikuwa *competitor* wetu kwa mambo ya utalii, maana siku zote walikuwa wanatangaza. Wakienda kwenye yale Masoko ya Kitalii wanasema *if you want to see Kilimanjaro come to this country. If you want to see Ngorongoro come to this country not knowing* kwamba, watu wengi walikuwa hawajui kwamba hizi zote zipo Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa bada ya *Royal Tour* ya Mama, nikilinganisha miaka hii miwili nchi yetu na nchi hiyo sitaki niiseme, utashangaa. Hizi nimezipata kwenye *google search* kwamba, mwaka 2022-2023 Mapato ya Tanzania yatokanayo na utalii yame-*raise from 2.5 billion dollars to 3.4 billion dollars, an increase over 10%, where's* in *Kenya sorry*, maji yakishamwagika hayazoleki *where in that country* ambayo sitaki kuitaja jina lake, lakini maji yakimwagika hayazoeki. Imeongezeka *from 1.85 to 2.7 billion dollars.* Sisi tupo kwenye *3.4 billion dollars* mwaka huu. Sasa hilo ni jambo zito sana. Inafaa tumpigie makofi mama yetu na tumpe maua yake. hayo yasingewezekana kama si jitihada za mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama mama yetu ametufikisha hapo na *the biggest hazardously* katika kutangaza utalii ni kwamba *always* Tanzania tumekuwa *not so aggressive in marketing*. Tukienda kwenye *trade tours* wenzetu wanatupiga karata, kwa sababu yeye anasema; "*If you want to see Mount Kilimanjaro come to Kenya, if you want to see Ngorongoro come to Kenya.*" Sisi wenyewe hatutangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri suala la ku-*raise* mapato mengi ya utalii ni suala la msingi sana na kwa kutumia Shirika letu la Utalii *(Tanzania Tourism Board)* kuwapa pesa ambazo watatutangazia utalii. Nadhani tukiwasaidia *TTB* waka-*embark* katika *aggressive*

*marketing strategies* nadhani tutafika mahali tutafika pazuri na pale tunachokipata ni fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia la tatu na la mwisho nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Kilimo. Najua watu wengi wamesema habari ya sijui *sugar gap* na nini. Mimi nasema, labda niseme Kiswahili kidogo hapa kwamba; "Mti wenye matunda mengi, ndio unaopigwa mawe." Sisi kamati yetu baada ya kukaa na Waziri wa Kilimo jambo hili nilitaka mnisikilize vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, *bear in mind* kwamba Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta au tasnia ya sukari. Nafikiri viwanda vingi hivi vilianzishwa na Serikali. Viwanda vitano hivi vilivyokuwepo vingi ukiacha hiki Kiwanda cha Bagamoyo cha Bakhresa. Kwa hiyo, *investment* kubwa sana imefanywa na Serikali katika tasnia ya sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini utashangaa hii *sugar gap* ambayo inazungumzwa humu Bungeni, *production* ya sukari tumeona inaongezeka *over the years* na mwaka huu tuta-*exceed* matakwa ya sukari kwa mwaka. Matakwa hayo ni *490,000 tones,* mwaka huu tutazalisha *more than 500,000*. Mwaka unaokuja tutazalisha zaidi tutafika mahali nchi hii itakuwa inauza sukari nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa *as the production of sugar increases lineally,* ninapofanya mkono wangu nafikiri mnanielewa watu wa hesabu, lakini *to the contrary the sugar gap is declining asymptotically tending to zero*. Kwa hiyo tutafika mahali hatuna *sugar gap,* itakuwa ni ndoto. *There will be no sugar gap*. Sasa hili lazima tumpe maua yake Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jamani kuendesha nchi siyo jambo la masihara, mwenzetu ana kazi ngumu. Mimi nilikuwepo kule mbele. Mimi ukiniambia niende kule mbele sasa hivi sitaki, *to be honest*. Ni kazi ngumu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. *(Kicheko)*

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja 100%. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilimwacha amalizie mafunzo kwa sababu unajua hatua za mtu mzima zipo taratibu kidogo. Kwa hivyo, lazima kiti kitambue hatua hizo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia jioni ya leo na mimi nianze kumpongeza mtoa hoja kwa wasilisho lake zuri. Pia nichukue fursa hii kuipongeza sana Kamati ya Bajeti ambayo inaongozwa na uzalendo mkubwa sana na wanaipenda sana nchi hii na wapo tayari kuhakikisha kwamba kila jambo linakwenda vizuri. Tumekaa na kushauriana nao na tumejifunza mambo mengi kupitia Kamati hii ya Bajeti na hivyo imetufanya tumefikia hapa tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi hoja yangu kubwa ni suala la usafishaji wa madini na hasa dhahabu kwa *gold refineries* tulizonazo hapa nchini na ndiyo umekuwa Mchango wa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, suala la usafishaji wa madini ni sehemu ya Sera ya Madini na ni jambo ambalo tunalipa mkazo mkubwa sana kwa sababu lina faida mkubwa sana kwa nchi. Tuna viwanda sita vya usafishaji wa dhahabu hapa nchini, kimoja kinamilikiwa na *STAMICO* ambaye ameingia ubia na mwekezaji na vingine hivi vinamilikiwa na Watanzania wazawa, ambao tuna kila sababu ya kuwalinda, ili waendelee kupata *feedstock* na mwisho wa siku waweze kukidhi ithibati ya *LDMA* ambayo inataka kuwepo na *feedstock* isiyopungua tani 10 ya dhahabu kwa mwaka na tani 50 ya *cooper* kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo Serikali ilichukua hatua katika Sheria ya Fedha ya mwaka jana tuliyopitisha hapa Bungeni ambayo ndiyo inaenda kuishia, Serikali ilipunguza mrabaha wa dhahabu yote inayopelekwa katika viwanda vya kusafisha, kutoka asilimia sita kwenda asilimia nne. Vilevile, Serikali ilifuta ada ya ukaguzi kutoka asilimia moja mpaka sifuri. Lengo lake kubwa lilikuwa ni kichochea dhahabu kwenda katika viwanda vya usafishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo za Serikali za kuhakikisha kwamba dhahabu inakwenda katika viwanda vya kusafishia dhahabu, lakini dhahabu nyingi haikwenda. Kwa mfano, Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu pale Geita cha *GGR*, dhahabu ambayo waliipata ni kilo 418 tu na wakati huo huo *BOT* walitenga fedha kwa ajili ya kununua dhahabu tani sita. Tatizo ni nini? Kwa nini dhahabu haiendi na mrabaha umeshushwa kutoka asilimia sita kwenda asilimia nne na ada ya ukaguzi asilimia kwenda sifuri?

Mheshimiwa Spika, hapa kuna tatizo kubwa ambalo lazima niliseme hukmu ndani na Wabunge walielewe na tulitatue sote kwa pamoja. Wafanyabiashara wetu wa dhahabu na wachimbaji wadogo wa dhahabu hawana mitaji ya uhakika na ya kuwafanya kufanya bishara hii. Kwa hiyo, mitaji mikubwa wanayoitegemea ni mitaji inayotoka nje ya nchi. Kwa hiyo, asilimia kubwa wanaingia makubaliano ya awali. Anapokea fedha kutoka kwa wafanyabishara wengine wakubwa nje ya nchi kwa ajili ya wao kutafuta dhahabu kuwauzia wao. Ndiyo maana unaweza ukastaajabu kwamba katika hali ya kawaida kila mfanyabiashara angependa kutengeneza faida, lakini hapa tunawashushia mrabaha kutoka asilimia sita kwenda asilimia sita na dhahabu haiendi. Kwa hiyo, tatizo kubwa na la msingi ni kwamba watu wetu hawana mitaji ya kutosha ya kufanya biashara hii ya dhahbu.

Mheshimiwa Spika, suluhisho ni nini? Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesoma hapa asubuhi. Tunakwenda kufanya marekebisho ya Kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini Sura ya 123 ambacho Kifungu cha awali kilimpa Waziri mamlaka, baada

ya ku-*consult* na wenye haki madini, kutenga kiasi kadhaa cha madini kwa ajili ya *refinery* na *smelting.* Ndiyo kifungu kilikuwa kinasoma hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa kifungu hiki mimi nikawaita wenye haki madini wote ili tupate dhahabu ambayo itakwenda katika viwanda vya kusafishia dhahabu. Tulivyowabana kwenye kifungu hiki hoja yao ikawa ni kwamba, kifungu kilichopo hivi sasa kinasema; "Waziri atashauriana na wenye hakimadini, kutenga kiasi kadhaa cha madini kwa ajili ya kufanyiwa *refinery* au *smelting.*" Wakatuambia Waziri sisi ni *compliant,* haya ambayo yapo ndani ya sheria hii sisi tunayafanya. Kwa hiyo, kama Serikali tukaona kwamba kuna mwanya ambao lazima tuuzibe.

Mheshimiwa Spika, *spirit* ya kile Kifungu ilikuwa ni kwamba, lazima kiasi kadhaa cha madini ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia kibaki humu ndani kisitoke chote, lakini haikuwa *captured* hivyo! Ndiyo maana Waziri wa Fedha amekuja na mapendekezo na ameongeza maneno kwamba, "Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Madini kwa kushauriana na wenye haki madini, watatenga kiasi kadhaa cha madini kwa ajili ya kuwa *refined* na kufanyiwa *smelting* na biashara ndani ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikaenda mbali zaidi ikasema, "Kiasi ambacho kitatengwa kitaamuliwa na Waziri baada ya kutunga Kanuni na kisipungue asilimia 20 ya madini yote yatakayozalishwa hapa nchini Tanzania". Sasa, Waheshimiwa Wabunge hoja ambayo ilikuwa inasemwa hapa ni kwamba *refinery* hazipati *feed stock*, mzigo hauendi.

Mheshimiwa Spika, nimesema changamoto ya Kifungu cha 1 ilikuwa ni ngumu kuitekeleza. Kwa hiyo, kwa mapendekezo haya maana yake ni kwamba, mimi nitatunga Kanuni ya kumtaka mzalishaji yeyote wa dhahabu hapa nchini, yeyote! ahakikishe anatenga asilimia 20 ya uzalishaji wake kwa ajili ya *trading* ya ndani ya nchi. Hapo ndipo *BOT* atapata dhahabu na viwanda vya

kusafisha dhahabu vitapata dhahabu. Isipokuwa tu inawaondoa wale ambao tuliingia nao mikataba ya awali ambayo tuna *framework agreement* na baadhi ya kampuni lakini katika hali ya kawaida tunaanza na asilimia hizo ambazo zimesemwa na Kifungu kile kinaniambia isipungue asilimia 20. Kwa hiyo, maana yake ninaweza nikaenda asilimia nyingi zaidi kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa dhahabu kwa viwanda vyetu vya ndani. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwaondoe hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili na la mwisho, hili ni kubwa zaidi kwamba watu wetu hawana mitaji lakini tunayo njia ya kuwasaidia. Badala ya kutegemea fedha kutoka Dubai, tuna uwezo wa kuwasaidia kuwawezesha ndani ya nchi, fedha ile wakaipatia hapa hapa ndani ya nchi wakafanya biashara hapa na fedha ikabaki hapa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeongea na wenzetu, nimeongea na Gavana wa Benki Kuu na Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha wana *export credit guarantee scheme*, ile itumike kwa ajili ya kuwapa dhamana, wafanyabiashara wa Kitanzania wakakopeshwa, wachukue fedha wanunue dhahabu wenyewe kuliko ilivyo sasa hivi. Sasa hivi changamoto ni kubwa kwa sababu watu wetu hawana mitaji na tunayo namna ya kuweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka niwaondolee hofu Waheshimiwa Wabunge ya kwamba, kile kilio cha upatikanaji wa dhahabu kwenda kwenye viwanda sasa hivi tunakwenda kukitatua kwa sababu itakuwa ni sharti la lazima la kutenga kiwango kadhaa kwa ajili ya kwenda kusafisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo ninaunga mkono hoja. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, pili kukushukuru wewe kwa namna ambavyo unaendelea kutuongoza katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninataka niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa maoni katika sekta inayohusu kilimo na michango yao kama Serikali tutaendelea kuifanyia kazi na kurejesha mrejesho kwa kwao.

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo makubwa matatu. Kwanza, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu; ninamshukuru Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu vilevile ninaomba nimshukuru kwa dhati kabisa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote wa kodi wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulipeleka mapendekezo na ushauri kuhusu sekta ndogo ya chai na changamoto zinazokabili sekta ya chai. Ninawashukuru kwa kusikiliza. Mambo matatu yatatokea katika *Finance Bill* hii. Kwanza ni kutoa unafuu wa *corporate tax* ya *exemption* kwa miaka mitatu kwa viwanda vyote vya chai nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kama Taifa tulikuwa tunatumia chai inayozalishwa na viwanda vyetu vya ndani wastani wa kilogramu milioni sita kati ya kilogramu milioni 24 tulizokuwa tunazalisha. Kwa kuwa tuko kwenye soko moja la *EAC*, wenzetu walifanya jitihada ya kuanzisha *blending facility* katika mnada wao na kuwapa unafuu wazalishaji wao. Chai yao ikawa nafuu kuingia kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wazalishaji wa kwetu wamekuwa na *disadvantage* kwenye *VAT*, kwenye *blended tea for local production*. Ninamshukuru sana Waziri, tumekubaliana kwamba katika *amendments* za Serikali zinazoingia leo hapa, tunaenda kutoa *exemption* kwa *local processors*. Wanapata *VAT exemption* ya *blended tea* katika viwanda vyetu vya ndani ili kufanya viwanda vya ndani viweze kuchakata chai na itumike ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kwenye *fermented tea,* tumekubaliana kwamba Kanuni za *TRA* zitawekwa wazi ili kuondoa *VAT* kwenye *process* ya *fermentation* ya chai ili kuweza kuifanya chai yetu kuendelea kuwa *competitive*, hii itaweza kuinua sekta yetu ya chai na viwanda kurudi kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ninamshukuru sana kwa kukubali kutoa fedha za *P4R* kwa ajili ya sisi kama Serikali kufunga *blended facility* kwenye mnada wa chai wa Tanzania ili wafanyabiashara wetu sasa waanze kuichanganya chai na wakiuza iwe katika *form* ya *blending* na iweze ku-*compete* na wengine, jambo ambalo wangetakiwa wa-*invest* wao, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nichangie eneo la pili kuhusu eneo la sukari. Kumekuwa na mjadala mkubwa sana ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Ni yapi mabadiliko tunayoyafanya na haya mabadiliko tunayoipa *Nationa Food Reserve Agency* mamlaka ya kusimamia pale ambapo kunakuwa na *sugar gap*.

Mheshimiwa Spika, moja, siyo jambo jipya duniani, leo hii tunavyoongea, *Food Reserve Agency* ya Misri imeingiza sokoni jumla ya tani 400,000 walizokuwa wamezihifadhi miaka miwili iliyopita. Siyo jambo jipya duniani linafanyika. *Mandate* ya *Food Reserve Agency* ni kuhifandhi na kusimamia uratibu wa suala la chakula pale ambapo kunatokea upungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia, *mandate* ya *Nation Food Reserve Agency* kwenye sukari itakuwa kuratibu, kusimamia na kuhifadhi *sugar gap* na siyo kitu kingine, siyo kitu kingine! Kama tunafika mahali hatuiamini Serikali na kuitilia hofu kwamba, Serikali yenye jukumu ya kusimamia usalama wa chakula, usalama wa wananchi, usalama wa wawekezaji, tunakuwa na hofu nayo, *then* tutakuwa na tatizo kubwa sana kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge; niwahakikishie na tumekaa na Kamati yako ya Bajeti

tumekubaliana tutaweka *additional two amendments* kwenye hiki kipengele ambazo zitakuja pamoja kuweza kuweka *buffer* kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, moja, kipengele kitaongezeka kinachosema wazi hakutakuwa na *importation* ya *sugar* pale ambapo tumefika kwenye kujitosheleza katika nchi yetu. Hii inawekwa na *amendment* tume-*move*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, utaratibu wa ku-*determine sugar gap* ulikuwa umeelezwa kwenye Kanuni sasa tunauweka kwenye Sheria. Kwamba, *Technical Committee* inayohusisha Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha, *TRA*, ambayo itakuwa inafanya *quarter review* kuangalia *against performance agreement* tutakayosaini na viwanda dhidi ya mahitaji ya nchi, hii itakuwa inafanya kazi kila *quarter* na kuonesha taarifa ya uzalishaji dhidi ya uhitaji ili tuwe na *future* ya kuamua kwamba je, tutakuwa na *gap* ama tutakuwa hatuna *gap* badala ya utaratibu uliopo wa kusubiri mwisho wa mwaka kufanya tathmini na kupeana vibali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu wa kuipa *NFRA* unatuondolea haya mambo ya kushakiana na utaratibu wa kutazamana na mambo ya vibali vibali na kuondoa siasa zinazozunguka kwenye sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na mimi sitaki ku-*condemn* mtu yeyote, niwakumbushe 2016/2017 tulienda kutafuta sukari kwa bunduki ni Tanzania hii, 2018 kwenda 2019 tulitafuta sukari kwa bunduki na polisi na kufungua maghala. Kwa nini ikiguswa sukari *becomes a big issue* in *our country*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaliomba Bunge lako Tukufu, kinachoshughulikiwa na *National Food Reserve Agency* ni *gap* siyo kitu kingine. Wazalishaji waendelee kufanya kazi ya kuzalisha na Serikali itaendelea kuwalinda na kuwaangalia. Serikali hii kwa

mwaka huu kwa ajili ya ku-*support expansion* ya viwanda, bajeti tuliyopitisha tunatenga 7.2 *billion shillings* kwa ajili ya kwenda kuwasaidia wakulima walioko Kilombero kwa ajili ya kuzalisha miche. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti tunayomaliza tarehe 30, Serikali imetoa fedha, kampuni inayoitwa Saba *Consultancy* inafanya *feasibility study* na *detailed design* kwenye Bonde la Kilombero kwa ajili ya ekari 30,000 za wakulima wa miwa. Ni namna gani Serikali inayowekeza fedha za umma namna hii itaamua kwenda ku-*distort the economy*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachokitafuta mwekezaji alindwe, mkulima alindwe na mlaji alindwe. Hiki ndicho tunachokitengeneza. Mapendekezo tuliyoyaweka hapa tunataka *transparency* kwenye *cost of production*, lazima tuwe na *transparency*! hatuwezi kutengeneza *a monopoly* ambayo *Government to access information becomes difficulty* na kwa sababu tu ya sheria tuliyoweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunachokitaka, *distribution network* iwe *transparent* na kuwe na uwazi, tunachokitafuta, Bodi yetu ambayo ni *regulator*, kuna hoja ameisema Mheshimiwa Vedastus ninataka niijibu. Moja tu, kwa nini *mandate* hii ya kuhifadhi na kuratibu sukari hatumpi Bodi ya Sukari? Mwenye mamlaka ya kisheria ya usalama wa chakula katika nchi hii anaitwa *Nation Food Reserve Agency*, ndiye amepewa *mandate*. Leo hii kukitokea upungufu wa mahindi katika nchi yetu, kukitokea upungufu wa mchele katika nchi yetu, hata kama tuna-*import* kutoka nje, mamlaka yako chini ya *Nation Food Reserve Agency*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tumemwamini kwa chakula chetu cha mahindi, tumemwamini mpunga ambacho ni *staple food* ya watu wetu, tumemwamini mtama, tumemwamini kwa dhana ya chakula, kwa nini hatutaki kumwamini kwenye sukari?

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya kwamba atahifadhi wapi, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tusipewe *terminology* za Kizungu za kututisha. Ni hivi, hakuna muujiza katika kuhifadhi sukari, hakuna! Sukari inahifadhika na tunahifadhi katika magodauni ya kawaida. Haihitaji *air condition*, haihitaji nini, tunahifadhi katika magodauni ya kawaida na una uwezo wa kuhifahdi sukari mpaka miaka miwili na ukai-*dispose*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeipa *mandate NFRA* na tumeenda ku-*gazette* kwenye upande wa *food* kui-*gazette* katika *regulation*, hii ni *instrument* ambayo tunaitumia *for stabilization*. Kama ambavyo tunawa-*stabilize* wakulima, kwa nini tusiwe *positive* tu tukafikiri kwamba kuna siku kutakuwa na *surplus sugar* kwenye nchi hii na kutakuwa hakuna mahali pa kupeleka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *National Food Reserve can intervene* na akahifadhi na viwanda vikaendelea kufanya kazi. Kwa hiyo, mimi ninataka niombe, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuiamini Serikali. *There is no bad intention, there is a good intention* na tuta-*protect* uwekezaji unaondelea katika sekta hii, tuta-*protect* viwanda, tutasimamia jambo hili kwa uwazi na hatuta-*distort* eneo ambalo linakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwa kunatokea *market failure*, hutokea *market failure*, ndilo jukumu la Serikali kufanya *intervention*. Kwa hiyo, ninataka niombe Bunge lako Tukufu, nia ya Serikali ni njema na ninataka niwaambie wawekezaji, Serikali itaendela kuwa-*support*. Tutaendelea ku-*expand* na tutaendelea kuwapa msaada wowote wanaohitaji ili waweze kuendelea kuwekeza katika sekta ya sukari, *bottom line* tunao Watanzania ambao tunahitaji kuwahudumia, ni lazima tuwahudumie, ni lazima tutende haki kwenye *economy*, ni lazima tuwatazame Watanzania hawa wanyonge katika nchi yetu ambao kipato chao ni kidogo. Bila kufanya hivyo, bila kuweka mkono wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo katika *mandate* hii mnayotupitishia kwenye sheria tutaweza ku-*regulate*, leo kuna *disparity*, mkulima

aliyeko Kagera analipwa shilingi 70,000 *per ton*. Mkulima alioko Kilombero *100,000 shillings,* wanatwambia *this is a free market economy, it is a discussion,* Serikali lazima i-*intervene*. Ninataka niwaambie wakulima wa Kagera, wakulima wenu watalipwa *equal* na wakulima wa Kilombero. Watalipwa *equally* na wakulima wa Kilombero tukipitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, nia ya Serikali ni njema na tutakachoshughulikia kwa mujibu wa sheria hii tunayoifanyia marekebisho leo ni kusimamia, kuhifadhi, kuagiza na kusimamia usambazaji wa sukari ya *gap* peke yake siyo kufanya hili jambo linakuwa la kiholela. Hatuwezi kuua sekta ambayo tumeijenga kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshawaamini *Private Sector*, mwanzo walikuwa wanaingiza *traders*, Serikali ikawapa *producers* tumepata matatizo, sasa kachukua baba mwenye nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Ninataka kuelewa jambo moja, hii *National Food Reserve Agency*, *Reserve* ninadhani Kiswahili chake ni Hifadhi. Inaitwa mamlaka ama inaitwa nini ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula? Inaitwa Wakala, Wakala wa nini? Hebu sema kwa Kiswahili.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni Wakala wa Uhifadhi wa Chakula wa Taifa.

**SPIKA:** Sawa. Kama sukari ikiwa sehemu ya chakula, kuna sentensi moja hapa umesema, maana tutakuja kwenye kutunga sheria Waheshimiwa Wabunge lazima tutunge sheria ambayo wote tunakuwa na uelewa sawasawa.

Umesema mtaongeza Kifungu kwenye yale marekebisho ama maboresho ya sheria, kwamba hakutakuwa na uingizaji wa sukari

nchi ikijitosheleza kwa sukari. Kama huyu Wakala kazi yake ni kuhifadhi, nchi kama haikuwa na *gap*, kwa mfano sasa hivi si mnahifadhi ya mahindi? Kuna tatizo la mahindi hapa nchini? Hapana, tuna tatizo la mahindi hapa nchini?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, hapana.

**SPIKA:** *NFRA* ina mahindi haina?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, inayo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, sukari tutakuwa hatuhifadhi ila mahindi, maharage, kila kitu tutahifadhi isipokuwa sukari. Kwa sababu kama ni sehemu ya chakula, maana yake na yenyewe inahitaji ihifadhiwe ili inapotokea changamoto iwepo. Ama sukari ni maalumu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, *logically* unachokiongea ni sahihi. Kwa hiyo, katika *discussion* tuliyofanya na wenzetu wa Kamati ya Bajeti, Serikali iliona kwamba ili tuweze kufika mahali kuifanya Kamati ya Bajeti kuwa na *confidence,* kwa sababu hofu ilikuwa ni kubwa, tukasema kwamba pale ambapo nchi inakuwa imejitosheleza ina *surplus*, basi *NFRA* hatofanya kazi ya kuagiza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu *function* tunayompa, mojawapo ni kuagiza *at this moment*.

**SPIKA:** Sawa. Mimi nimekuelewa lakini kwa sababu linakuja kwa sura ya kutunga sheria, nitasubiri nikione hicho kifungu. Kwa nini, kwa sababu kama tumeipa kazi hiyo huyu Wakala wa Kuhifadhi Chakula, halafu vingine vyote ahifadhi isipokuwa sukari, halafu sukari mvua itakapotokea tutasema mwaka huu hakukuwa na *gap*. Tulijitosheleza katika soko kwa hivyo, ndiyo maana kwenye ghala letu hakuna sukari. Sina hakika kama huko ndiko tunakotaka kufika.

Mheshimiwa Waziri ninafikiri tunataka kwenda mahali ambapo kama ambavyo mahindi yakikosekana Serikali inapeleka mahindi

sokoni kusaidia bei isipande, ndivyo ambavyo inapaswa kuwa kwenye hifadhi ya sukari pia, kwa sababu huyu ni Wakala wa Hifadhi na anahifadhi chakula. *(Makofi)*

Namuona Mheshimiwa Mbunge, nyuma kule amesimama, Mheshimiwa Manyinyi. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nadhani Mheshimiwa Waziri, amesema vizuri sana kwamba ile sheria hii ambayo tunaitunga itafanya kazi moja tu, kuhakikisha pale penye *gap* ina *intervene*. Sasa kwa sababu saa hizi viwanda vyote vinazalisha, hatuna *gap* na sukari tani zisizopungua 70,000 zipo njiani zinakuja, sasa *NFRA* wakubali waanze kutunza hiyo sukari katika hiki kipindi ambacho hakuna *gap* ili hivi viwanda viweze kufanya, waweze kuendelea kuuza sukari.

Mheshimiwa Spika, maana tofauti na hapo bei yao ni kwamba itakuwa juu ambayo ni shilingi 125,000, bila kodi itakuwa shilingi 102,000, hii ya nje ambayo haina kodi itakuwa shilingi 115,000. Sasa ili waweze kufanya kazi basi Serikali itunze.

**SPIKA:** Umeeleza vizuri sana. Bei ya sukari Malawi ni shilingi ngapi mfanyabiashara na bei ya sukari Zambia na bei ya sukari Kenya na bei ya sukari Uganda ni shilingi ngapi? Yaani hapo tunalingana ama tupo tofauti na hizo nchi?

Subiri kwanza namuuliza Mheshimiwa Mbunge, anataarifa zote labda kama kuna mtu anataka kumsaidia, Mheshimiwa bei unazijua za Sukari?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, mimi bei ninayoijua ni bei ya sukari ambayo ni *imported* na bei ya sukari ambayo ni ya hapa nchini, hizo zingine sina taarifa kamili.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mwijage anataka kutusaidia, tusaidie bei za sukari Mheshimiwa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, bei za sukari duniani hutofautiana na huu ukanda wa chini ambao umeu-*refer* Malawi, Swaziland, *South Africa* mmiliki wa kiwanda ni mmoja au ni ndugu wawili, kwa sababu gani? Viwanda vyao vimesha-*mature*, yaani ili unapozalisha sukari, kiwanda kinafika kimesha-*mature* na ndiko sasa hivi vinapokwenda viwanda vya Tanzania, ile *productivity* imeshakuwa kubwa. Kwa hiyo, ukishindana na vile viwanda utakuwa na *disadvantage*, ndiyo maana mimi Serikali hii iliwahi kunituma nikaenda kuomba zile nchi zisilete sukari kwenye nchi hii, walinituma mimi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa watu wengine...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikwambie moja, nikueleze...

**SPIKA:** Ngoja, ngoja...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, ngoja...

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, *I am coming*. Nikueleze moja, niwape mfano ambao watu wanapenda kuurejea, wanarejea nchi za Brazil. Brazil kwa sababu ya *maturity* yake sukari...

**SPIKA:** Ngoja, Mheshimiwa Mwijage, usiende kule mbali sana kwa sasa, twende hapa jirani na nimeuliza swali rahisi tu, bei ya sukari Malawi, Zambia, Uganda na Kenya zinalingana? *(Makofi)*

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, mimi ninazo.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mwijage, ameketi kuashiria bei haijui. Haya Mheshimiwa Priscus Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa siendi kwenye bei, lakini pale mwanzo ulipoanza kwenye kuhifadhi, kwenye kuhifadhi, sukari ina kipindi cha kukaa siyo kama mahindi. Sukari baada ya kutengenezwa haizidi miaka mitatu, kwa hiyo kama *NFRA* akiihifadhi kila baada ya miaka miwili atamwaga...

**SPIKA:** *NFRA* atakapoihifadhi yeye atajua inaisha lini muda wake ataitoa, si tumeambiwa hapa mfano jamani wa Egypt wametoa, mbona tunakuwa na wasiwasi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye swali ulilouliza, kwa kuwa mimi natoka Mkoa wa Songwe na ndiyo tumepakana na hiyo nchi ya Zambia na Malawi, sukari kule tunanunua shilingi 2,500. Sisi Tunduma tunatumia sukari ya Zambia na Malawi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, mimi kwa mujibu wa gazeti la *East African* umeuliza bei, nimeangalia hapa kwa mujibu wa gazeti la *East African* naomba nisome bei za Afrika Mashariki. Nitazisoma kwenye dola halafu mta-*convert*.

Mheshimiwa Spika, bei ya sukari Tanzania kwa mujibu wa gazeti la *East African* ni dola 2.37, bei ya sukari Kenya dola 1.30, bei ya sukari Uganda dola 1.35. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenisongole, ulikuwa umesimama.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa taja bei yako na wewe naona unawasikiliza majirani.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ni shilingi 3,000 mpaka shilingi 3,500 bei ya sukari ambayo tunanunua pale kwetu Mbozi. Ila kwa kuongezea ni shilingi 3,000 mpaka 3,500 ila kwa kuongezea...

**SPIKA:** Ipi sasa ya hapa nchini ama wapi?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, hapana, ambayo inatoka nje. Sisi kule hatutumii sukari ya Tanzania na hatuna hata wakala mmoja wa hivi viwanda kwenye mkoa wetu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana umeshaeleweka.

Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, mimi nasema bei ya Uganda ni shilingi 2,100 kwa leo.

**SPIKA:** Kwa pesa ipi?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ya Tanzania.

**SPIKA:** Shilingi 2,100 kwa pesa ya Tanzania.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya, ahsante.

Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, sisi tunapakana na Msumbiji, sukari ya Msumbiji ambayo inapita pale *boarder* tunanunua shilingi 1,900.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Spika, mimi naongelea sukari ya Malawi tunanunua shilingi 2,500 kule Malawi.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa...

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Spika, kwa kilo Malawi.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, hapa nchini sukari ni shilingi ngapi?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida tukiacha wakati wa madhara na matatizo, mlaji wa mwisho anakula sukari kati ya shilingi, hata sasa hivi sukari ya Kagera, *retail price* wanataka kuuza kwa shilingi 4,000. Wanauza shilingi 4,000 na risiti nilipeleka kwenye Kamati ya Maadili iliyonihoji juzi.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, narejea kwa Mheshimiwa Mwijage, vile viwanda ulivyosema vyenyewe vimekuwa kwa hiyo ndiyo maana bei iko chini kama hapa tumesikia Msumbiji shilingi 1,900. Vile viwanda vile ambavyo vimekuwa, vilikuwa vinahitaji muda gani ili tujue vya kwetu hapa kwa muda huo ambavyo tumekaa navyo vitakapofika umri huu vitakuwa vimekuwa na sisi Sukari iweze kushuka, hebu tusaidie Mheshimiwa Mwijage. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nilipokwenda *SADC* na Mheshimiwa Tax, alikuwepo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Aah, nawaeleza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tax alikuwepo, Mheshimiwa Profesa Mkenda alikuwepo, niliomba wanipe mpaka mwaka 2025

kusudi viwanda vyangu viweze ku-*compete*, *it is in record*. Mheshimiwa Tax, ndiyo alikuwa Katibu Mkuu...

**SPIKA:** Kwa hiyo, kwa maneno hayo nikiyachukua hayo hapo ni kwamba mwakani 2025 viwanda vyetu vitakuwa vimeshakuwa, bei ya sukari itashuka?

Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, wachumi wana kitu wanaita *ceteris paribus* kama masharti yale au vigezo nilivyokuwa nimeviweka vitazingatiwa, mwaka 2025 mtakuwa mme-*mature*. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmepata picha, kwa hiyo hii mamlaka yetu hii, Mamlaka ya Uhifadhi wa Chakula ya Taifa *(National Food Reserve Agency)* tunasubiri hivyo vifungu tutakapovipitia kesho ili huyu wakala apewe kazi inayomstahili, lakini pia wakati huo huo tumeshayasikia haya mawazo yote na tunaamini kama ambavyo Mwenyekiti wetu wa Kamati alizungumza hapa kwamba tutawafikia hawa wadau kupitia Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, tutawasikia kupitia huko. *(Makofi)*

Sisi kama nchi lazima tupige hatua na kwa kweli Bunge hiyo ndiyo kazi yetu, tunaposikia mambo haya na sisi tuwe tunajiweka humo. Tusijiweke kana kwamba sisi sasa kwenye mambo mengine sisi ni sehemu ya majirani, sehemu ya dunia, halafu kwenye mengine sisi siyo, sisi ni kisiwa hapana. Wananchi wote lazima watendewe haki na Bunge ndiyo hili hili, wawekezaji watendewe haki, wafanyabiashara watendewe haki na wananchi pia watendewe haki. *(Makofi)*

Kwa namna yoyote ile ambayo tutahitaji kutenda haki hiyo ndiyo kazi yetu. Sasa nianze na jambo moja hapa kabla ya hili tangazo la wageni, Mheshimiwa Tarimba, wakati anachangia alieleza kwamba Serikali katika huu Muswada ambao imeuleta

kwetu ili tuweze kupitia, kuishauri na baadaye kuweza kupitisha, Sehemu ya XXV inayohusu *Amendment of the Value Added Tax Act,* kifungu cha 93 kinasema; *The principal Act is amended in section 2* maana yake *Value Added Tax Act* ndiyo inakuwa *amended*, inasema *by adding in the appropriate alphabetical order the following new definitions*: *"gaming supply" means a supply of gaming activities as defined under the Gaming Act.*

Sasa alikuwa amesema hii sehemu inatoa tafsiri ya *gaming supply* ambayo inaweza kuwa pengine inaingilia ile kesi ambayo ipo Mahakamani, ambayo inauliza pamoja na mambo mengine, lakini inauliza maana ya hii *gaming supply*.

Sasa alinipa hapa mbele niweze kupitia siyo hukumu, lakini nipitie kile ambacho kipo mbele ya Mahakama kwa ajili ya Mahakama kufanya maamuzi.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, hii sehemu Bunge ni kazi yetu kutunga sheria na kwa namna kilivyoandikwa hiki kifungu kwa sababu kinaenda kwenye sheria nyingine, hapa hakijatoa maelezo ya ziada, maana yake hakuna namna yoyote ambayo Bunge kwa kutunga sheria hii itakuwa inaingilia uhuru wa Mahakama kwa maana ya kufanya yale wanayopaswa kufanya huko, ikiwa ni pamoja na kutoa hiyo tafsiri. Watakapotoa hiyo tafsiri basi na sisi tutaitazama halafu tuone kama tutaitungia sheria, lakini kwa maana ya kifungu hiki namna kilivyoandikwa hakitakuwa kwa namna yoyote kinaingilia ule mchakato wa hiyo kesi ambao upo mbele ya Mahakama.

Kwa hiyo, nimeona nilifafanue hilo kwa sababu Mheshimiwa Tarimba alilichangia, lakini pia nilimwambia anileteee hiyo taarifa aliyokuwa anaisema na mimi nimeipitia hapa mbele na haina huo mkanganyiko kama nilivyousema.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu taarifa tulizokuwa nazo ni kwamba leo tungemaliza ama niseme kuanzia asubuhi tulipoletewa hoja hii na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kisha

Kamati yetu ya Bajeti kuleta hapa maoni ya Kamati, tumewasikiliza na michango ilivyokuwa inaenda tulikusudia kumaliza leo muswada huu, lakini hatujamaliza kwa sababu Kamati yetu ya Bajeti yapo mambo ambayo imepelekewa na Serikali kwa nia njema tu, kuna mambo ambayo wameona wayaongeze kwa sababu ya haya majadiliano ambayo imekuwa ikiendelea nayo pamoja na mambo mengine, lakini tunafahamu kumekuwa na changamoto na wafanyabiashara na kwa hiyo Serikali imekuwa ikizungumza nao, kwa hiyo yale ambayo tunaweza kuyafanyia kazi katika kipindi hiki Serikali imeomba hiyo nafasi na sisi tumewapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutafanya hili zoezi la kuhitimisha kesho, Mheshimiwa Waziri atahitimisha na kama kutakuwa na sababu ya yale ambayo yatakuwa yamekuja basi huenda kabla Mheshimiwa Waziri hajahitimisha tunaweza kutoa fursa fupi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kama kutakuwa na sababu, lakini kama vile vifungu vitakuwa vimeenda vizuri na tunaona kwamba tunaweza kuelezana tu vizuri kwenye Kamati yetu ya Bunge Zima basi tutaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tutamalizia kesho asubuhi kwa ajili ya kutoa nafasi kwa Kamati yetu ya Bajeti kuyatazama yale mapendekezo mapya ambayo Serikali imekuja nayo. Kwa hiyo, hiyo pia inatoa nafasi hata kwa yale ambayo pengine Kamati ilikuwa tayari imesema humu kwamba hawajakubaliana na Serikali hii ni nafasi pia kama ambavyo Serikali imeshasikia michango ya Wabunge huku pengine kuna mambo mengine itataka kufanya marekebisho watakuwa wanaruhusiwa pia kufanya hivyo, nimeona niliseme hivi ili wasiende huko wakawa wamejibana wanaweza kuyatazama hayo, halafu kesho tutafanya kazi ya kutunga hiyo sheria.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wapo nasi jioni hii, kwanza ni wageni 121 wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambao ni Taasisi ya Mtetezi wa Mama kutoka Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Bunda Vijijini, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 52 wa Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Biashara na Uchumi pamoja na Shule Kuu ya Sheria kutoka mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Songwe, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 28 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*

**27 JUNI, 2024**